Nipashe
Jumatatu Novemba 18, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580078
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




UKURASA 13



## Familia ya marehemu Balali yamwangukia Rais Magufuli

UKURASA 3

# Serikali yashtukia upigaji mabilioni ununuzi korosho

UKURASA 2



## WALIOCHOMA SHAMBA LA MWEKEZAJI WASAKWA

UKURASA 3

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Ajenda ya Kitaifa za Utafiti wa Mifugo, Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji ya mwaka 2020-2025 katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mjini Morogoro. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare (wa pili kulia), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kushoto) na Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda. Habari ukurasa wa 2. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Scan Hapa
Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

# Mkapa: Utitiri wa vyama hatari kwa demokrasia

UKURASA 2

MICHEZO MAXIME ATAKA TATU ZA JUU LIGI KUU BARA UK. 31 MAONI, KATUNI UK.6

# Mpina aizindua ajenda ya kitaifa utafiti wa mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amezindua ajenda ya kitaifa ya utafiti wa mifugo, uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji ya mwaka 2020-2025 na kutangaza kuzifumua na kuzi-ibua tafiti zote zilizofanywa na wasomi na kutelekezwa kwenye makabati miaka ya nyuma.

Kutokana na hali hiyo, zitaingizwa kwenye mfumo rasmi wa matumizi ili kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na maendeleo.

Pia agenda hizo zitaleta msisimko mpya wa kufanya utafiti nchini na kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na maendeleo tofauti na ilivyokuwa kipindi cha nyuma ambapo tafiti nyingi zilifanywa na kutelekezwa kwenye makabati na watafiti mbalimbali wakiwamo Wanafunzi wa Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu (PHD) katika vyuo vikuu mbalimbali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ajenda hizo kitaifa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Mazimbu mjini Morogoro, Waziri Mpina aliziagiza Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) kubadilika ili kufanya tafiti kwa vigezo vilivyowekwa na kuleta mabadiliko chanya katika sekta za mifugo na uvuvi nchini.

Waziri Mpina alisema chimbuko la kuandaliwa kwa ajenda hizo za utafiti ni baada ya kubaini kuwa ajenda zilizokuwapo awali za mifugo na uvuvi zilishindwa kuibua na kuzitumia tafiti zilizofanywa kuchochea mabadiliko kwenye sekta hiyo muhimu ya uzalishaji.

Pia ajenda za utafiti zilizokuwapo za mifugo na uvuvi hazikuwa na utaratibu wa kuzitambua, kuziorodhesha na kuzitumia tafiti zinazofanywa na wanafunzi wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu, lakini sasa ajenda za utafiti zilizozinduliwa zimeweka utaratibu wa namna ya kuzitambua, kuziorodhesha na kuzitumia tafiti za wasomi hao.

"Haiwezekani tafiti za wasomi wa kiwango cha juu kiasi hicho wanazozifanya wakati wa kukamilisha masomo yao ziishie kupata alama za ufaulu na kutupwa

INAENDELEA UK. 8

# Serikali yashtukia upigaji mabilioni ununuzi korosho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameunda timu ya watu wasiozidi watano kwa ajili ya kuhakiki uuzaji na ulipaji wa korosho kwa wakulima katika msimu wa kilimo 2018/19, baada ya kubaini kuwapo na madudu kwenye malipo hayo.

Pia, amemwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuchunguza kiasi cha Sh. bilioni 53.2 kilichobaki kwenye akaunti ya Mfuko wa Wakfu wa kuendeleza zao la korosho uliofutwa, ambazo zilikuwa kwa ajili ya kujenga viwanda vitatu vya kubangua korosho na maghala.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Hasunga alisema katika msimu huo serikali ilinunua korosho kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, lakini imebainika kuwapo na madudu mbalimbali ikiwamo malipo hewa, kilo za uongo na wakulima feki huku akiwataka wakulima wanaodai kupeleka madai yao kwa timu hiyo na kamati za ulinzi na usalama.

Alisema timu hiyo itashirikiana na kamati iliyokuwa chini ya wizara hiyo ambayo iliundwa kwa ajili ya kuhakiki ununuzi wa zao hilo na kazi yake itakamilika ifikapo Januari 15, mwaka huu.

Hasunga alisema fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili hiyo zaidi ya Sh. bilioni 700 ni nyingi hivyo kuna umuhimu wa kujiridhisha kama zimewafikia wakulima.

"Tumeunda timu ya watu wasiozidi watano ili kushirikiana na kamati ya wizara iliyokuwa inahakiki, tuhakiki tuwe na uhakika wa korosho zilizopokelewa, zilizouzwa, fedha zilizopatikana na kama kuna upungufu ibaini na tume ihakikishe wote waliolipwa ni wale wanaostahili kulipwa."

"Tuhakikishe majina yaliyotoka kwenye vyama vya msingi kuja kwenye vyama vikuu na walioenda kwenye mfumo wa malipo kwenda benki ya TADB, na kwa kushirikiana na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko mpaka majina yaliyopelekwa kwenye benki, fedha zilizoingia ziliingia kweli kwenye akaunti za wakulima," alisema.

Kadhalika timu hiyo itaangalia kama kunaunyaufu ulijitokeza ili kutoa taarifa yenye uhalisia.

"Tumebaini kuna baadhi ya vyama vya ushirika, pamoja na kwamba kamati za ulinzi na usalama zilihakiki, lakini kuna udanganyifu katika malipo ya wakulima, kutokana na udanganyifu huo tunapata mashaka huenda baadhi ya wakulima waliolipwa sio sahihi," alisema.

Alitoa mfano wa Mkoa wa Pwani katika Chama cha Msingi cha Sangasanga Amcos ambacho alisema kilidanganya kikaonyesha wamekusanya kilo 218,000, lakini kilo halisi ni 212,000.

"Kuna kilo za uongo hapo, lakini walidanganya wakaweka kwamba korosho zilizopatikana zina ubora wa daraja la kwanza wakati kilo 244 zilikuwa hazina ubora huo, malipo hewa kwa baadhi ya watu siyo

INAENDELEA UK. 8



Mjumbe wa Mtandao wa Wanawake, Katiba na Uongozi, Maria Charles, akikemea vitendo vya ubaguzi, wakati akitoa maoni yake juzi, jijini Dar es Salaam, katika mkutano wa wadau wa uchaguzi kuhusu nafasi ya mwanamke katika uongozi, uliondaliwa na Mtandao wa Jinsi Tanzania (TGNP). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mkapa: Utitiri wa vyama hatari kwa demokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu, Benjamin Mkapa, amesema anaamini kuwapo kwa idadi kubwa ya vyama vya siasa nchini ni hatari kwa demokrasia.

Anaona utitiri wa vyama vya siasa nchi unadhoofisha ushindani, akidokeza kuwa vyama vingi vilivyopo nchini vimeanzishwa kwa maslahi ya wachache badala ya maslahi ya umma. Mkapa aliyeiongoza Tanzania kwa miaka 10 kuanzia mwaka 1995, anayasema hayo katika kitabu chake cha 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudi Langu).

Rais huyo wa awamu ya tatu anaeleza Tanzania ina vyama vingi vya siasa, lakini vingi vimeanzishwa kwa lengo la wahusika kujinufaisha kiuchumi badala ya kulisaidia taifa.

Anasema baadhi ya vyama havina hata idadi kubwa ya wanachama na muundo wake ni sawa na alichokiita familia.

"Uwapo wa vyama vingi vya siasa unadhoofisha demokrasia. Watu wanaingia katika siasa kusaka manufaa ya kiuchumi, siyo kwa nia tukufu ya kuwatumikia wananchi," anasema katika kitabu hicho kilichozinduliwa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Mkapa anaongeza kuwa hata kwenye uchaguzi mkuu uliopita, Tanzania ilikuwa na vyama vya siasa zaidi ya 20, lakini ni vitano tu vilivyofanikiwa kupata kura za kuviwezesha kuwa na uwakilishi bungeni.

Katika kitabu chake hicho, Mkapa anaeleza zaidi kuwa zamani Tanzania haikuruhusu wafanyabiashara kujihusisha na siasa, lakini sheria ilipolegezwa, ilitoa mwanya kwa kundi hilo kunufaika.

Anasema wafanyabiashara wengi wametumia mwanya huo kujiingiza kwenye siasa ili kulinda maslahi yao, akieleza kuwa hata bungeni, ni wabunge wachache wanaoingia kwenye chombo hicho kutetea wananchi.

Mkapa anasema nchi inakabiliwa na kikwazo cha wabunge na wasomi wake wengi kuhangaika kusaka fursa za posho na safari za nje badala ya kusaidia taifa lao.




Wanachama wakereketwa wa Chama Cha Mapinduzi( CCM) Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wakisherehekea uzinduzi wa kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa jana, katika Kata ya Ndanda mjini Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Familia ya Balali yamwangukia JPM

**Na Mwandishi Wetu**

FAMILIA ya marehemu Daudi Babali, imemwomba Rais John Magufuli kuisaidia kuokoa mali za Gavana huyo wa zamani wa Benki Kuu (BoT), ambazo inadai zimechukuliwa na 'wajanja wa mjini'.

Balali aliyeripotiwa kufariki dunia Marekani Mei 16, 2008, alikuwa Gavana wa BoT katika uwatala wa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Benjamin Mkapa.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, baadhi ya ndugu wa Balali, wakiwamo kaka na dada zake, walidai kupokwa kwa mali za ndugu yao huyo kulianza mwaka 2012 baada ya watu wasiojulikana kuvamia kwa mama yake Boko jijini na kuiba sanduku lililokuwa na nyaraka mbalimbali za marehemu.

Walidai kuwa ndani ya sanduku hilo kulikuwa na hati za mashamba, nyumba na viwanja vilivyokuwa mali ya Balali na mama yake mzazi, Rahel Vasolela Balali.

Yassin Mgunda, mpwa wa marehemu Balali, alidai upokwaji wa mali za Balali ulishamiri zaidi mwaka 2017, walipojitokeza watu wakidai ni wamiliki halali wa viwanja na mashamba ya marehemu mjomba wake.

"Mjomba kabla hajaondoka hapa Tanzania kwenda Amerika, kila kitu alikabidhi kwa bibi (Rahel). Bibi alipofariki dunia Februari 7, 2010, mama yangu aliteuliwa kuwa msimamizi wa mali zote za mjomba Balali.

"Mwaka 2017, mama aliitwa kwenda kutoa maelezo kwamba amepeleka taarifa za uongo Wizara ya Ardhi kuhusu baadhi ya mashamba na viwanja vya Balali.

"Tulipobaini kwamba kuna wajanja wanataka kujipatia mali za ndugu yetu, tuliliwasilisha suala hili kwa (Lazaro) Mambosasa (Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam) ili lichunguzwe.

"Malalamiko yetu ni kuhusu watu kujitokeza wakidai kiwanja cha Masaki, chenye ukubwa wa ekari mbili, ni mali yao ilhali tunajua kilinunuliwa kwa mzungu na bibi (mama yake Balali) kwa Dola za Marekani 72,000," alidai.

Mgunda alidai kuwa baada ya upelelezi wa timu ya Kamanda Mambosasa uliohusisha uhakiki wa hati za pande zote zilizodai kuwa mmiliki wa kiwanja hicho, jalada la uchunguzi liliwasilishwa kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua zaidi za kisheria.

"Ili kiwanja kisiendelezwe, Kamanda Mambosasa aliweka zuio kwenye hati, lakini tunashangaa kwamba kwa zaidi ya mwaka mmoja na nusu Ofisi ya DPP haijatoa faili la suala

INAENDELEA UK. 8

# Matumizi taasisi za elimu yashtukiwa

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imebaini fedha nyingi zinazotengwa kwa ajili ya vyuo vya elimu ya juu hazifiki kwa wahusika, ikiahidi kufanyia kazi suala hilo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, kwenye mahafali ya 54 ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kampasi ya Dar es Salaam.

Mahafali hayo yalihusisha wahitimu 2,439 katika fani mbalimbali kwa kiwango cha astashahada, stashahada, shahada na uzamili.

"Pamoja na uwekezaji ambao serikali inaufanya katika elimu ya juu, serikali inatambua bado fedha zinazotengwa katika bajeti ya sekta ya elimu hazikidhi mahitaji kulingana na hali halisi. Pia, kumekuwa na tatizo la fedha hizo kuhifadhi kwa taasisi zote za elimu ya juu," alisema.

Alisema wameanza kufanyia kazi na watahakikisha taasisi zote za umma zinazotoa elimu ya juu zinafaidika na fedha zinazotengwa kwa ajili ya sekta ya elimu bila kujali kuwa ziko katika wizara gani.

Kiongozi huyo alikipongeza chuo hicho kwa kusimamia mapato na matumizi yake vizuri na kupata hati safi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi ya Umma (PPRA).

Wakati Manyanya akiyasema hayo, Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) limeidhinisha mapendekezo ya mabadiliko ya kanuni za fedha za chuoni hapo ili kuzuia mianya ya matumizi mabaya ya fedha zinazotoka serikali kuu na zile zinazopatikana kutoka vyanzo vya ndani vya mapato vya chuo.

Mwenyekiti wa baraza hilo, Jaji mstaafu Damian Lubuva, aliyasema hayo juzi wakati wa mahafali ya 49 ya chuo kikuu hicho kikongwe zaidi nchini.

Alisema baraza hilo lilihidhinisha mapendekezo ya mabadiliko ya kanuni za fedha mapema mwaka huu.

Akizungumza katika mahafali hayo, Jaji Lubuva alisema baraza hilo halitamvumilia yeyote atakayeonekana kwa namna moja ama nyingine anajaribu kutumia fedha kinyume cha malengo yaliyowekwa au kujinufaisha mwenyewe.

Pia alisema vikwazo walivyonavyo ni mikopo ya wanafunzi na uhaba wa malazi na baraza hilo linavishughulikia, lakini akaiomba serikali kusaidia kuvitatua.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. William Anangisye, alisema katika mahafali ya mwaka huu, jumla ya wahitimu 8,313 (wanawake wakiwa 3,201, sawa na asilimia 38.5) wamefuzu na kustahili kutunukiwa tuzo mbalimbali.

Mhitimu wa Shahada ya Awali katika Elektroniki na Mawasiliano, Arnold Matemu, akisoma hotuba kwa niaba ya wenzake, alisema uboreshaji wa chuo hicho siyo tu utategemea serikali bali pia wale wote waliosoma chuoni hapo.

**Imeandikwa na Joseph Mwendapole na Romana Mallya, DAR**

# Msako waanza wanaodaiwa kuchoma shamba la Mzindakaya

**Na Gurian Adolf,** NKASI

SERIKALI wilayani Nkasi mkoani Rukwa imeliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwachukulia hatua watu waliowashawishi wakazi wa kijiji cha Nkundi kuchoma shamba la mwekezaji na mwanasiasa mkongwe, Chrisanti Mzindakaya, na kusababisha hasara ya Sh. milioni 95.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Said Mtanda, wakati akizungumza na wakazi wa kijiji hicho alipokwenda kushuhudia tukio hilo.

Alisema shamba hilo ni mali ya Mzindakaya na analimiliki kisheria hivyo wananchi wasijidanganye kuwa wanaweza wakamnyang'anya kwa nguvu na kuwataka wafuate taratibu za kisheria.

"Kitendo cha kuchoma shamba kimefanywa na wananchi wachache katika kijiji hicho, hivyo ninaliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka wote pamoja na watu wanaowashawishi kufanya hivyo ili sheria ichukue mkondo wake, na wakae wakijua kuwa serikali ya wilaya haipo tayari kuona wawekezaji wanahujumiwa, kama wananchi wana madai wafuate taratibu za kisheria," alisema.

Alieleza kuwa akiwa mlinzi wa amani amebaini migogoro inayotokea mara kwa mara na baina ya wananchi wa kijiji hicho na mwekezaji huyo inatokana na baadhi ya watu kuwatia hasira wananchi, kwenda kuvamia shamba la Mzindakaya na kufanya uhalifu wakiwaaminisha kuwa kwa kufanya hivyo watapewa shamba hilo jambo ambalo haliwezekani.

Katika mkutano huo baadhi ya wananchi, Apolinary Msuku na Jofrey Mashauri walimwomba mwekezaji huyo eneo la shamba, ili wananchi wapate ardhi ya kulima kwa kuwa hawana maeneo ya kulima ndiyo maana wamekuwa wakitumia nguvu bila ya kujua kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Naye diwani wa kata hiyo, Karasi Kipeta, alisema mwekezaji kwa upande wake alishawaambia kuwa wanaotaka kulima shamba hilo wajiorodheshe ili wakamwombe maeneo ya kulima na atawapatia, lakini wananchi hawataki wanachotaka ni kujimilikisha shamba hilo.

Shamba la Nkundi ambalo lilikuwa ranchi ya taifa lenye ukubwa wa hekta 6,000, aliuziwa Mzindakaya na linazungukwa na vijiji saba vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi pamoja Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, wananchi wa vijiji hivyo wanadaiwa kufanya vitendo vya hujuma ili mwekezaji huyo alirudishe na wapewe maeneo ya kulima.

# Katibu NLD apingana na mwenyekiti uchaguzi mitaa

**Na Sabato Kasika**

WIKI chache tangu Mwenyekiti wa Chama cha NLD, Oscar Makaidi, atangaze chama hicho kujitoa katika uchaguzi wa serikali za mitaa, upande wa katibu wa chama hicho, Tozy Matwanga, umeibuka na kudai kwamba kitashiriki.

Mwenyekiti huyo alikaririwa na vyombo vya habari akisema NLD kimeamua kujitoa katika uchaguzi huo kwa kuwa una kasoro kubwa na haziwezi kurekebishika katika muda uliobaki.

Hata hivyo, katibu huyo, katika barua yake kwa vyombo vya habari, yenye kumb namba NLD/PRESS/05/2019, amesema, chama hicho kinakanusha vikali kauli ya Makaidi, akidai kwamba hiyo ilikuwa ni kauli yake binafsi.

"Hakuna kikao chochote cha chama kilichoamua na kutoa maamuzi ya ovyo kama hayo. Chama kina taratibu zake za maamuzi kupitia vikao vya chama siyo maamuzi ya kiongozi mmoja," amesema Matwanga.

Amesema, NLD inaheshimu katiba yake, siyo kukurupuka ili kujifurahisha na kwamba wagombea wa chama hicho wamepata gharama za maandalizi yao ya uchaguzi na kwamba chama hakiwezi kuwapuuza.

"NLD itaendelea kushiriki uchaguzi kama ilivyopangwa, ila tunaitaka Tamisemi kurekebisha yale yote yaliyolalamikiwa kuwa ni kasoro za uchaguzi, ili uchaguzi uwe huru na haki," alisema.

Msimamo huo wa katibu umekuja, huku mwenyekiti wa taifa akiwa amewawatangazia wanachama na wagombea wote nchi nzima kutojihusisha kwa lolote kuhusiana na uchaguzi huo watakapotaarifiwa vinginevyo.

Mbali na NLD, vyama vingine vilivyotangaza kujitoa ni ACT-Wazalendo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Chauma, NCCR-Mageuzi, UPDP, Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Kijamii (CCK).

Kutokana na kauli za viongozi hao kutofautiana, huenda NLD sasa ikabaki njiapanda, wakati huu, ambao kampeni za uchaguzi huo zimeanza.

# TRA yafikia zaidi ya wafanyabiashara 700

**Na Veronica Kazimoto,** MOROGORO

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imewafikia na kuwaelimisha zaidi wafanyabiashara 700 kupitia kampeni ya huduma na elimu kwa mlipakodi iliyofanyika mkoani hapa.

Lengo la kampeni hiyo ilikuwa ni kutoa elimu kuhusu masuala ya kodi pamoja na kusikiliza malalamiko, changamoto na maoni kutoka kwa wafanyabiashara hao.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa kampeni hiyo mwishoni mwa wiki, Ofisa Msimamizi wa Kodi Mkuu wa TRA, Julius Mjenga, alisema mamlaka hiyo ililenga kuwafikia wafanyabiashara 500, lakini mwitikio wa watu umefanikiwa TRA kuvuka lengo hilo na kuwafikia zaidi ya 700.

"Wiki hii moja ya elimu kwa mlipakodi, tuliwalenga wafanyabiashara wa wilayani, kumekuwa na changamoto ya kutokupata elimu ya kodi kwa wakati. Nashukuru tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu tumewaelimisha wafanyabiashara 774 katika kampeni hii," alisema Mjenga. "Tumefika karibu wilaya zote za mkoa huu wa Morogoro ambazo ni Malinyi, Ulanga, Kilosa, Mvomero, Kilombero na Gairo na kila mahali tulipopita tumepata mwitikio mkubwa kutoka kwa wafanyabiashara na wananchi mbalimbali."

Kwa upande wa wafanyabiashara waliotembelewa na TRA, wameishukuru mamlaka hiyo kwa kuwaelimisha masuala mbalimbali yanayohusu kodi na kuomba elimu hiyo iwe endelevu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafanyabiashara hao walisema, TRA ya sasa siyo ile ya zamani kwa sababu sasa hivi maofisa wake wako karibu na walipakodi na hawana tabia ya kufunga biashara zao.

"Zamani mtu alikuwa akisikia watu wa TRA wanakuja, anafunga duka anaondoka, lakini siku hizi, TRA wamekuwa marafiki, wanatuelimisha na wala hawafungi biashara zetu, kwa kweli tunashukuru sana," alisema Eleonora Kisimba, mfanyabiashara wa duka la nguo wa wilayani Mvomero.

Naye Stanphord Mjumbe, mfanyabiashara wa duka la vifaa vya ujenzi wilayani Gairo, alisema kampeni ya elimu kwa mlipakodi ifanyike mara kwa mara kwa sababu wafanyabiashara wengi hususani wadogo hawajasoma hivyo wanahitaji kuelimishwa zaidi haki na wajibu wao katika ulipaji kodi.

Wafanyabiashara hao pia wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania kurejesha kodi ya zuio kwa wamiliki wa majengo kwa kuwa baadhi yao hawataki wapangaji kuzuia asimilia kumi na kuiwasilisha TRA.

Vilevile, wameomba kuelimishwa jinsi ya kulipa kodi ya mapato kwa awamu mara tu wanapokadiriwa kodi hususani kwa wafanyabiashara wapya kwa kuwa wengi wao wanapitiliza tarehe za kulipa kodi hiyo kwa kukosa uelewa.

Kampeni ya huduma na elimu kwa mlipakodi imemalizika jana na ilifanyika katika mikoa ya Morogoro na Pwani kwa wafanyabiashara kupata fursa ya kutembelewa katika maduka yao na wengine kuhudhuria semina kwa ajili ya kuelimishwa masuala mbalimbali yanayohusu kodi.



Kazi ya usimikaji nguzo ikifanyika katika Kijiji cha Mwasubuya wilayani Bariadi, Mkoa wa Simiyu kupitia mradi wa usambazaji umeme vijijini wa Awamu ya Tatu, mzunguko wa kwanza (REA III). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TGNP yawapa ilani wadau wa uchaguzi

**Na Sabato Kasika**

WADAU wa uchaguzi na uongozi juu ya nafasi ya mwanamke katika uchaguzi, wamekutana kujadili kwa kina jinsi ya kumwezesha mwanamke kushiriki kikamilifu katika chaguzi mbalimbali.

Uchaguzi unaolengwa ni wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ambao mwanamke naye anatakiwa kuwania nafasi ya uongozi na kuchaguliwa bila kuwekewa mizengwe.

Mkutano wa kujadili suala hilo, ulifanyika Dar es Salaam juzi, ukisimamiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD).

Wadu wengine walikuwa ni wawakilishi wa vyama vya siasa, Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Ulingo wa Wanawake na Siasa.

Mbali na hao, wadau wengine katika mkutano huo walikuwa ni Mtandao wa Wanawake na Katiba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (Zec).

Akitoa neno katika mkutano huo, Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Lihundi, alisema, Tanzania inaelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2019, na Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

Alisema, TGNP imeandaa Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake inayohusu chaguzi hizo, ikilenga kutoa sauti za pamoja za wanawake na makundi mbalimbali (wanawake na wanaume), katika uwezeshaji wa wanawake kushiriki kikamilifu kwenye mchakato mzima wa uchaguzi na kuhakikisha ajenda yao inapewa kipaumbele katika mipango ya serikali inayopewa rdhaa.

"Chaguzi hizi zinafayika kukiwa na historia iliyowekwa katika nchi kwa kupata kwa mara ya kwanza Makamu wa Rais mwanamke (Mama Samia Suluhu Hassan) katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na mgombea mwanamke katika nafasi ya urais (Mama Anna Mghwira)," alisema Lihundi.

Alisema, chaguzi hizo zina umuhimu mkubwa kihistoria, katika harakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla, ndiyo maana TGNP ikaanda Ilani hiyo iweze kutoa mchango.

"Ilani hii ni nyenzo muhimu kwa wapigakura wakati wa kusikiliza wagombea wanapojinadi iwapo wamebeba madai haya au la, pia itatumika kuuliza maswali wakati wa kampeni na nyenzo muhimu ya ufuatiliaji na utekelezaji wa ahadi za wagombea vyama na serikali watakapoingia madarakani," alisema.

Katika mkutano huo, wadau walijadili mikakati ya kufanikisha chaguzi hizo, lakini baadhi

INAENDELEA UK. 8



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Wasichana Ndwika wilayani Masasi mkoani Mtwara, wakiangalia gari aina ya Nissan walilopewa msaada jana na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa. **PICHA: HAMISI NASRI**

# RC amaliza adha usafiri shuleni

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, ametoa msaada wa gari kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Ndwika iliyopo wilayani Masasi kwa ajili ya kutatua tatizo la usafiri shuleni hapo ambalo limedumu kwa muda mrefu.

Mapema mwaka huu, Byakanwa alifanya ziara katika shule hiyo na kuelezwa uwapo wa changamoto ya usafiria ikiwamo kubeba wanafunzi pale wanapougua na kuhitaji kwenda hospitali.

Hafla ya kukabidhi gari hilo aina ya Nissan ilifanyika jana katika viwanja vya shule hiyo na kuhudhuriwa na viongozi pamoja na watu mbalimbali.

Akizungumza baada ya kukabidhi gari hilo, Byakanwa alisema amefarijika kutoa msaada wa gari hilo kwa sababu ahadi yake imetimia ya kutatua changamoto ya gari la usafiri kwenye shule hiyo.

Alisema aliitoa ahadi hiyo baada ya kuguswa na uwepo wa changamoto ya ukosefu wa gari la usafiri, na kwamba ofisi yake na jitihada zake mwenyewe aliamua kuhangaika usiku na mchana ili kupata gari hilo.

Alisema gari hilo litumike kama inavyokusudiwa na lisibadilishiwe matumizi.

Byakanwa alisema kazi ya kwanza ya matumizi ya gari hilo ni shughuli za shule ikiwamo wanafunzi kulitumia kwenda hospitali wanapohitaji kufuata matibabu.

Hata hivyo, Byakanwa hakutaja thamani ya gari hilo na kueleza kuwa kikubwa ametimiza ahadi yake.

Mkuu wa shule hiyo, Pauline Ndomba, alisema uongozi wa shule na wanafunzi kwa ujumla wanamshukuru kwa kuwapatia gari hilo, na kuwa kwa muda mrefu wamekuwa katika mazingira magumu ya kusafiri pamoja na wanafunzi kushindwa kwenda hospitalini kwa wakati kutokana na ukosefu wa gari.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Changwa Mkwanzu, alisema gari hilo litasaidia kuondoa adha ya wanafunzi kutumia usafiri wa bodaboda hasa nyakati za usiku.

# Ushirika kujenga kiwanda tumbaku

**Na Shaban Njia,** DODOMA

UMOJA wa Vyama Vikuu vya Ushirika wa Tumbaku (TCJE) vimeazimia kuanzisha kiwanda cha kusindika na kuchakata tumbaku ili kuongeza thamani ya zao hilo.

Lengo lingine ni kupambana na changamoto ya ukosefu wa masoko kwa wakulima wa zao hilo kila msimu.

Hayo yalibaishwa jana na Mwenyekiti wa TCJE, Emmanuel, katika kikao kilichowakutanisha viongozi wa vyama vikuu vya ushirika kutoka mkoa wa Katavi, Chunya, Kigoma, Tabora, Urambo, na Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dk. Titus Kamani jijini Dodoma.

Alisema lengo la kuanzisha kiwanda cha kusindika na kuchakata tumbaku ni kuongeza soko duniani na kuuza bidhaa zilizoongezwa thamani ikiwa ni njia ya kutatua changamoto ya ukosefu wa masoko kwa wakulima wa zao hilo.

Charahani alisema, bei ya tumbaku imekuwa ikishuka kila msimu na kusababisha wakulima kupata hasara, na kuongeza ili kutatua changamoto hiyo, ni vema kuanzisha kwa kiwanda hicho ambacho kitakuwa kinanunua tumbaku moja kwa moja kutoka kwa wakulima au katika vyama vya msingi.

Alisema mwaka 2016/17 bei ya soko la tumbaku ilikuwa ni Dola 2.00, mwaka

INAENDELEA UK. 8

# Wanawake Kisarawe wachangamkia usajili TIN

**Na Mwandishi Wetu,** KISARAWE

IDADI kubwa ya wanawake wilayani Kisarawe Mkoa wa Pwani imejitokeza kujisajili Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kupata Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kwa ajili ya kutumbulika na kufanya biashara zao kwa uhuru na halali.

Hali hiyo ilijitokeza wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma, Elimu ya Kodi na Usajili wa Walipakodi inayoendelea katika mkoa huo na wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji zikiongozwa na idadi kubwa ya wanaume waliojitokeza kupata namba hizo.

Meneja wa Huduma kwa Mlipakodi kutoka TRA, Honesta Ndunguru amesema ni kweli kwamba idadi kubwa ya wanawake wamejitokeza kupata Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi katika Wilaya ya Kisarawe ikilinganishwa na wilaya zingine za mkoa wa Pwani walikopita.

Ndunguru alisema, TRA imevutiwa na mwamko wa wananchi wa wilaya zote katika mkoa huo na kuwapongeza waliojitokeza kupata huduma, elimu pamoja na kujisajili kuwa walipakodi.

"Kwa mwitikio huu, inadhihirisha kwamba elimu ya kodi tunayoitoa inawafikia walengwa na wanafuata sheria ya kodi inayomtaka kila mfanyabiashara kujisajili na kupata Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi inayotolewa bure na TRA," alisema Ndunguru.

Kwa mujibu wa Ndunguru kati ya wananchi 10 waliojitokeza kupata TIN, wanane kati yao walikuwa wanawake, tofauti na wilaya nyingine, idadi kubwa ilikuwa wanaume.

Baadhi ya wanawake waliojitokeza katika viwanja vya stendi ya zamani ili kusajiliwa, walisema wamepata mwamko kufuata sheria za nchi zikiwamo za kulipa kodi ili waweze kutumia fursa mbalimbali ambazo zionatokana na kutambulika na serikali kama vile kupata mikopo ya wajasiriamali na huduma zingine muhimu.

"Binafsi nimehamasika na kuja kupata TIN kwa sababu nimeelimishwa na maofisa wa TRA na nimeelewa umuhimu wa kujisajili kama mlipakodi na kulipa kodi kwa nchi yangu," amesema Fatma Omari.

Naye Sophia Ndume mkazi wa Kisarawe amesema wanawake wa Kisarawe ni wahangaikaji katika biashara ndiyo maana wamehamasika kwa wingi kuja kuchukua TIN ili wakafanya biashara zao kwa uhuru bila kubughudhiwa.

Zainess Madeng'ha ambaye ni mmiliki wa saluni ya kike, amesema amehamasika kuchukua TIN baada ya kupata elimu kutoka kwa maofisa wa TRA na kwamba huduma hiyo imesogezwa karibu na inapatikana bure.

TRA inafanya wiki ya elimu kwa mlipakodi katika mikoa ya Pwani na Morogoro kwa lengo la kusogeza huduma za ulipaji kodi karibu na wananchi, pia kusajili ili kuongeza idadi ya walipakodi nchini.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars Watanzania wanataka tatu za Libya kufuzu Afcon

**TAYARI** Taifa Stars ipo nchini Tunisia ikijiandaa kushuka dimbani kesho kuivaa Libya kwenye mechi ya pili ya Kundi J kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Cameroon 2021.

Stars itashuka dimbani ikiwa na morali wa hali ya juu wa kutaka kuendeleza ushindi baada ya kuanza vema kampeni hiyo kwa kuitungua Equatorial Guinea mabao 2-1.

Ushindi huo Stars iliyoupatia Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Ijumaa iliyopita, umeifanya kukaa katika nafasi ya pili kwenye Kundi J ikizidiwa tu kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa na vinara, Tunisia ambao waliichapa Libya mabao 4-1 siku hiyo. Hivyo, ushindi katika mechi hiyo ya kesho utaiweka Stars katika nafasi nzuri ya kuelekea kufuzu fainali hizo ambazo kila kundi linatoa timu mbili.

Tunaamini Stars inaweza kabisa kubeba alama tatu za kwa kushinda mchezo huo ambao ni kama hauna mwenyeji kutokana na Libya na yenyewe kuchezea ugenini nchini Tunisia kutokana na hali ya machafuko ya kisiasa yaliyopo kwao kwa sasa.

Kwa maana hiyo hautakuwa mchezo wenye presha kubwa ya mashabiki wa kuibeba Libya kutokana na timu zote kuwa ugenini, hali ambayo inatufanya kuamini kwamba timu itakayoonyesha kandanda safi ndiyo itakayopata sapoti zaidi uwanjani.

Lakini hata kama Libya watapata mashabiki wengi kutokana na ukaribu wao na Tunisia, hatuna shaka katika hilo kutokana na uzoefu mkubwa wa Stars wa kuhimili presha za mechi za ugenini, hiyo ni kutokana na kufanikiwa kuibuka na ushindi ugenini nchini Sudan baada ya kuichapa kwa mabao 2-1 na kutinga hatua ya makundi kuwania kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Si mechi hiyo tu inayotupa jeuri ya kutoa kauli hiyo, bali pia Stars imefuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) mwakani nchini Cameroon ikiwa ugenini nchini Kenya, kwa kuitoa Harambee Stars kwa changamoto ya mikwaju ya penalti.

Hatua inayotufanya kutokuwa na hofu kwa Stars kucheza na kupata matokeo ugenini, lakini uwezo ulionyeshwa na Taifa Stars katika mechi dhidi ya Sudan ugenini na kisha dhidi ya Equatorial Guinea ni sababu nyingine inayotufanya tuamini kurejea na ushindi ni jambo linalowezekana.

Kinachotakiwa kwa benchi la ufundi ni kuzidi kuwajenga wachezaji kisaikolojia kwa kuwapa mbinu zaidi kuelekea mchezo huo ambao tunaamini benchi la ufundi limeshajua namna Libya wanavyocheza.


Tunasema hivyo tukiamini kwamba Kocha Mkuu wa Stars, Etienne Ndayiragije na wasaidizi wake, Juma Mgunda pamoja na Sulemani Matola walikuwa na muda wa kutosha kuisoma Libya wakati ikicheza dhidi ya Tunisia Ijumaa saa nne usiku baada ya mechi ya Stars kumalizika.

Kilichobaki ni Watanzania kuendelea kuiombea Stars kushinda mechi yake hiyo ya pili ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu fainali hizo kwa mara ya pili mfululizo.

Nipashe hatutaki kuona tukilazimika kufuzu tena kwa presha kama ilivyokuwa wakati wa kuwania kufuzu Afcon 2019 nchini Misri, baada ya kusubiria hadi mechi ya mwisho dhidi ya Uganda na wakati huohuo tukiombea Cape Verde iifunge Lesotho.

Presha hiyo itatoweka tu kwa kumaliza biashara mapema hususan kwa kupata ushindi katika mechi hiyo ya kesho kabla ya Agosti mwakani kukutana na kigogo cha soka, Tunisia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tunaishangilia wote Stars, ikipoteza tuwe wote pia

Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** ni siku ya furaha sana kwa Watanzania baada ya kuwachapa Equatorial Guinea mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Ijumaa usiku, watu walitoka kwa hoi hoi na nderemo uwanjani mpaka majumbani kwao. Kwenye vibanda umiza nako kulilipuka shangwe kwa mashabiki wa soka kuishangilia timu yao ya taifa.

Kuna abiria waliokuwa kwenye mabasi na magari madogo waliokuwa wakitoka kwenye shughuli mbalimbali za kijamii, wengine kazini, wakirejea majumbani kwao usiku huo nao wakiwa wanasikiliza matangazo ya mechi hizo kwenye redio walionekana kulipuka kwa sauti za kushamgulia na vigelegele kwa kinamama. Kila Mbongo alifurahi. Watu waliongea lugha moja. Hakukuwa na Usimba, Uyanga wala Uazam. Huu ndiyo ule uzalendo uliokuwa unatakiwa na kuhimizwa tangu mwanzo.

Uzalendo huu unatakiwa udumishwe na kuendelezwa kwa mechi zingine zinazofuata bila kujali matokeo.

Tatizo kuna baadhi ya Wabongo ambao ni wengi, wana tabia ya kuwa vigeugeu. Stars inaposhinda kila kitu kinakuwa sawa na cha wote. Hakuna mtu anayetoa makosa, wala kulalamika kuwa kulikuwa na tatizo sehemu fulani. Ni kwa sababu tu timu imeshinda kama hivi sasa.

Kesho Stars itakipiga na Libya nchini Tunisia kwenye mwendelezo wa michuano hiyo hiyo ya kutafuta tiketi ya kufuzu Afcon nchini Cameroon mwaka 2021.

Tukishinda kama wote tunavyoombea furaha zitaendelea kwa Watanzania wote. Lakini itakapotokea kupata sare au kufungwa tatizo litaanza. Wabongo tutaanza kugeukana.

Baadhi watasikika hata kwenye redio wakimponda Juma Kaseja kuwa si kipa, badala yake arudishwe Aishi Manula. Na hili lilianza baada ya kufungwa bao la kwanza dhidi ya Equatorial Guinea, ila limefutika baada ya ushindi.

Kwanza huko mitaani na kwenye mitandao ya kijamii ndiyo balaa mara nyingi litakapoanzia. Utaanza kusikia iliyofungwa siyo timu ya taifa ni timu fulani kwa sababu tu ina wachezaji wengi wa klabu hiyo.

Wengine watasema timu haikushinda kwa sababu mchezaji fulani na fulani hawakuchanguliwa kwenye kikosi hicho.

Baadhi watasikika hata kwenye redio wakimponda Juma Kaseja kuwa si kipa, badala yake arudishwe Aishi Manula. Na hili lilianza baada ya kufungwa bao la kwanza dhidi ya Equatorial Guinea, ila limefutika baada ya ushindi.

Bado kuna wale watakaosema kuwa Kocha Etienne Ndayiragije hafai. Tatizo la Wabongo wengi timu inapokuwa haifanyi vema basi kila mmoja anakuwa kocha. Haikatazwi kutoa maoni, lakini yawe ya kujenga, na si ya kuzidi kuwachanganya watu na wasijue la kufanya.

Timu inapokuwa haifanyi vizuri maoni yaonekane kwa ya ushauri zaidi kuliko kulaumu, na hii italisaidia sana hata Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuchukua ushauri na kuufanyia kazi.

Kama ambavyo kwa sasa tupo pamoja kwenye furaha ya ushindi, ikitokea kwa bahati mbaya kama Stars haikufanya vizuri Wabongo tuwe wote kwenye huzuni.

Tushangilie na kuhuzunika pamoja huku tukitoa maoni ya nini kifanyike badala ya lawama zisizo na kichwa wala miguu na zisizotatulika.

## HABARI KITAIFA

# Kero hii stendi Segerea mpaka lini?

**Mhariri,**

*NITUMIE nafasi hii kutoa machache ya nafasi yangu kuhusiana na matumizi nisiyofurahia kwa stendi yetu ya mabasi ya Segerea, jijini Dar es Salaam.*

*Hivi sasa ukifika utakuta matumizi ya kituo yanakuwa katika mambo mbalimbali yasiyohusika, kwa lengo lake.*

*Sehemu ya kupumzika abiria, ndio panageuzwa pa wachuuzi wadogo kukalisha wateja wao kwa biashara za namna tofauti na wateja wanahangaika, mfano hai katika sehemu ya abiria waendao Chanika, Ubungo, Makumbusho na Kawe, hata Mnazi Mmoja.*

*Hata maeneo mengine kuna shida abiria wanataabika mno kwa kuwapo rundo la uchafu katikati ya stendi, chombo cha kuzoa taka kimewekwa katikati na kuelemewa.*

*Hayo yanatokea, mahali hapo kukiwapo mengi tu ya usimamizi wa kiserikali, mojawapo ni ofisi za serikali ya mtaa, pia watumishi wa serikali mahsusi wanaokusanya mapato na mengine ya usalama. Hapo ndipo kiulizo zaidi kinanikaa.*

*Nasema ni utamaduni kuwa na haki na wajibu, vitu viwili vinavyoendana. Kama kuna wanaofanya kazi ya kukusanya mapato na kusimamia eneo la stendi na Segerea kwa jumla, kulikoni wanashindwa kuangalia mabaya, baadhi hata hayahitaji gharama?*

*Kujiuliza swali dogo, kivuli cha stendi hadi kuachwa mali ya wajasiriamali wa kuuza chai na mahitaji mengine madogo, badala ya watumiaji wa msingi maana yake? Je, inahitaji gharama yoyote kulichukulia hatua?*

*Hapo pia ndio inaibua swali la msingi, kuhusu umuhimu wa walinzi na mamlaka za usimamizi waliopo stendi Segerea.*

*Au ndiyo miundombinu hiyo ambayo ni zao la kodi za wananchi, haikulengwa kwa wasafiri bali wajasiriamali na wateja wao na si abiria wanaoshinda juani, ilhali wamejengewa na Manispaa ya Ilala, stendi moja na ya kisasa.*

**Mwananchi,**
**Mtaa wa Migombani,**
**Segerea, Dar es Salaam.**




# Mkude, wenzake wajitafakari kwa kauli hii ya CEO wa Simba

**Na Adam Fungamwango**

AKIWA kwenye ziara katika chombo kimoja cha habari nchini, Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingiza amesema mchezaji wake Jonas Mkude ana uwezo wa kucheza Ligi Kuu yoyote duniani endapo tu ataacha masuala ya utovu wa nidhamu.

Mazingiza alisema hayo alipoulizwa juu ya wachezaji wengi wa Tanzania kushindwa kucheza soka sehemu mbalimbali Afrika na hasa Afrika Kusini, badala yake wamekuwa ni wa kuhesabu tu.

Akajibu kuwa suala la nidhamu ndiyo limekuwa likiwagharimu wachezaji wengi wa Kibongo kupata nafasi ya kucheza nje ya nchi, ikiwamo nchi za Kiafrika.

"Wachezaji wengi Tanzania wanashindwa kucheza soka Afrika Kusini na sehemu nyingine za Afrika kwa sababu nidhamu inawafelisha wengi.

Mfano Mkude, siyo kwamba ana uwezo wa kucheza Ligi ya Sauzi tu, ila ana uwezo wa kucheza popote pale duniani, kwa sababu uwezo anao ila anatakiwa kuacha mambo mengine nje ya uwanja," alisema Mtendaji huyo na kuongeza.

"Pale anapokuwa halali kwa wakati, hapumziki na muda anaotakiwa kufanya mazoezi hafanyi vizuri, lakini bado unamuona yuko vile, jaribu kuangalia kama angekuwa anafanya kila kitu kwa nidhamu ingekuwaje?" Akahoji waandishi.

Maneno haya ya Mtendaji Mkuu huyu raia wa Afrika Kusini hayawezi kupita bila kujadiliwa.

Ni maneno ambayo kwa haraka unaweza kuyachukuliwa kwa urahisi, lakini kama ukikaa na kuyachambua na kuyaangalia kwa jicho la tatu, ni mazito na yanafaa kufanyiwa kazi.

Ni kweli amewasifia wachezaji wengi wa Kitanzania kuwa wana vipaji na uwezo mkubwa wa kutandaza kabumbu, lakini kwa upande wa pili ameona kuwa wachezaji wengi wa Kibongo ni kama hawautilii maanani mpira, kwa sababu hawajitunzi na hawana nidhamu na mchezo wenyewe.

Kusema kuwa wengi wanashindwa kucheza ligi Sauzi kwa sababu ya nidhamu, hii inamaanisha kuwa Ligi ya Sauzi ni ngumu mno, lakini pia ina pesa nyingi ambazo wachezaji wanalipwa na ili mchezaji kukubalika kuchezea huko ni lazima ujitambue, nidhamu, kujinyima na kujitunza, kitu ambacho wachezaji wengi wa Kitanzania hawana uthubutu huo.

Mtendaji wa Simba akawa anamtolea mfano Mkude. Senzo ni CEO wa Simba, Mkude ni mchezaji wa Simba, hapa unaona kabisa kuwa tayari bosi huyo kwa muda mfupi tu tangu aje, ameshagundua kuwa mchezaji huyo ni mmoja wa vinara wa watovu wa nidhamu nchini upande wa wachezaji wao.

Pamoja na kumsifia kuwa kama anakuwa na uwezo mkubwa kama huu na hajitunzi, je, akiamua kujitunza kiuchezaji itakuwaje, lakini ni ishara ya hatari kwa mchezaji huyo kwani atakuwa akimulikwa zaidi.

Kama Mkude mwenyewe atakuwa amemsikia bosi wake, basi akae akijua kuwa endapo akiendelea na hali hii mbele ya safari, sidhani kama anaweza kuwa na maisha marefu kwenye klabu ya Simba.

Sidhani kama Senzo ambaye hata hana miezi sita anaweza kuvumilia kuwa na wachezaji wasio na nidhamu ndani ya klabu yake kwa sababu hata yeye mwenyewe amenukuliwa kuwa amekuja kuibadilisha klabu hiyo kutoka kuwa yenye malengo kama ya ridhaa na kuwa ya kulipwa, huku pia ikikaa kibiashara zaidi.

Klabu ya Simba huko inakoelekea na si muda mrefu inatarajia kuwa ni klabu yenye wachezaji wa kulipwa wenye kujitambua na kupambana ili kuwa na kikosi imara kitakachowafurahisha mashabiki na wanachama wa klabu hiyo na kuwafanya kutoka kuwa mashabiki na wanachama na kuwa wateja.

Kwa maana hiyo, klabu haiwezi kuvumilia kukaa na wachezaji wasiojua thamani ya klabu na wasiojitambua, hivyo yeyote yule mwenye tabia hii ndani ya klabu ya Simba kwa maneno ya Senzo kama hatobadilika, basi hana maisha marefu.

Kingine ni kwamba kumbe wachezaji wengi wa Tanzania wana uwezo mkubwa sana wa kucheza hata Ligi ya Sauzi na kwingine Afrika na duniani kwa ujumla, ila kinachokwamisha ni utovu wa nidhamu wa wachezaji wenyewe, hivyo inabidi sasa waanze kujirekebisha.

Ukiangalia hata Mbwana Samatta na Simon Msuva walipokuwa wakicheza Ligi Kuu Tanzania, hawakuwa na uwezo mkubwa zaidi na wa ajabu kushinda wenzao waliokuwa wanacheza nao. Kilichowabeba hadi kufika huko walikofika kwa asilimia kubwa sana ni kujitambua na nidhamu tu.

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Serikali yashtukia upigaji mabilioni

INATOKA UK. 2

wakulima, hawakuleta korosho pale kwenye chama cha msingi, lakini majina yao yapo kwenye malipo ya mwisho na wamelipwa," alisema.

**UDANGANYIFU KATIKA ULIPAJI**

Alibainisha kuwa fedha zilizolipwa kwa watu ambao sio wakulima ni Sh. milioni 222.3 kwa chama hicho.

"Hii ni kwa chama hicho kimoja tu, lakini kuna vyama vingine tumepata changamoto ya aina hiyo kule Tandahimba kama isingekuwa uaminifu wa watu waliokuwa wanahakiki kulikuwa na Sh. bilioni 1.6 zilikuwa za udanganyifu, na maeneo mengine kumeonekana na udanganyifu," alisema.

Vile vile, wamebaini baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kwa kushirikiana na viongozi wengine kutoa majina ya uongo na si halisi ya wakulima.

"Kabla ya kumaliza kulipa, na kumaliza msimu tukaona ni vyema tujiridhishe kwanza tani zote zilizopokelewa za korosho kwa vyama vyote kwa msimu huo, ndiyo hizo zote tulizopeleka kwenye mauzo na kama kuna upungufu wa tani nani aliyesababisha ili tuchukue hatua zinazostahili," alisema.

Pia watahakiki majina yanayotoka kwenye vyama vya msingi, wanatakiwa kulipwa kiasi gani kutokana na kilo alizouza ili kujua kama ndiyo walioliрwa.

"Kama sivyo nani kapindisha na wapi ili kuchukua hatua stahiki, pia tunataka kuhakiki kama kuna wakulima ambao hawajalipwa maana natumiwa meseji nyingi kuwa sisi hatujalipwa wakati tumeshatangaza malipo yote tumemaliza, pale Rais alipotoa Sh. bilioni 40 za kumalizia," alisema.

Hasunga alitaka kujua kama kuna mkulima hajalipwa ni nani na kwa sababu gani. "Tumeona hata kwenye ufuta mnunuzi anazidishiwa kilo kwa makusudi na njama zinafanya na viongozi wa vyama vya ushirika," alisema.

Alifafanua kuwa hadi mwisho wa msimu huo zilikuwa zimekusanywa tani 222,561.2 za korosho ghafi na thamani yake ilikuwa ni Sh. bilioni 723.8. "Korosho zilikuwa na madaraja tofauti tofauti, daraja la kwanza zilipatikana tani 204,476.1 ambazo zilikuwa na thamani ya Sh. bilioni 674.71, lakini daraja la pili zilipatikana tani 18,084.9, zenye thamani ya Sh. bilioni 47.7."

Kuhusu korosho ambazo zimeshalipwa ni tani 217,786 ambazo zina thamani ya Sh. bilioni 707.8.

"Tumelipa hizi korosho, lakini kuna mambo machache yamejitokeza, kwanza wananchi hawajamalizika kulipwa na azma ya serikali ni kulipa malipo ya wakulima wote."

Vile vile alisema: "Katika kikao cha mwisho tulichokutana na Rais, wakuu wa mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani kila mmoja aliulizwa ni kiasi gani unachodai wakulima hawajalipwa, kila mmoja alitaja kiwango kinachodaiwa na tukapata takribani Sh. bilioni 40."

Waziri Hasunga alifafanunua kuwa Rais aliruhusu fedha hizo zitolewe kwenda kumalizia malipo ya wakulima, lakini akasema hadi sasa malipo hayo hayajaisha kutokana na mambo machache ambayo yamejitokeza kwwa baadhi ya vyama vya ushirika, pamoja na kwamba kamati za ulinzi na usalama zilihakiki, lakini kuna udanganyifu.

**UKAGUZI WA CAG**

Waziri Hasunga alisema Desemba mwaka 2016, serikali ilifuta Mfuko wa Wakfu wa kuendeleza korosho na kwenye akaunti kulikuwa na Sh. bilioni 53.2 zilizokuwa kwa ajili ya kujenga viwanda vitatu vya kubangua korosho na maghala.

"Kazi nyingine ilikuwa ni kuendeleza zao la korosho, kilichojitokeza Bodi ya Korosho badala ya kutekeleza maagizo ya serikali walikiuka na walibadilisha matumizi," alisema.

Alisema kilichowashtua mwaka huu wakati minada inaendelea, waliagiza magunia wameleta madeni kwamba wanaidai serikali kutokana na kusambaza magunia 2017/18.

"Kuna kampuni inadai Sh. bilioni saba, nyingine bilioni tano, wanasema walisambaza magunia, wakati utaratibu ulikuwa mnunuzi ananunua na kulipia gunia, swali linakuja hizo fedha hazikulipa magunia na kwanini madeni yaje leo."

"Tulipoomba maelezo Bodi wakatuletea matumizi ya fedha zilizobaki kwenye mfuko wa zile Sh. bilioni 53.2, katika fedha hizo walitumia Sh. bilioni 28.1 kununua viuatilifu, kibaya zaidi wanasema wametumia Sh. bilioni 12.2 kununua magunia, sasa swali mnunuzi alikuwa analipia magunia, lakini kama walilipa madeni ya magunia kwanini kuwe na madeni leo, ukiangalia yana kiwango hicho hicho," alisema.

**MADUDU YABAINIKA**

Waziri Hasunga aliendelea kueleza kuwa wameamua kujiridhisha na fedha hizo na matumizi yake kwa kumwagiza CAG kukagua ili serikali ichukue hatua zinazostahili kutokana na kuwapo na madudu kwenye matumizi hayo.

"Kuna fedha zimetolewa kwenda kulipia madeni ya benki ya nyuma kwa vyama vya ushirika, Chama cha Tanecu kilipewa Sh. bilioni 1.87, Koecu kilipewa Sh. bilioni 2.12 kulipia madeni ya nyuma wakati zilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na maghala, kibaya zaidi eti wakati wanasimamia zoezi wamelipana Sh. milioni 638.9 watendaji wa bodi, zingine vikao vya wadau wamelipata fedha nyingi takribani Sh.Bilioni moja kuandaa vikao," alisema.

Hasunga alisema kumekuwa na mwenendo mzuri tangu kuanza kwa minada ya wazi na idadi ya wanunuzi wanaojitokeza ni kubwa huku bei zinaendelea kupanda kutokana na mahitaji makubwa ya korosho.

## Ushirika kujenga kiwanda tumbaku

INATOKA UK. 5

2017/18 Dola 1.75, mwaka 2018/19 Dola 1.72, na kubainishwa kuwa, kushuka kwa bei hizo kunaathiri mapato ya wakulima, halmashauri na Taifa. Charahani alieleza mwaka 2018/19 uzalishaji wa tumbaku ulikuwa ni kilo milioni 54, huku mwaka 2019/20 mahitaji ni kilo milioni 41 na kuongeza kuwa vyama vya msingi zaidi ya 76 vinaweza kukosa soko kwa msimu huu.

"Ili mkulima aweze kunufaika na tumbaku, tumeona ni muhimu viongozi tujadiliane na tume juu ya uanzishwaji wa kiwanda kwa malengo ya kuongeza uzalishaji wa zao hili na kupanua wigo la soko kwa kuuza bidhaa za tumbaku zilizochakatwa ndani na nje ya nchi," alisema Charahani.

Naye Kaimu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege, alisema, uamuzi wa kujenga kiwanda hicho utasaidia wakulima kuwa na uhakika wa tumbaku yao kununuliwa na kuongeza wigo wa wanunuzi wa tumbaku nchini.

Naye Dk. Kamani amewataka viongozi wa umoja huo kuendelea kufuatilia kwa karibu taratibu za kuanzisha kiwanda hicho ili sekta ya ushirika kupitia vyama vya ushirika viweze kushiriki kikamilifu katika kipaumbele cha Tanzania ya viwanda.

## TGNP yawapa ilani wadau wa uchaguzi

INATOKA UK. 4

wakidai kuonewa na Jeshi la Polisi, rushwa, ubaguzi na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Zahra Ali Hamad ni Naibu Katibu Ngombe ya Wanawake CUF, Zanzibar, ambaye alilitaka Jeshi la Polisi kufanya kazi bila upendeleo na kukumbusha kuwa bila utawala bora hakuna maendeleo.

"Waache uwanja wa kufanya siasa uwe tambarare badala ya kuegemea upande mmoja wakati nchi hii ni yetu sote na tunatakiwa kuijenga kwa kushirikiana bila upendeleo wowote," alisema Zahra.

Naye mwanaharakati, Gemma Akilimali, alisema umefika wakati sasa wanawake kuchagua wanawake wenzao wanaowania uongozi bila kuangalia vyama wanavyotoka, ili mradi wawe na uwezo wa kuongoza.

Kwa upande wake mwakilishi wa IGP, Inspekta Issa Asali, aliwataka wadau hao kufanya shughuli zao, ajenda ya kwanza iwe ni usalama, kwa vile usalama, amani na utulivu vikikosekana, hakuna ustawi wa jamii.

"Tusitake mambo yaharibike ndipo tuonyoosheane vidole, hivyo hata nyie asasi za kiraia, katika mikutano yenu shirikisheni askari wetu, wapo nchi nzima," alisema Inspekta Asali.

Akizungumzia rushwa ikiwamo ya ngono, mwalikishi kutoka PCCB, Mercy Manyalika aliwataka Watanzania waelewe uthamani wa kura zao kuliko vitu wanavyopokea na kuweka madarakani viongozi wabovu.

"Kwa wale wote watakaombana na kadhia hiyo ya rushwa wapige simu namba 113 wakiwa sehemu yoyote nchini, PCCB itachukua hatua haraka iwezekanavyo," alisema Mercy.

Naye Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mathew Mwaimu, aliwataka wadau wote watakaokumbana na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu, watoe taarifa.

## Mpina aizindua ajenda ya kitaifa utafiti wa mifugo

INATOKA UK. 2

kwenye makabati, leo kila mhitimu atalazimika kuandaa 'policy brief' ambayo itawezesha watumiaji na serikali kurekebisha au kuandaa sera na sheria," alisema Waziri Mpina (pichani).

Aliongeza kuwa ajenda za utafiti zilizokuwapo za mifugo na uvuvi hazikuwa na utaratibu wa kuweka kanuni ambazo zitahakikisha kuwa utekelezaji wa ajenda za utafiti unafanyika, lakini ajenda za utafiti iliyotangazwa inaweka kanuni zitakazotoa mwongozo na usimamizi wa utekelezaji na wajibu wa kila mhusika.


Aidha, Waziri Mpina alibainisha kuwa ajenda za utafiti zilizokuwapo za mifugo na uvuvi hazikuwa na utaratibu wa kuwaunganisha watafiti wa mifugo na uvuvi nchini, na hivyo kupelekea kila mmoja kufanya utafiti kivyake hali iliyosababisha jambo moja kufanyiwa utafiti na mtafiti zaidi ya mmoja na kukosa jukwaa la kuratibu na kuchambua tafiti zinazofanywa nchini.

"Ajenda ninayoizindua leo inakwenda kujumuisha watafiti na wataalamu mbalimbali waliobobea katika fani za mifugo, uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji ili kuyapitia matokeo ya utafiti, teknolojia zilizoibuliwa na utafiti na kuzisambaza kwa watumiaji kwa manufaa ya Taifa," alisema Waziri Mpina.

Pia Waziri Mpina alibainisha upungufu mwingine uliyomo kwenye ajenda za utafiti zilizokuwapo za mifugo na uvuvi ni pamoja na kutoweka msingi mzuri wa kusimamia watafiti na kufanya tafiti kulingana na mahitaji ya soko badala yake taasisi za utafiti na watafiti kufanya tafiti nyingi za nje na mambo muhimu ya wananchi yanayohitaji kufanyiwa utafiti kutelekezwa.

## Familia ya Balali yamwangukia JPM

INATOKA UK. 3



letu.

"Katika mazingira haya, tunaona Mheshimiwa Rais John Magufuli (pichani) atusaidie kunusuru mali za ndugu yetu. Rais wetu ameshajipambanua ni mtetezi wa wanyonge, nadhani hata ninyi waandishi wa habari mmeshangaa kutukuta tunaishi maisha ya aina hii ilhali ndugu yetu alikuwa Gavana wa BoT," alisema.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam (Mambosasa), akiri ofisi yake kupokea malalamiko hayo, akieleza kuwa iliyafanyia kazi na kukabidhi kwa DPP.

Hata hivyo, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, DPP, Biswalo Mganga: "Hatufanyi kazi kwa shinikizo, tuache tufanye kazi."

**MAKAZI NAIBU GAVANA**

Magret Balali, dada wa marehemu Balali, alidai wanasikitika kuona kila mali ya Balali iliyopo nchini wakijaribu kuigusa kwa sasa wanaambiwa ni mali ya mtu mwingine.

"Tunaomba Mheshimiwa Rais atusaidie, DDP atoe lile faili kwa sababu mbali na mali za Balali, pia linashikilia mali za marehemu mama yetu ambazo hatuwezi kuzitumia kwa sasa kutokana na zuio.

"Wakati kaka (Balali) anaanza kuugua, nilikuwa ninaishi naye kule Masaki. Ile nyumba aliniambia ni yake lakini sasa anaishi nafikiri Naibu Gavana, hatuna uwezo wa kuidai tena ile nyumba kwa sababu 'documents' (nyaraka) zote zimeshachukuliwa. Ndio maana tunaomba msaada wa Mheshimiwa Rais.

"Bila msaada wake, hawa watu wanaoibuka na kusema ni wamiliki halali wa mali za ndugu yetu, wengine wanasema walikuwa wake wa Balali, watatuweka mahali pabaya.

"Balali alikuwa na mke, raia wa Argentina aliyezaa naye watoto wawili; Rahel na Octavo ambao wote kwa sasa wanaishi Marekani na mama yao huyo. Mali zote za Tanzania alisema alikabidhi kwa mama yake ambaye ni mama yetu pia," alidai.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emmanuel Maganga, akikata utepe wakati wa uzinduzi wa duka jipya la Tigo 'Tigo Shop' mkoani Kigoma. Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Ziwa, Uthmaan Madati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni kununua kilo 250,000 tumbaku

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

KAMPUNI ya usambazaji wa mbolea ya Yara na pembejeo nyingine za kilimo, Petrobena East African Limited, imeahidi kununua tumbaku kwa wakulima wa Chama cha Msingi cha Ngolo, Kahama mkoani Shinyanga.

Imesema lengo ni kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli za kuwainua wakulima ili kufikia uchumi wa kati.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Kahama mwishoni mwa wiki,

Mkurugenzi Mtendaji wa Petrobena, Peter Kumalilwa, alisema kuwa kampuni yake itaendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika kuinua maisha na hali za wakulima kwa kuwapa soko la uhakika.

"Dhamira yetu ni kuhakikisha kuwa wakulima wa tumbaku wanainuka na kufaidika na kilimo wanachofanya, tumewasambazia mbolea kwa wakati na tunawajibika pia kuwatafutia masoko ya ya uhakika kwa mazao, alisema Kumalilwa.

Kumalilwa licha ya kuwaahidi kuwatafutia soko kwa tumbaku watakayoizalisha msimu ujao, amesema kampuni yake itanunua kilo 250,000 au zaidi ya hapo kwa tumbaku itakayokidhi ubora unaotakiwa.

"Kuna changamoto katika kupata soko la tumbaku, tunawaahidi kupeleka zao hili sokoni kwa msimu ujao na Petrobena itanunua zaidi ya kilo 250,000 kwa tumbaku itakayoandaliwa kwa ubora," alisema na kuongeza kuwa kampuni yake itaendelea kuunga mkono jitihada za serikali kwa kusaidia jamii kwa kadiri itakavyowezana. Mwenyekiti wa Kahama Cooperative Union (KACU), Emmanuel Peter aliishukuru kampuni ya Petrobena kwa jitihada

inazofanya za kusaidia jamii husasuni wakulima ili kujinasua katika lindi la umasikini.

"Tunawashukurua sana Petrobena kwa jitihada zenu za kuwaunganisha wakulima na fursa za masoko na uhakika wa pembejeo ikiwamo mbolea na wakati umefika kwa kampuni za kizalendo kama hii kuwaonesha wakulima njia nzuri za kuendesha kilimo ili kiwe na tija hali itakayochangia ukuaji wa uchumi kupitia viwanda, alisema Peter.

Peter aliiomba Bodi ya Tumbaku Tanzania kuendelea kutoa vibali kwa kampuni mbalimbali ili ziweze kununua tumbaku kwa lengo la kuondokana na hali ya kukosa wanunuzi kama ilivyojitokeza kwa miaka ya hivi karibuni. Godfrey Mkunga ambaye ni mkulima wa tumbaku alisema uwepo wa Petrobena umeleta matumaini mapya kwa wakulima wa zao hilo baada ya miaka kadhaa= ya kutokuwa na soko la uhakika na pembejeo.

Naye Meneja Mkoa wa Kitumbaku- Kahama, Albert Chale, licha ya kutoa shukurani zake kwa Petrobena, alitumia hadhira hiyo kuwataka wataalamu wa kilimo waache kukaa ofisini na kuwafikia wakulima ili waweze kuzalisha tumbaku bora.

# Wachina wafichua siri ya maendeleo endelevu

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Umoja wa Wafanyabiashara wa China nchini (CABCT), Xian Ding, amesema ili kufikia maendeleo endelevu ya kiuchumi, ipo haja ya kutiliwa mkazo wa ufaulu wanafunzi kuanzia awali hadi chuo kikuu.

Ding aliyasema hayo katika mahafali ya 55 ya darasa la saba ya Shule ya Msingi Mohoro, Rufiji mkoani Pwani, huku akiipongeza serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya kufundishia.

Akizungumza akiwa mgeni rasmi wa mahafali hayo, Ding alisema wakati wanafunzi wakisoma kwa bidii walenge kuanzisha biashara kubwa, kuajiriwa au kubuni teknolojia za kisasa katika kuendeleza nchi yao.

"Serikali chini ya Rais John Magufuli imeweka mazingira mazuri ya elimu ikiwamo elimu bure, sisi Wachina tutaendelea kusaidia kwenye jambo hili la elimu," alisema.

Akizungumza na wahitimu hao wa darasa la saba, aliwataka wazingatie elimu waliyoipata na watakayoendelea kupokea kwa sababu wazazi wao wamewekeza kwao.

"Ili uchumi uweze kukua mahali popote pale kunahitajika watu wabunifu waliobobea kwenye fani mbalimbali, hii itatokana na kusoma kwa bidii na kujituma muwapo shuleni," alisema.

Pia aliwaeleza kuwa wanatakiwa kusoma kwa bidii ili waweze kuwa viongozi bora baadaye wa kulijenga kujenga na kusimamia sera ya kukuza uchumi wa viwanda. Mwenyekiti wa huyo wa CABCT, pia ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Huatan Investment Group inayomiliki miradi ya uwekezaji nchini ikiwamo kiwanda cha kutengeneza chakula cha mifugo, kiwanda cha kuchakata betri zilizokwisha muda wake kilichopo Rufiji.

Aidha, katika kutekeleza sera ya kushirikiana na jamii inayomzunguka, Ding ametoa msaada wa viatu vya shule kwa wanafunzi wa darasa la tatu na nne na fedha taslim kama zawadi kwa wahitimu waliofanya vizuri.

Pia ametoa fedha kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Nyamwage waliokaa kambini kujisomea.

# Shule yakunwa na uwezeshaji Tasaf

**Na Elizabeth Zaya,** LUDEWA

SHULE ya Msingi Ngalawale katika Halmashauri ya Ludewa mkoani Njombe, iimeushukuru Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) kwa kuwajengea vyumba vya madarasa, nyumba ya mwalimu, ofisi ya walimu na matundu ya vyoo shuleni hapo.

Aliyetoa shukrani hizo ni mkuu wa shule hiyo, Beatrice Mtweve, alipokiwa akizungumza mbele ya maofisa wa Tasaf waliotembelea shuleni hapo, na kueleza kuwa kabla ya kujengewa vyumba hivyo vya madarasa, shule hiyo ilikuwa na vyumba vitatu tu lakini kwa sasa wanavyumba sita baada ya kusaidiwa vitatu na mfuko huo wa Maendeleo ya Jamii.

Alisema mbali na upungufu wa vyumba vya madarasa, pia shule hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa nyumba za walimu na upungufu wa walimu wenyewe.

"Hapa shule yetu ilipo hakuna hata nyumba za kupanga, kwa hiyo walimu wanalazimika kutoka umbali wa kilomita tisa kuja kazini, na ili ufike kazini ni lazima utumie pikipiki ambayo kwa siku ni Sh.7,500, kwa hiyo wanatumia gharama kubwa," alisema Mtweve na kuongeza:

"Hali hii kwa namna moja ama nyingine inahatarisha kupunguza ali ya kufanya kazi kwa walimu, kwa sababu endapo akikosa nauli ya pikipiki kuna uwezekano wa kushindwa kufika kazini."

Alisema pamoja na kujengewa nyumba moja ya walimu, lakini bado kuna uhitaji mkubwa wa nyumba hizo.

"Tunaishukuru sana Tasaf wametuona kwa jicho la tatu kwa kutushika mkono, wameonyesha njia lakini tunaiomba tena serikali iendelee kutuona ituongezee angalau nyumba tano za walimu," alisema Mtweve.

Aliishukuru Tasaf kwa kuwasaidia watoto waliokuwa wakiishi katika mazingira magumu yaliyokuwa yakichangia kurudisha nyuma maendeleo yao.

"Katika shule yetu, pia tunao watoto ambao wanatoka katika familia maskini zinazosaidiwa na Tasaf ambao kabla ya kuanza kusaidiwa walikuwa na maisha magumu, wakati mwingine walikuwa wanashindwa kufika shuleni kwa kukosa sare za shule, walikuwa wanajiona wanyonge na hali hii ilichangia wasifanye vizuri kwenye masomo, lakini kwa sasa tunaona wanafanya vizuri sana," alisema Mtweve.

# Wizara yafuatilia uhalali wa kodi kwa mwekezaji

**Na Patrick Chambo,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imesema inafuatilia uhalali wa kodi ya pango la ardhi ya Sh. 496,706,000 kwa mwekezaji Mark Colman Ngalo, mkazi wa Kijiji cha Mafui wilayani Pangani mkoani Tanga, kama utoWizara hiyo ilishatoa mwongoza wa Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 katika utozaji wa kodi za ardhi hapa nchini ili kuondoa dosari zilizopo katika ulipaji wa kodi kwa upande wa serikali na wamiliki wa ardhi nchini.

Kamishna msaidizi kanda ya kaskazini Leo Komba na Kaimu Kamishna Mkuu nchini, Wilsoni Luge na ofisa habari wa wizara hiyo, Hassani Mabuye, wamesema hayo kwa Nipashe nyakati tofauti walipokuwa wakijadili malalamiko ya mwekezaji Mark Colman Ngalo anayedai kutakiwa kulipa kodi ya Sh. 496,706,000

Viongozi hao wamesema lengo la wizara ni kuondoa malalamiko kwa wawekezaji ili kuwavutia wawekeze nchini na serikali iendelee kupata kodi zake, na kwamba wanafuatilia kama kuna mahali pamekosewa ili parekebishwe haraka. Mwekezaji huyo mwenye Kiwanja cha hoteli wilayani Pangani, amesema kutokana na hali hiyo, amevunjika moyo wa kuendelea kuwekeza kwa kumuunga mkono Rais John Magufuli aliyewataka wafuate sheria za nchi na kulipa kodi halali za serikali.

Maofisa hao wa wizara walisema mwishino mwa wiki kuwa endapo mwekezaji huyo aliingizwa kimakosa katika mfumo wa kodi kabla ya wakati taratibu hazijakamilika watafuta na kumwondoa katika mfumo ila kwa sasa kinachoendelea kwao ni wao kujiridhisha kama malalamiko hayo endapo yana ukweli na kwamba kazi hiyo ni rahisi.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, wawekezaji wenye maeneo yaliyo ufukweni mwa nahari maombi yao yanatakiwa kupitishwa na Kamati ya Ugawaji Ardhi ya Wizara inayoshughulikia mambo hayo.

Katika malalamiko ya mwekezaji huyo aliyoyatoa kwa katibu mkuu wa wizara hiyo tarehe Novemba 14, mwaka huu wizarani hapo na nakala kutumwa kamishna msaidizi kanda ya kaskazini, Ngalo amesema yeye ni miliki wa kiwanja namba 2 kilichopo Kijiji cha Mafui Pangani.

Anasema alipata barua ya kupewa (letter of Offer No 00112769) Desemba 21, mwaka 2007 yenye kumbu namba PA/2159/02. Hata hivyo, alipoomba kuandaliwa hati alielezwa kuwa hawezi kuandaliwa hati hadi maombi yake yakajadiliwe kwenye kamati ya kitaifa ya kujadili utoaji wa kiwanja hicho ndipo taratibu zingine za kiserikali ziendelee kama tangazo la serikali Namba 72/2001 na Sheria Namba 2001 sehemu ya C(iii) ilivyotoa mamlaka kwa kamati hiyo.

Alisema anahitaji hati hiyo haraka ili aweze kuchukua mkopo benki utakomwezesha kuendeleza kiwanja hicho.

Alisema kuwa aliwasiilisha maombi ya kufutiwa madai hayo katika Ofisi ya Kamishna Msaidizi Kanda ya Kaskazini Mei 2019, lakini maombi yake hayajafanyiwa kazi hadi sasa, hivyo kuwasilisha maombi yake kwa Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi kwa msaada wa haraka.




Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori (kushoto) na Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi, Omary Mtiga (wa pili kulia) wakifunua kitambaa kuashiria uzinduzi rasmi wa tawi jipya la NMB Mbezi Louis, juzi jijini Dar es Salaam. Kulia ni Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## Mbezi Louis wapata huduma za kibenki

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Mbezi Louis wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, wamenufaika kwa kusogezewa huduma za kibenki, baada ya kufunguliwa kwa tawi jipya la Benki ya NMB.

Benki hiyo imefungua tawi lake jipya katika eneo hilo ukiwa ni utekelezaji wa mpango wake wa kufikisha huduma za kibenki kwa Watanzania wengi ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

Ufunguzi wa tawi hilo unaifanya benki hiyo kuwa na jumla ya matawi matano ndani ya Wilaya ya Ubungo.

Akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa tawi hilo mwishoni mwa wiki, mkuu wa kitengo cha wateja binafsi wa NMB, Omari Mtiga, alisema uamuzi wa kufungua tawi hilo umetokana na tafiti mbalimbali zilizoonyesha kuwa Mbezi Louis ni eneo linalokuwa kwa kasi katika biashara.

"Tumeona eneo hili linakuwa kwa kasi sana kibiashara lakini wateja wetu bado wamekuwa wakilazimika kusafiri kilometa 15 wakifuata huduma zetu katika matawi ya Ubungo, Sinza, Mlimani City na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sambamba na kauli mbiyo yetu ya: Karibu yako, tumeona tufungue tawi hapa hapa," alisema.

Akifungua tawi hilo, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, alisema upatikanaji wa huduma za kibenki ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Ufunguzi wa tawi hili utasaidia kukuza idadi ya Watanzania wanaotumia huduma za kibenki ambao kwa hivi sasa wapo chini ya asilimia 20," alisema.

Aliipongeza NMB kwa kuja na njia za kidijiti za kufikisha huduma zake kwa Watanzania, akitolea mfano wa huduma inayowezesha watu kufungua akaunti ya benki hiyo moja kwa moja kwa kutumia simu za mkononi bila kulazimika kwenda katika tawi lolote la benki.

"Hivi karibuni, NMB imekuja na huduma inayolenga kuwahudumia waendesha bodaboda. Hii ni hatua inayostahili pongezi," alisema Makori.

Tawi la Mbezi Louis linaifanya NMB kuwa na jumla ya matawi 224 nchi nzima.

# Vituo vya mafuta vyatakiwa vifaa

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAMILIKI wa vituo vya kuuzia mafuta kisiwani Pemba wametakiwa kuweka vifaa madhubuti vya kuepuka maafa yanayoweza kutokea.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa ukaguzi wa vituo hivyo, Chakechake pamoja kituo kikuu cha mafuta Wesha, Naibu Mkurugenzi kutoka Kamisheni ya kupambana na Maafa Zanzibar, Mwadini Ali Mwadini, alisema hatua hiyo itawasaidia kupunguza gharama na hasara endapo kutatokea moto katika vituo vyao.

Alieleza kuwa utaratibu wa kutembelea vituo hivyo ni endelevu, kwani mwanzoni tu mwaka huu kamati hiyo ilipita na kuona mapungufu mengi katika vituo hivyo.

Wakiwa katika kituo kikuu cha kusafirishia mafuta ambacho kinamilikiwa na kampuni ya GAPCO huko Wesha, Naibu huyo aliiomba kampuni hiyo kuweka chupa za gesi kwa ajili ya kupambana na moto unapotokea, kwani chupa zilizopo sio madhubuti wala hazina nembo sahihi ya sehemu zinapotoka.

Aidha, aliiutaka uongozi wa kampuni hiyo kuweka sare maalum kwa wafanyakazi wake pale wanapoingia kazini pamoja na kuwapatia vifaa ambavyo vinahusika katika sehemu zao za kazi.

"Lakini pia kuwapatia mafunzo maalum wafanyakazi wa kampuni hii namna ya kutumia hii mitungi ya gesi, ili kujiokoa pale inapotokea hitilafu ya moto," alisema.

Awali, alivipongeza vituo vya mafuta vilivyopo Tibirinzi, Chakechake na Bakar Petrol Station kwa matengenezo makubwa waliyoyafanya.

Aidha, aliwataka wamiliki hao kushirikiana na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi pamoja na Kamisheni ya Maafa Pemba, ili kuwapatia mafunzo wafanyakazi wao.

Nae Ofisa kutoka kikosi Cha Zimamoto na Uokozi Pemba, Ali Abdi Hashim, alieleza kuwa katika vituo hivyo kuna baadhi ya vifaa ambavyo vimesambazwa na kampuni ambazo hazina sifa ya kuuza vifaa hivyo, na kuwa vinaharibika mwaka 2020, ingawa havina kitu chochote ndani.

Naye ofisa kutoka taasisi inayosimamia afya na usalama kazini, Juma Ali Makame, aliuomba uongozi wa kampuni ya GAPCO kuwafanyia uchunguzi wa afya wafanyakazi wake kila mwaka mara moja.

# Watuhumiwa kula fedha za kikundi watiwa mbaroni

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Arusha, inamshikilia mweka hazina wa kikundi cha ujasiriamali cha Imani kwa tuhuma za kutafuna Sh. milioni 39 za wanakikundi.

Wanakikundi 28, juzi walikesha wakilia nyumbani kwa mweka hazina huyo, anayejulikana kwa jina la Halima Mwidadi, mkazi wa Osunyai jijini hapa, baada ya kuambiwa kuwa fedha hizo walizokuwa wavunje kibobo na kugawana, zimepotea katika mazingira ya kutatanisha.

Wengine waliokamatwa na Takukuru ni Katibu wa Kikundi hicho Deogratius Seif, na Mwenyekiti wake Aisha Saidi, ambao walikamatwa jana na kuachiwa kwa dhamana huku mwekahazina huyo akiendelea kusota mahabusu ya polisi kwa sababu za kiupelelezi. Akizungumza kwa niaba ya wanakikundi wenzake, Aziza Abdalah, alisema wanakikundi hao waliitwa Takukuru kwa ajili ya kutoa maelezo ambapo kila mmoja alihojiwa kwa nyakati tofauti na walieleza kiasi cha fedha anachodai. Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Arusha, Frida Wikesi, alikataa kuzungumzia suala hilo, kwa kile alichodai kuwa ni sababu za kiupelelezi.

Alisema madai hayo wanayafanyia kazi, huku akikiri kwamba baadhi ya viongozi wa kikundi hicho wanashikiliwa. Wiki iliyopita, wanakikundi hao walijikusanya nyumbani kwa Mwidadi kwa lengo la kugawana faida Sh. milioni 39, hata hivyo mweka hazina huyo aliwajibu fedha zimetoweka katika mazingira ya mazingaombwe.

Mwanachama mwingine wa kikundi hicho, Grace Magala, alisema kikundi chao kilianzishwa miaka mitano iliyopita na hawakuwahi kugawana faida hadi juzi walipokaa na kukubaliana kugawana faida.

Alieleza kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na katibu wa kikundi hicho, Deogratius Seif, kikundi hicho hadi kuvunjwa juzi kilikuwa na faida ya Sh. milioni 39, ambazo zilipaswa kugawanywa kwa wanakikundi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Breweries Limited (TBL), Philip Redman (kulia), akihojiwa na Deogratius Kithama, kwenye mwendelezo wa kampeni ya Kibiashara Zaidi inayoendeshwa na East Africa Television na East Africa Radio. Kampeni hii ina lengo la kuchochea ukuaji wa shughuli za kibiashara nchini. **PICHA: EATV**

# Mavunde awapa mbinu vijana za kupata zabuni

**Na Cyinthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Anthony Mavunde, amewataka vijana kutumia ujuzi walionao kupata zabuni katika halmashauri nchini, ili kujikwamua kiuchumi.

Aidha, alisema serikali imeweka mazingira kwa vijana, kwa kupitisha sheria inayozitaka halmashauri hizo kutoa zabuni kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Akizungumza jijini hapa wakati wa ufungaji wa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Baraza la Taifa la Uwezeshaji, alisema vijana watumie ujuzi walionao ili kupata zabuni hizo, kwani serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, inatekeleza mipango mbalimbali za ukuzaji ujuzi ili vijana wazalishe mali.

Alisema 2019 hadi 2020 kupitia mpango wa taifa wa ukuzaji ujuzi jumla ya vijana 46,000 nchini watanufaika na kupatiwa mafunzo kujifunza kwa vitendo mahali pa kazi, kurasimisha mfumo usio rasmi wa elimu, kilimo cha kisasa kwa teknolojia.

Kwa mujibu wa Mavunde, asilimia 56 ni vijana ambao ni nguvu kazi, wameathiriwa na ukosefu wa ajira, tofauti na makundi mengine na kuwa kikwazo kwao cha kushindwa kufanya shughuli za ujasiriamali wenye tija na mafanikio.

"Kutokana na hali hii inasababisha washindwe kushiriki miradi ya kimkakati na fursa zinazojitokeza, hali ya ujuzi nchini bado ipo chini katika makundi yote, ndio maana serikali imetoa mafunzo kwa vijana, ili kufikia uchumi wa kati, kama ilivyobainisha dira ya maendeleo ya taifa 2025," alisema Mavunde.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, alisema vijana waliofanya mafunzo ya ujasiriamali ni 168 ambapo wanaume 109 na wanawake 59, ikiwa lengo kuu ni kuongezeka ajira nchini.

"Vijana hawa wamepata fursa hiyo kwa kupata mitaji mbalimbali ikiwamo mapato ya ndani ya halmashauri ambayo ni asilimia 10 kwa mgawanyo wa asilimia nne kwa vijana asilimia mbili walemavu na asilimia nne wanawake," alisema Kwitega.

Mratibu Mafunzo hayo, Flora Kajela, alisema hadi sasa vijana 1,390 wamenufaika na mafunzo hayo, katika mikoa nane, ikiwamo Dodoma, Ruvuma, Geita, Mwanza, Mbeya, Lindi, Tanga na Arusha, ambapo wenye ulemavu ni 83.

"Kwa miaka mitano tumewafikia vijana 10,000 kupitia programu mbalimbali za mafunzo ikiwemo kijana jiajiri,Ajira yangu,kliniki ya vijana wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu, JKT, mifuko ya uwezeshaji na watoa huduma," alisema.

Mmoja wa vijana waliopewa mafunzo ya ujasiriamali na ujuzi mbalimbali, Babu Sindyo, alisema kupitia mafunzo hayo ya siku tisa, yamemsaidia vitu vingi kwani alikuwa hajuwi jinsi ya kupanga biashara yake na mahali pa kupata mtaji.

# 'Tatizo ajira liwe fursa kiuchumi'

**Na Allan Isack,** ARUSHA

VIJANA wametakiwa kutumia tatizo la kukosekana kwa ajira kama njia ya kuanzisha biashara ndogo na kujishughulisha na kilimo ili kujikwamua kiuchumi.

Rai hiyo, ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwakilishi wa Mkuu wa Mtandao wa AgriProFocus Tanzania , Ernest Likiko, wakati akizungumza na vijana katika kongamano kilimo na mazingira.

Alisema kongamano hilo limewashirikisha vijana kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, lengo likiwa ni kuangalia fursa zilizopo katika nchi hizo,na kuzitumia kwa pamoja kubadilishana uzoefu.

Likoko alisema katika kongamano hilo, walijadiliana kwa kina kuhusu suala la mabadiliko ya tabia ya nchi, na kutafuta njia za kukabiliana na tatizo hilo.

Hata hivyo, alisema vijana walioshiki kwenye kongamano hilo, wametoka katika sekta ya kilimo na biashara kutoka katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema walifundishwa namna ya kufanyabiashara na kilimo sambamba suala la utunzaji wa mazingira ili kuepukana na tatizo la mabadiliko ya tabia ya nchi.

"Kongamano hili limeratibiwa na Shirika la SNV (Craft) kwa kushirikiana na mtandao wa AgriProFocus, limewakutanisha vijana zaidi ya 2,000 kutoka nchi za Kenya ,Tanzania na Uganda na wengine kutoka nje ya Bara la Afrika, ambao waliungana na sisi kupitia teknolojia video kwa lengo la kupata elimu kilimo na biashara, pamoja na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema Likoko.


Mwezeshaji Mkazi wa Mtandao huo, Hilda Okoth, alisema kongamano hilo limewaunganisha vijana wanaojishughulisha na kilimo na biashara.

Okoth alisema tatizo kubwa iliyopo katika sekta ya kilimo ni kuwapo kwa viatilifu ambavyo vinasababisha magonjwa kwa mimea na wakati mwingine yanasababisha kutokea kwa mabadiliko ya tabianchi.

Alisema vijana wengi hawana taaluma ya kukabiliana na matatizo yanapotokea kwenye shughuli zao za kilimo kutokana na uelewa mdogo waliyonao

Neema Mollel, mmojawapo wa washiriki, alisema kila mara kukiwapo kwa makongamano hayo, yatawasaidia vijana kupata elimu kuhusu namna ya kukabiliana na matatizo yanayojitokeza katika sekta ya kilimo.

Naye Tobiko Sambai, alisema kongamano hilo, limewafundisha na kuwapa mbinu za kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi, na kutambua madhara yake.



# Muwsa yapongezwa ukusanyaji mapato

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amesema hivi sasa analazimika kutumia nguvu nyingi kusimamia makusanyo ya mamlaka za maji nchini, lakini Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi Mjini (Muwsa), ndiyo inayompa 'amani' kwa uwezo wake wa kukusanya kati ya mamlaka saba alizoziwekea nguvu zaidi.

Alikuwa akizungumza jana mjini hapa, wakati akizindua Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi Mjini.

"Wakati wangu wote natumia nguvu nyingi kusimamia makusanyo kwenye mamlaka za maji, ziko ambazo zikitaka hata kufunga nati kwenye miradi zinakuja wizarani, Katibu Mkuu naomba fedha, nikasema biashara hii iishe. Mmepewa taasisi hizi lazima mkusanye kodi na kila siku tunavyoendelea nakuwa mkali zaidi."

"Mamlaka hizi kama tutazisimamia vizuri zina uwezo mkubwa sana, lakini bado tuko kwenye usingizi. Nataka kila bodi mpaka watendaji wabadilike na kuiga mfano wa Mamlaka ya Maji ya Moshi Mjini. Mimi baada ya kuingia katika Wizara hii niliamua kuzifuatilia mamlaka kama saba ambayo ni Dar es Salaam, Moshi, Arusha, Morogoro, Mbeya na mamlaka za maji ndogo ndogo za Kilwa na Makonde."

Alisema kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa Muwsa, inampa moyo wa kuendelea kukaa katika wizara hiyo hasa kutokana na takwimu kuonyesha kuna jitihada za kuongeza makusanyo yake kila mwezi.

"Mimi ukiniuliza, nasema Muwsa ina uwezo wa kukusanya Sh. bilioni 1.2 kwa mwezi na hilo halina ubishi, kwa sababu mwezi Januari 2019 tulikuwa tumekafika Sh. milioni 814," alieleza Mbarawa.

Bodi hiyo mpya ya Muwsa itakayofanya kazi kwa muda wa miaka mitatu, inaongozwa na Mwenyekiti wake, Prof. Jaffary Kidegesho ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Aron Joseph, alisema hali ya utoaji wa huduma ya maji kwa sasa inaridhisha, kutokana na kutoa huduma katika kata 21 zilizopo ndani ya Manispaa ya Moshi na Wilaya ya Hai na Moshi Vijijini.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, akizungumza kabla ya Waziri Mbarawa kuhutubia, alisema kulikuwa na utitiri wa mamlaka za maji 159 nchi nzima, lakini mamlaka hizo zimepungua na kufikia 83.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Muwsa aliyemaliza muda wake, Prof. Faustine Bee, ambaye kwa sasa ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), alimweleza Waziri Mbarawa kuwa mpaka wanaondoka katika nafasi hiyo, deni la ankara za maji katika taasisi za umma ni Sh. bilioni 2.16

Pia, alimweleza kuwa mkakati mahususi waliouacha mchakato wake uendelezwe na bodi mpya ni pamoja na upanuzi wa mabwawa ya majitaka yanayopokea majitaka kutoka maeneo mbalimbali ambao gharama zake zinafikia Sh. bilioni 7.6.

# Washikiliwa kwa tuhuma za kusafirisha madini

**Na Mary Mosha,** KILIMANJARO

OFSI ya Madini Kanda ya Kilimanjaro inawashikilia watu wanane kwa tuhuma kufanyabiashara bila kibali na kusafirisha madini mbalimbali yakiwamo ya vito na felispa kinyume cha sheria. Madini hayo yaliyokamatwa katika wilaya za Same na Moshi yanakadiriwa kuwa kilo 3,000 na vito 2,925.

Akizungunza na Nipashe, Ofisa Madini Mkazi Kilimanjaro, Fatma Kyando alisema walilazimika kufanya msako mkali katika Mkoa wa Kilimanjro wa wiki mbili na kuwakamata watuhumiwa hao.

"Tulifanya msako kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaofanya biashara ya madini kinyume na taratibu, Manispaa ya Moshi tuliwakamata watuhumiwa wawili waliokutwa na madini aina ya vito yenye uzito wa kilo 2,925," alisema Ofisa Fatuma na kuongeza:

"Pia tuliwakamata watuhumiwa wengine wawili katika Kata ya Njoro, Wilaya ya Same, wakiwa na madini vito kilo 65, huku watatu walikamatwa wakisafirisha madini ya felispa kutoka Simanjiro."

Ofisa huyo aliwataka wachimbaji wa madini na wafanyabiashara kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu za nchi zinazowataka kuuzia madini yote ndani ya soko la madini lililowekwa.

"Serikali imeweka sheria na taratibu za kuuza madini ndani ya soko na ikiwa mfanyabiashara yeyote atafanya vinginevyo atakuwa amevunja sheria hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa," alisema.

Elirenoti Msuya, mkazi wa Bomang'ombe, Wilaya ya Hai ambaye ni mfanyabiashara wa madini, aliiambia Nipashe kuwa serikali ilihakikisha inaweka mazingira rafiki ya wafanyabiashara na wananuzi wa masoko ya madini ili kulinda matumizi mabaya ya uuzwaji wa madini nchini.

"Ifike mahali wafanyabiashara wenzangu tukubali kufuata sheria na taratibu zilizowekwa tuweze kufanya biashara katika mazingira salama kiutendaji na kukuza pato lamkoa na nchi kwa ujumla," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, Julai 19, mwaka huu akifungua soko la madini katika Wilaya ya Same alikaririwa akisema sekta ya madini mkoani hapa inachangia pato la taifa Sh. bilioni 3.7.

Alisema fedha hizo zinatokana na mrahaba kwa serikali pamoja na ada ya ukaguzi kwa kipindi cha miaka sita 2014 hadi 2019, hali inayoonyesha Wilaya ya Same ina madini mengi ya vito na 'metal'.




Wahitimu wa fani mbalimbali katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Dar es Salaam wakimsikiliza Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya kwenye mahafali ya 54 ya chuo hicho mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara watakiwa kupenda michezo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAJASIRIAMALI nchini wameshauriwa kujikita katika michezo kama njia ya kujitangaza na kujenga uhusiano mzuri na wanaowahudumia (jamii) ili kunyanyua uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa.

Pia wameaswa kutengeneza bidhaa zenye ubora, na kufuata sheria na taratibu za nchi.

Ofisa mipango wa magazeti ya serikali, Joseph Laizer, alitoa rai hiyo kwenye mbio za 'Kiliwomen Run 2019' zilizoandaliwa na kikundi cha wanawake cha Kiliwomen Sports Club cha Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Alisema ni lazima kutambua kila fursa inayotokea katika sekta hiyo ni muhimu kufahamiana na watu wengine ili kuwa karibu na jamii na kuvutia wateja wao.

"Tunaweza kufanya biashara ila kama hatuna watu hatuwezi kufikia malengo, hatutakuwa na soko hivyo michezo isiwe kukimbia tu bali iwe njia ya kupata fursa zingine za kutangaza bidhaa zetu kwenye masoko mbalimbali ndani na nje ya Mkoa wa Kilimanjaro," alisema.

Mwenyekiti wa Kiliwomen Sports Club, Theresia Komba, alisema, klabu hiyo ni jinsia ya kike, lakini katika michezo wanajumuisha jinsia zote.

"lengo la mbio hizo fupi ni kujenga mtandao wa kibiashara na uhusiano mzuri na wadau ikiwa wao ni wajasiriamali wenzetu katika maeneo mbalimbali ya mkoa na taifa kwa ujumla," alisema Komba.

Mmoja wa washiriki wa mbio hizo mwenye ulemavu, Faustina Urassa, aliitaka jamii kuachana na dhana potofu ya watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye mambo ya kijamii.

"Serikali na jamii zinayotuzunguka zinawasahau watu wenye ulemavu...mimi nimejitokeza leo ili kuwaonyesha wadau mbali mbali kuwa licha ya ulemavu wetu, lakini tuna uwezo wa kushiriki kila fursa tunayopewa," alisema Faustina.

Queen Isack, alisema ushiriki wa mbio hizo unaweza kuleta mabadiliko kwenye biashara yake kutokana na kukutana watu wengi pamoja na kujifunza uzoefu kutoka kwao.

"Ninapokuja kwenye mashindano haya, huwa nakuja na bidhaa ninazotengeneza, napata oda nyingi ikiwa ni pamoja na kuuza... wapo wanaotoa ushauri ili kuboresha zaidi biashara zetu, tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kutuletea wataalamu wa biashara kila yanapoandaliwa mashindano mengine kama haya," alisema.

Nipashe
Spotika



**MAKOCHA WA5 WANAOLIPWA ZAIDI DUNIANI** UK. 20



# MSHIKEMSHIKE...

Kiungo wa Urusi, Roman Zobnin, akipata wakati mgumu wa kumdhibiti mshambuliaji wa Ubelgiji, Eden Hazard katika mechi ya kuwania kufuzu Euro 2022 iliyopigwa St Petersburg, Urusi juzi. Ubelgiji ilishinda 4-1. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

Katika mabao zaidi ya 700 Cristiano Ronaldo aliyofunga kwenye ngazi ya klabu na timu ya taifa, 442 (sawa na asilimia 63.1) alifunga kwa mguu wa kulia, huku mabao 129 (sawa na asilimia 18.6) akifunga kwa mguu wa kushoto na mabao 127 (sawa na asilimia 18.2) alifunga kwa kichwa, huku mawili akifunga kwa sehemu nyingine ya mwili. **Soma zaidi UK. 16& 17**

SOKA


Werner

# NYOTA 6 WAKUVAA VIATU VYA SUAREZ

**BARCELONA, Hispania**

KUMEKUWA na mjadala mkubwa wa nani atakayemrithi mshambuliaji Luis Suarez ambaye kwa sasa kiwango chake kinaelekea kwenye 'jua kuzama' pale Barcelona.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, wanakusudio la kuachana na Suarez hapo kwenye dimba la Camp Nou, lakini wanamtafuta mtu ambaye atakuwa mrithi wa muda mrefu wa raia huyo wa Uruguay.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2021 na anaweza kutaka mshahara mkubwa ili kubaki, lakini bila shaka Barcelona watakuwa wanatafuta mchezaji mwenye ubora wa kubeba mikoba yake.

Kwa uwezo wa Suarez kuondoka kwake kwenye kikosi kinachowajumuisha Lionel Messi, Antoine Griezmann na Ousmane Dembele, kwa vyovyote kutakuwa na pengo kwenye safu yake ya ushambuliaji.

Suarez tayari ana mabao nane msimu huu, hivyo mrithi wake pale Catalunya ni lazima awe mtu mwenye kiwango cha juu zaidi.

Makala haya inakuchambua wachezaji sita ambao Barca wanaweza kuwaona wanafaa kubeba mikoba ya Suarez, teleza nayo...

**Timo Werner**

Kwa sasa nyota huyu wa Ujerumani, Werner amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu ya Liverpool, lakini kwa miaka kadhaa dili hilo limeshindikana. Werner amefunga mabao 11 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, hadi sasa na amefikisha mabao 15 katika mechi 16 za mashindano yote.

Kama akitua pale Barca uwezo wake unaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho.

**Erling Braut Haaland**

Bila shaka, kumpata mtu ambaye amefunga mabao 26 katika mechi 18 msimu huu litakuwa jambo zuri zaidi. Barcelona wanaweza kujua machache kuhusu uwezo wa kufunga mabao wa kinda huyu mwenye umri wa miaka 19 akiwa pale kwenye klabu ya Red Bull Salzburg.

Haaland amekuwa mchezaji wa pili mwenye umri mdogo zaidi kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Karim Benzema, kufunga katika mechi zake tatu mfululizo kwenye mashindano hayo, yakiwamo mawili dhidi ya Napoli na moja dhidi ya mabingwa watetezi, Liverpool.

Licha ya kwamba ana uhusiano mzuri na Ole Gunnar Solksjaer wakiwa wote pale Norway katika klabu ya Molde, na kwamba ana nafasi kubwa ya kwenda Manchester United, lakini huyu anaweza kuwa mrithi sahihi wa Suarez pale Barca.

**Tammy Abraham**

Pengine inaweza kuwa kazi ngumu, lakini mtu pekee ambaye hana shaka yoyote na uwezo wa Tammy Abraham ni Abraham mwenyewe.

Mshambuliaji huyu wa England haogopi kujithibitishi yeye mwenyewe ubora wake, akiwa amezichezea timu kama Bristol City, Swansea na Aston Villa kwa mkopo. Kwa sasa katika umri wake wa miaka 21, amekuwa akitamba kwa kufunga mabao kwenye Ligi Kuu ya England, akishika nafasi ya pili nyuma ya Jamie Vardy.

Abraham ni mchezaji imara na mwenye nguvu, ingawa kuondoka pale Chelsea inayonolewa na kocha Frank Lampard linaweza kuwa jambo gumu, lakini Barcelona wakimpata huyu anaweza kuwa msaada mkubwa kwao.

**Habib Diallo**

Pengine anahitaji msimu mzima wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, ili kuonekana zaidi kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, lakini Habib Diallo ni nyota chipukizi mwenye uwezo na kipaji cha hali ya juu.

Aling'ara kule kwenye Ligue 2 msimu uliopita akiwa na mabao 26 katika mechi 37 alizocheza akiwa na Metz. Kwa sasa yupo nyuma ya Wissam Ben Yedder wa Monaco na Moussa Dembele wa Lyon kwenye orodha ya kufumani nyavu akiwa na mabao nane.

Katika umri wake wa miaka 24, anaweza kuwa mmoja wa wachezaji wenye nafasi kubwa ya kuvaa viatua vya Suarez.

**Harry Kane**

Ndio, huyu ni mtu muhimu zaidi pale Tottenham. Bila shaka yoyote Harry Kane amejithitibishia yeye mwenyewe kwamba ni mfungaji mzuri zaidi wa mabao.

Nahodha huyo wa England bado hajafikia mafanikio anayoyataka pale Tottenham Hotspur.

Kane ambaye alikuwa mfungaji bora kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 kwa kutwaa Kiatu cha Dhahabu, anaweza kwenda Barcelona na kupata yale mafanikio ambayo amekuwa akiyasaka kwa muda mrefu. Katika umri wake wa miaka 26, kuna nafasi kubwa kwake kwenda kutua pale Barca.

**Moussa Dembele**

Pengine unaweza kujiuliza wachezaji wangapi walianzia kule Fulham na kuhamia Barcelona?

Pengine hakuna. Jari Litmanen alifanya kwa njia yake.

Hata hivyo, Moussa Dembele anaongoza kwenye Ligue 1 katika orodha ya kufumania nyavu kwa sasa akiwa na mabao tisa kwa jina lake.

Anaweza kuwa na thamani kubwa ya pauni milioni 19.7 ambazo Lyon walilipa Celtic mwaka 2018, lakini rekodi yake ya kuzifumania nyavu ni ya kuvutia na pengine anaweza kuwasaidia Barca.

**JE, WAJUA?**



TANGU Agosti 2018, Sadio Mane ameifungia Liverpool mabao 22 kwenye Ligi Kuu England katika Uwanja wa Anfield - idadi ambayo ni kuwa zaidi kuwahi kufungwa na mchezaji mmoja katika uwanja mmoja.

# MICHEZO



Mshambuliaji Mbwana Samatta (kushoto) akiwatoka wachezaji wa Equatorial Guinea wakati wa mchezo wa kufuzu AFCON 2021 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KILICHOIBEBA TAIFA STARS KWA EQUATORIAL GUINEA

**Na Adam Fungamwango**

TAIFA stars kwa sasa inakamata nafasi ya pili kwenye Kundi J, baada ya kuifumua Equatorial Guinea mabao 2-1 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar Salaam usiku wa Ijumaa iliyopita.

Ilikuwa ni siku ya furaha kwa Watanzania, ambao wanatafuta tena kwa mara ya pili mfululizo tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) mwaka 2021 zitakazofanyika nchini Cameroon.

Mwaka huu, Stars ilifanikiwa kufuzu na kucheza fainali hizo zilizofanyika nchini Misri. Mara ya mwisho Stars kufanya hivyo ilikuwa ni 1979 ilipofuzu na ikacheza fainali zake 1980 nchini Nigeria.

Stars inakamata nafasi ya pili kwa pointi tatu, mabao mawili, ikiwa imefungwa moja ikizidiwa tu kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa na Tunisia ambayo siku hiyo hiyo ikiwa nyumbani, ilitoa kipigo cha mabao 4-1 dhidi ya Libya.

Kesho, Stars itakuwa uwanjani kwenye Uwanja wa Mustapha Ben Jannet nchini Tunisia kucheza dhidi ya Libya ambayo haichezi nchini kwao kutokana machafuko ya kisiasa.

Haikuwa rahisi kwa Stars kupata ushindi nyumbani kwani ilikuwa kwenye wakati mgumu kuanzia dakika ya 15, wageni walipopata bao lililofungwa na Pedro Obiang na kudumu hadi mapumziko.

Kipindi cha pili, Stars ilirejesha hai matumaini kwenye dakika ya 69, Simon Msuva aliposawazisha bao na dakika ya pili ya nyongeza kati ya nne zilizoonyeshwa, Salum Aboubakar 'Sure Boy' aliipata Stars bao la pili.

Mwandishi wa Makala haya anachambua kilichoifanya Stars ishinde mechi hiyo, na ugumu wa mechi hiyo ulivyokuwa, komaa nayo...

**1. Kumkamia zaidi Samatta**

Benchi la ufundi la Equatorial Guinea lilionekana kumfungia kazi zaidi Mbwana Samatta.

Ilionekana kabisa kuwa Samatta ndiye alikuwa tishio kwao, hivyo aliwekewa walinzi wawili na wa tatu alikuwa kama wa akiba kuangalia chochote kile kitakachotokea.

Mabeki wa timu hiyo ambao ni warefu na wenye nguvu, walionekana kula sahani moja na Samatta kwa kiasi kikubwa walifanikiwa kumfanya asifurukute, ingawa hilo kwao baadaye lilikuwa kosa ambalo walilijutia kwani kulitoa nafasi kwa Msuva na wenzake kufanya kweli.

**2. Kutomjali sana Msuva**

Kosa walilolifanya wageni ni kumchukulia poa Msuva. Kwa siku za karibuni Msuva ndiye amekuwa mhimili mkubwa wa mafanikio ya Stars kuliko hata Samatta. Nadhani walishindwa kulijua hilo.

Wakati wako bize na Samatta, Msuva ndiye alikuwa akiwahenyesha kwenye wingi ya kulia na kusababisha madhara mengi na kama Stars ingekuwa makini ingevuna mabao mengi.

**3. 'Sub' ya Nchimbi na Dilunga**

Kocha Mkuu wa Stars, Etienne Ndayiragije alifanya mabadiliko bora zaidi kwenye mechi hiyo, alipowatoa Hassan Kessy dakika ya 50 na kumwingiza Ditram Nchimbi dakika ya 50 na Farid Mussa dakika ya 75 na kumwingiza Hassan Dilunga.

Mabadiliko haya kwa kiasi kikubwa ndiyo yaliyoleta chachu ya ushindi huo ambao Watanzania wote wanajivunia.

**4. Nchimbi aliwachanganya mabeki**

Kuingia kwa Nchimbi na purukushani zake, ziliwafanya mabeki wa Equatorial Guinea kuchanganyikiwa wasijue wamkabe nani kati ya Samatta na Nchimbi.

Ikumbukwe kuwa Stars ilikuwa ikicheza na straika mmoja wa kati, hivyo kuingia kwa mshambuliaji huyo kuliongeza namba na kufanya wawe wawili, huku Nchimbi alionekana sasa ni hatari kwao zaidi kuliko Samatta.

Hii iliwafanya sasa waanze kukatika na kuanza kuachia mianya ya madhara golini kwao mara kwa mara.

**5. Dilunga alimsaidia Mzamiru 'kukichafua kati'**

Kwa siku za karibuni, Mzamiru Yassin amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu. Baadhi ya wachunguzi wa masuala ya michezo wanasema kuwa huenda ana kiwango kizuri zaidi kuliko hata alichokuwa nacho Mtibwa Sugar na hata kile cha Simba mwanzoni wakati anajiunga.

Japo alikuwa anafunga mabao, lakini hakuwa na nguvu, kasi, pumzi na ari ya kupambana kama hivi sasa.

Awe Simba au Stars, Mzamiru kwa sasa ni tegemeo kubwa kwenye kiungo cha kukaba, huku pia akisaidia kwenye mashambulizi pamoja na Salum Aboubakar.

Kwenye mechi hiyo baada ya kufanya kazi kubwa kipindi cha kwanza, aliongezewa nguvu kwa kuingizwa Dilunga, kiungo mshambuliaji mwenye kasi na nguvu ambaye alikuja kumsaidia pale kati na hawakupata tabu sana kwa sababu wanajuana kutokana na kucheza kwenye klabu moja ya Simba.

**6. Kujihami kwa Equatorial Guinea**

Ilionekana kabisa tangu dakika ya 15 ilipopata bao, Equatorial Guinea walibadilisha mfumo wa uchezaji na kuamua kujilinda zaidi. Hata hivyo, inaonekana tatizo kwao lilikuwa ni kupata bao mapema. Huenda wangeweza kufanya hivyo kama wangechelewa kulipata. Dakika 75 za kujilinda, huku kukiwa na nne za nyongeza, ukichanganya na hali ya hewa ambayo hawajaizoea, kuliwafanya kuchoka zaidi kadri dakika zilivyozidi kusonga mbele na kupoteza umakini.

## NJE YA UWANJA

POINTI 17 na hasi moja (-1) ya tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa Arsenal iliyovuna katika mechi 12 za kwanza kwenye Ligi Kuu England, ndiyo rekodi mbaya zaidi kuwahi kutokea kwao mwanzoni mwa msimu baada ya idadi hiyo ya mechi tangu msimu wa 1982-83. Pia ilivuna pointi 17 katika msimu wa 2014-15, lakini tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa ilikuwa +5.





# SABABU 5 KWA NINI RONALDO BADO NI BORA KULIKO MESSI

**LONDON, England**

LINAPOKUJA suala la nani anastahili kupewa jina la mchezaji bora wa wakati wote, linakuwa jambo gumu kuamuliwa kirahisi, kwani kumtambulisha mchezaji mmoja tu inakuwa ni jambo lisilowezekana.

Lakini kwa sasa duniani inawataja wachezaji wawili ambao ndio wanaostahili kuwa washindi wa mchezaji bora wa wakati wote, ambao ni Lionel Messi na Cristiano Ronaldo, na kiukweli kabisa wote wawili wameonyesha kila kitu uwanjani.

Wachezaji wote wawili kwa sasa kila mmoja amejiwekea rekodi yake ya kipekee wakitwaa mataji na kuendelea kuwa kwenye kiwango cha juu kwa kipindi cha miaka 15.

Na kwa uhakika kabisa historia itawakumbuka zaidi, kwani kila mmoja amejiweka kwenye nafasi ambayo ni ngumu kwa wachezaji wengine kuzifikia rekodi zao.

Kutokana na ubora wao waliounyesha uwanjani, kwa sasa si jambo la kushangaza kwa vyombo vya habari, wachambuzi na mashabiki kuingia kwenye ubishani mkubwa kuhusu nani hasa ni bora kati yao.

Messi na Ronaldo wametawala mijadala mbalimbali kwenye vyombo vya habari na hata kwenye mitandano ya kijamii huku kila mmoja akimtaja mmoja wapo kuwa ndiye bora zaidi ya mwenzake.

Huku mjadala huo ukiwa unaendelea na kuonekana kuwa mgumu, Ronaldo anaonekana kuwa ni bora zaidi ya Messi katika kizazi hiki cha soka.

Makala haya yanakuchambulia na kukuelezea sababu za kwa nini Ronaldo ni bora kuliko Messi, twende sasa...

**1. Mafanikio kimataifa**

Akiwa ameshinda mataji 34 na Barcelona, Messi ni mchezaji mwenye mafanikio makubwa zaidi katika historia ya klabu hiyo ya pale Catalunya, akimzidi Cristiano Ronaldo aliyeshinda jumla ya mataji 29 katika klabu alizocheza kuanzia pale Manchester United, Real Madrid na Juventus.

Hata hivyo, kwenye ngazi ya kimataifa Ronaldo ana historia ya kuvutia zaidi, akiwa ameiongoza kama nahodha Ureno kutwaa taji lake la kwanza la Euro 2016 na akarudia tena miaka mitatu baadaye kwa kutwaa taji la Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Kwa upande wake Messi, bado hajaonja mafanikio kwenye ngazi ya kimataifa, ingawa amekuwa kwenye kikosi kinachotajwa kuwa na wachezaji wenye vipaji zaidi cha Argentina kwa miaka kadhaa na ameshindwa kwenye fainali nne za kimataifa, mbili zikija mfululizo kati ya mwaka 2014 na 2016.

2. Uwezo binafsi wa kuibeba timu

Wote Ronaldo na Messi ndio wanaoweza kubadilisha matokeo ya mchezo kwa kutumia vipaji vyao binafsi.

Timu zao wanazozichezea zimekuwa zinanufaika zaidi na huduma zao kwa kipindi cha miaka kadhaa sasa.

Lakini kiuhalisia Ronaldo katika hili amekuwa bora zaidi, kwani hata wakati wa utawala wa Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kulitwaa taji hilo mara tatu mfululizo, Mreno huyo ndiye alikuwa nguzo kubwa.

Akiwa na mabao 127, Ronaldo ndiye mfungaji wa wakati wote wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na mabao yake mengi yalikuja katika wakati muhimu zaidi kwenye michuano hiyo.

Messi anaongoza kwa kuwa na mabao mengi 67 kwenye hatua ya makundi ya michuano hiyo ikilinganishwa na Ronaldo mwenye mabao 62, lakini hapo ndio ulinganisho wao unapoishia, kwani Muargentina huyo mtu wa kuishia kwenye hatua ya mtoano katika miaka michache ya hivi karibuni.

Ronaldo nyota wa zamani wa Manchester United yeye amekuwa na rekodi ya mabao kwenye hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa na mabao 65 ikilinganishwa na Messi mwenye mabao 48.

Mabao yake mengi yalikuwa ya muhimu zaidi kwa kuisaidia Real Madrid kuvuka kwenye hatua hiyo, mfano 'hat-tricks' dhidi ya Wolfsburg, Atletico Madrid, Juventus na Bayern Munich ziliwafanya 'Los Blancos' kujiwekea rekodi yao ya kipekee.

Hata akiwa na Juventus, Ronaldo alionyesha umuhimu wake, wakati alipoisaidia kuvuka hatua ya mtoano ya timu 16 kwa mabao yake matatu dhidi ya Atletico Madrid na kuwawezesha 'Bianconeri' hao kupindua matokeo ya awali ya 2-0 ya mchezo wa kwanza.

Kwenye hatua ya kimataifa, Ronaldo amezidi kung'ara kwa kuibeba Ureno.

Yalikuwa mabao yake ambayo yaliisaidia Ureno kufuzu hatua ya makundi ya Euro 2016 ambapo mwisho wa siku walilitwaa taji hilo, huku pia akifunga mabao yote manne dhidi ya Sweden kwenye kapu la kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2014.

**3. Kung'ara ligi tofauti**

Cristiano Ronaldo alianza kucheza soka la kiushindani akiwa pale Sporting Lisbon na baada ya msimu wake wa kuvutia kwenye klabu hiyo ya nchini Ureno, ukafuatia uhamisho wa kwenda Manchester United.

Kwa kipindi cha miaka sita pale Old Trafford, Ronaldo alionyesha njia ya kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye historia ya kikosi cha Manchester United na alikuwa na mchango mkubwa zaidi kwa mafanikio yaliyopatikana kwenye kikosi hicho.

Aliweka rekodi ya kununuliwa kwa ada kubwa zaidi duniani wakati anahamia Real Madrid mwaka 2009 na wakati alipoondoka pale kwenye dimba la Bernabeu mwaka 2018, hakukuwa na shaka kwamba ameacha historia ya kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi katika kikosi cha Ligi Kuu ya Hispania.

Ukurasa mpya umeandikwa katika klabu ya Juventus na bado ana safari ndefu ya kwenda, huku akiwa na nia kubwa ya kuwasaidia Bianconerri hao kulitwaa taji la Ligi ya Mabingwa walilolisubiri kwa miaka mingi.

Lakini kwa upande wake, Messi ametumia karibia muda wake wote wa kucheza soka akiwa pale Barcelona na bila shaka ndiye mchezaji bora zaidi katika historia ya klabu hiyo, kwani ameweka kivuli chake kikubwa zaidi kwenye kikosi hicho.

Kihistoria kuna wachezaji ambao walikuwa na mafanikio makubwa zaidi duniani kwa kucheza klabu moja tu katika maisha yao yote, kama vile, Paolo Maldini akiwa na AC Milan, Gerd Muller akiwa na Bayern Munich, Francesco Totti akiwa na AS Roma na hata Pele akiwa na Santos. Hivyo, mafanikio ya Messi yapo kwenye klabu moja tu ya Barcelona.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba, Ronaldo amekuwa na uwezo wa kuhama klabu tofauti tofauti na kote ameweza kuonyesha uwezo wake mwenyewe na hilo linamfanya kuwa juu ya Messi.

**4. Mchezaji aliyekamilika zaidi kuliko Messi**

Ronaldo ni mchezaji anayetumia mguu wa kulia, lakini kwa miaka ya hivi karibuni pia ameweza kuutumia vizuri mguu wake wa kushoto, na pia mfungaji mzuri zaidi wa mabao ya kichwa kwenye historia ya klabu hiyo.

Katika mabao yake zaidi ya 700 aliyofunga kwenye ngazi ya klabu na timu ya taifa, 442 (sawa na asilimia 63.1) alifunga kwa mguu wa kulia, huku mabao 129 (sawa na asilimia 18.6) alifunga kwa mguu wa kushoto na mabao 127 (sawa na asilimia 18.2) alifunga kwa kichwa, huku mawili akifunga kwa sehemu nyingine ya mwili.

Hii ni tofauti na Messi ambaye kwa asilimia kubwa anategema zaidi mguu wake wa kushoto, ambao ameutumia kwa kufunga asilimia 83.5 ya mabao yake 501 kati ya 600 aliyofunga katika klabu ya Barcelona, huku mabao 85 (sawa na asilimia 14.1) akifunga kwa mguu wa kulia na mabao 55 (sawa na asilimia 9.1) akifunga kwa kichwa.

Hii ina maana kwamba Ronaldo ni mchezaji aliyekamilika na mwenye uwezo wa kutumia miguu yote miwili tofauti na Messi.

**5. Kujituma**

Kwenye suala la kipaji halisi na akili ya soka Ronaldo hawezi kusogelea uwezo wa Messi. Lakini Ronaldo amefanya kazi kubwa zaidi kujipambanua na kujituma zaidi kuonyesha kwamba yeye ni bora zaidi.

Kuna stori nyingi kutoka kwa wachezaji wenzake na makocha waliomfundisha Ronaldo ambaye ana nidhamu kubwa zaidi linapokuja suala la mazoezi na kujiweka fiti wakati wote.

Wanasema kwamba, mara zote Ronaldo anakuwa wa kwanza kufika kwenye mazoezi na wa mwisho kuondoka.

Wachezaji wenzake wengi walijaribu kumuiga, lakini wakashindwa, kwani yeye linapokuja suala la mazoezi na kujiweka fiti hana mzaha hata kidogo.

Wengi wanaona kwamba, Ronaldo hana kipaji, lakini kijituma kwake ndio siri kubwa ya kuwa na ubora alionao na hivyo kumfanya aweze kushinda mara tano tuzo ya Ballon d'Or.

Tofauti na Messi ambaye yeye ni mmoja wa wachezaji wachache ambao wamezawadiwa kipaji cha uchezaji soka.

Ronaldo amepambana kwa nguvu kubwa kujithibitisha ubora wake, tofauti na Messi.

## Nukuu

"Utafika wakati ambao umri wangu hautaniruhusu kuishi hadi kile ambacho Barcelona inahitaji kushindana, lakini kwa kadri niwezavyo, maadamu nina nguvu, kunipa ushindani ni bora zaidi. Itakuwa bora kwangu na bora kwa klabu, kuleta mshambuliaji kwa sababu kutaleta ushindani," **Mshambuliaji wa Baracelona Luis Suarez akizungumza na gazeti moja la Uruguay.**



"Lazima tumshukuru [Cristiano] Ronaldo, kwa sababu amejitolea kuwa pale usiku wote wa leo [wakati Juve ikishinda 1-0 dhidi ya AC Milan Jumapili ya wiki iliyopita] katika hali ngumu. Amefanya kila liwezekano kucheza, lakini niliona hakuwa sawa na nikafikiri ilikuwa vema kumtoa nje. Ni kawaida mchezaji kupatwa na hasira akiondoka uwanjani, haswa anapofanya bidii ili awepo pale," **kocha wa Juve, Maurizio Sarri akijitetea baada ya kufanyia 'sab' Ronaldo na kuonyesha kukasirika.**



"Nina hamasa kubwa ya kufanya kazi katika nafasi yangu hii mpya na ni changamoto mpya kwangu," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger baada ya Rais wa Fifa, Gianni Infantino kumteua kuwa Ofisa Mkuu wa Maendeleo ya Soka Duniani.**





Kocha wa zamani wa Yanga, Mwinyi Zahera, akitoa maelekezo kwa nahodha wa timu hiyo, Pappy Tshishimbi kabla ya kutimuliwa.

# KOCHA GANI ANAFUATA HAWA 7 KUTIMULIWA?

**Na Mwandishi Wetu**

KABLA hata nusu msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika, baadhi ya makocha wameshaondoka kwenye timu kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kutolipwa stahiki zao na wengine kutimuliwa kutokana na matokeo mabovu.

Wakati Ligi Kuu imefikia raundi ya 11 sasa, makocha saba wameshaachana na timu walizokuwa wakizifundisha na kusababisha wachambuzi wa masuala ya michezo kutabiri kuwa hadi msimu wa Ligi Kuu 2019/20 utakapomalizika, huenda makocha zaidi ya 15 watakuwa wameshaondoka au kutimuliwa kwenye timu wanazozifundisha.

Hawa ni makocha ambao walianza kwa kuzifundisha timu kwenye Ligi Kuu, lakini kwa sasa wametimuliwa au kuondoka kwa sababu tofauti.

**1. Athumani Bilal 'Bilo' (Alliance FC)**

Kocha Athumani Bilal 'Bilo' aliyekuwa akiifundisha Alliance ndiye aliyeweka rekodi ya kutimuliwa mapema zaidi, nadhani kwenye historia ya soka la Tanzania.

Alitimuliwa baada ya mechi moja tu, kwani baada ya mechi ya kwanza kati ya timu yake dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, alionyeshwa mlango wa kutokea. Cha ajabu katika mechi hiyo, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, lakini viongozi waliamua kumtimua.

Hata hivyo, mwenyewe amesema kuwa alitofautiana na viongozi wa timu hiyo kwa madai walikuwa wanataka kuingilia majukumu yake.

Alisema alitofautiana na meneja wake, baada ya kufanya mabadiliko ya kumtoa mchezaji Jerry Tegete na kumuingiza Herry Kalisa.

**2. Amri Said (Biashara United)**

Akufukuzaye hakwambii toka. Huu ni msemo wa kiswahili. kwenye mechi za mwanzo tu za Ligi Kuu, kocha huyo alikuwa na mzozo na uongozi wa timu yake ya Biashara United ya Mara.

Amri Said, pamoja na mambo mengine alikuwa akidai malimbikizo ya pesa zake na akaonekana kujiweka pembeni kuifundisha timu hiyo.

"Huwezi kufundisha timu ambayo ni matatizo kila siku, mimi mwenyewe nawadai mishahara, pesa za gesti niliyokuwa nimekaa hazijalipwa, wachezaji wanadai kiasi kwamba hawajitumi, sasa hii siyo sahihi, ndiyo maana niko Dar nimerejea, lakini nasubiria haki yangu," alisema.

Hata hivyo, viongozi wa timu hiyo nao wakaibuka na kudai kuwa Amri haonekani kwenye kituo chake cha kazi, huku habari za ndani zikisema kuwa kocha huyo ameenguliwa kwa sababu ya matokeo mabovu ya timu hiyo mwanzoni mwa msimu. Mwisho wa siku, viongozi wa Biashara wametamka rasmi kuwa wameachana na Amri.

**3. Felix Minziro (Singida United)**

Kwenye mechi ya tatu tu ya Ligi Kuu, Kocha Mkuu wa Singida United, Felix Minziro aliamua kuondoka mwenyewe kwenye timu hiyo kwa madai kuwa wameshindwa kumpa mkataba wa kudumu na timu hiyo, badala yake amekuwa akifanya kazi katika mazingira magumu.

Hali hii ilitokea baada ya Singida United kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC Agosti 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

Viongozi wa Singida United hawakujibu, badala yake wakamtangaza kocha mpya ambaye ndiyo yupo mpaka sasa, Ramadhani Swazurimo.

**4. Etienne Ndayiragije (Azam FC)**

Uongozi wa Azam FC uliamua kwa dhati, kuachana na kocha wao mkuu, Etienne Ndayiragije ili aendelee na majukumu mengine.

Kitu kilichosababisha hali hiyo itokee si kwamba Ndayiragije ameshindwa kazi, la hasha. Ni kwa sababu alikuwa na majukumu mengine kwenye timu ya Taifa, Taifa Stars kama kaimu kocha, akiwa na mkataba na Wanalambalamba, kitu ambacho kilisababisha afanye kazi sehemu mbili, Azam FC kwenye mkataba na Stars ambako alikuwa ni kocha wa muda.

Azam ikamtangaza Aristica Cioaba kuwa Kocha Mkuu na siku chache baadaye Ndayiragije akatangazwa kuwa Kocha Mkuu wa Taifa Stars.

**5. Malale Hamsini (Ndanda FC)**

Baada ya mechi dhidi ya Yanga na kufungwa bao 1-0, Malale Hamsini alitimuliwa kwenye kikosi cha Ndanda FC.

Mwenyewe anasema kuwa alifuatwa na kiongozi mmoja wa kisiasa na kumuuliza maswali ambayo yeye kama kocha ilibidi aulizwe na viongozi wa klabu tu.

Kitendo cha kumuuliza kiongozi huyo yeye ni nani, kilitosha kabisa kumkatia tiketi ya kuondoka.

**6. Mwinyi Zahera (Yanga)**

Alikuwa Kocha Mkuu wa Yanga na kipenzi cha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo. Kisa cha kutimuliwa kilianza kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho kati ya timu hiyo na Pyramids ya Misri kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza. Nadhani Yanga walikuwa na matarajio zaidi kuliko uhalisia. Baada ya kupigwa mabao 2-1, mashabiki walimtupia mawe na kushinikiza uongozi umtimue. Lilikuwa suala la muda tu, kwani baada ya mechi ya marudiano nchini Misri na kuchapwa mabao 3-0, alitupiwa virago.


**7. Jackson Mayanja (KMC)**

Ilionekana mapema tangu mwanzo kuwa Jackson Mayanja hakuwa na maisha kwenye klabu hiyo.

Baada ya kutolewa mapema kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, KMC si tu kwamba haikuonyesha kiwango kizuri kwenye Ligi Kuu, bali hata matokeo yake yalikuwa ni ya kusuasua.

Hatimaye viongozi wa klabu hiyo wakaamua kumtimua na kuongeza idadi ya makocha waliofundisha Ligi Kuu na sasa hawapo kwenye klabu zao kufikia saba.

**NAJUA WAJUA**



Liverpool imeshinda mechi 11 kati ya 12 za mwanzo wa msimu wa Ligi Kuu England, hivyo kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi kwa pointi nane zaidi, ni Manchester United pekee msimu wa 1993-94 iliyowahi kukaa kileleni kwa alama nyingi zaidi baada ya mechi 12 (pointi tisa zaidi) kwenye ligi hiyo.

## SOKA



Liverpool ilipoibanjua Man City 3-1 msimu huu.

# UTABIRI 4 BORA EPL 2019-20

**LONDON, England**

USHINDANI ni kitu cha asili kwenye mchezo wa soka, huku wachezaji wake wakipambana dimbani kuhakikisha wanazisaidia timu zao kupata matokeo bora.

Kila mwaka Ligi Kuu ya England inakuwa na ushindani wa hali ya juu wa klabu, huku zikiwania pointi na mwisho wa siku kubeba taji.

Na hiyo inaifanya Ligi Kuu ya England kuwa moja ya ligi yenye burudani zaidi duniani kwa sasa.

Kila mwaka, mbio za nne bora kwenye ligi hiyo zinakuwa ngumu zaidi na kuvutia kweli kweli.

Hata hivyo, wakati ligi hiyo imeshashuhudia mechi 11 zikiwa zimechezwa hadi sasa (kabla ya mechi za juzi na jana), tayari wachambuzi wa soka wameanza kutabiri nani ambaye ataibuka kuwa bingwa wake.

Makala haya yanakuchambulia timu nne ambazo zina nafasi kubwa ya kuutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu, tiririka nayo...

**1. Liverpool FC**

Liverpool ni mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa sasa na ndio timu pekee kwenye Ligi Kuu ya England ambayo haijapoteza mchezo wowote hadi sasa. wakiwa na pointi 31 katika mechi 11, 'Wekundu' hao wanacheza soka la kuvutia na hawaonyeshi ishara kwamba watapunguza kasi.

Vijana hao wa kocha Jurgen Klopp tangu kuanza kwa ligi hiyo wanaonyesha wazi kwamba msimu huu wamepania hasa kulitwaa taji hilo. Na ikumbukwe kuwa Liverpool haijawahi kutwaa taji la Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha zaidi ya miaka 30 iliyopita.

Kwa sasa wapo kileleni na ndio wanaopewa nafasi kubwa zaidi ya kulitwaa taji hilo.

**2. Manchester City**

Liverpool kwa sasa ndio vinara wa ligi hiyo, lakini utakuwa ni ujinga kusema kwamba, mbio hizo ni za farasi mmoja.

Timu ya kocha Pep Guardiola, Manchester City nayo imetawala kwenye mbio za ligi hiyo kwa misimu miwili iliyopita.

Msimu uliopita Man City walishinda mataji manne, kitu ambacho hakikuwahi kufanywa na klabu yoyote ya Uingereza.

Mwaka huu, City pia wanaonekana wameanza msimu vizuri, wakiwa wamepoteza mechi mbili tu. Hata hivyo, kukiwa bado kuna mechi 27 zimebaki kabla ya kumalizika kwa ligi hiyo ni wazi kwamba Man City watakuwa kwenye mbio bora zaidi za kuwania taji hilo.

Kuna vitu viwili vinatarajiwa mwaka huu Liverpool na Manchester City zitapigana hadi dakika ya mwisho kwenye mbio za ubingwa wa ligi hiyo na timu zote mbili zimeonyesha wazi kuwa zimejiandaa vya kutosha.

**3. Leicester City**

Wakati Leicester City waliposhinda taji la Ligi Kuu ya England mwaka 2016, waliishangaza dunia. Msimu huu chini ya kocha Brendan Rodgers, wanaonekana wanaleta ushindani mkubwa wa kumaliza kwenye nne bora.

Kwa sasa wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa wamepitwa pointi mbili tu na Manchester City.

Leicester kwa sasa ina kikosi bora chenye wachezaji wengi vijana, wakiongozwa na mkongwe wao, Jamie Vardy ambaye kufunga ni kawaida yake.

Tangu kuwasili kwa Rodgers Machi mwaka huu hapo kwenye dimba la King Power, Leicester imekuwa moja ya timu bora kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England hadi sasa.

Kipigo cha mabao 9-0 walichokitoa kwa Southampton ni moja ya mifano inayoonyesha wazi kwamba timu hiyo msimu huu imejipanga kweli kweli.

Ingawa katika miaka ya hivi karibuni nne bora imekuwa ikitawaliwa na timu sita za Arsenal, Chelsea, Liverpool, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur, Leicester kwa sasa wanaonekana watavunja utaratibu huo.

**4. Chelsea**

Adhabu ya kufungiwa kutofanya usajili wa wachezaji na ujio wa kocha mpya ambaye ni mchezaji wake wa zamani, Frank Lampard kuliwafanya mashabiki wa Chelsea kuwa na hofu kubwa.

Huku ikiwa imempoteza Eden Hazard aliyetimkia Real Madrid mashabiki wengi walikuwa na hofu ya Chelsea kufanya vibaya msimu huu.

Kufungwa na Manchester United kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu, kukamfanya Lampard kuonekana kwamba ana kibarua kigumu kwenye mbio za ligi hiyo.

Kwa sasa wakiwa nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Chelsea imeshinda mechi zake tano zilizopita katika mashindano hayo, huku ikicheza soka la kuvutia.

Wakiwa na usajili mpya wa Christian Pulisic ameonyesha jinsi gani alivyo muhimu kwa kikosi hicho akiwa na Tammy Abraham.

Huku Manchester United na Arsenal zikiwa bado hazipo kwenye ubora wao, mambo yanaonekana kwenda vizuri kwa Chelsea na wana nafasi kubwa ya kumaliza kwenye nne bora msimu huu.

Ingawa wanaonekana wapo kwenye ushindani mkubwa na Leicester na Tottenham Hotspur, lakini ni wazi wanaonyesha wapo kwenye nafasi nzuri.

Hata hivyo, Spurs imeonekana kutokuwa kwenye kiwango chake bora tangu kuanza kwa msimu mpya wa ligi hiyo mwaka huu na tayari wamepitwa pointi 10 na Chelsea.

**NDANI YA 18**



Mohamed Salah amehusika katika mabao 69 kwenye mechi 60 alizoicheza Liverpool za mashindano yote ndani ya dimba la Anfield (mabao 51, pasi za mwisho 18), kati ya hayo akifunga matatu kwenye mechi nne alizocheza uwanja huo wa nyumbani dhidi ya Manchester City.

Nipashe
Spotika



LINAPOKUJA suala la nani anastahili kupewa jina la mchezaji bora wa wakati wote, linakuwa jambo gumu kuamuliwa kirahisi, kwani kumtambulisha mchezaji mmoja tu inakuwa ni jambo lisilowezekana.

Uk. 16-17

# MAKOCHA WA5 WANAOLIPWA ZAIDI DUNIANI

**LONDON, England**

KAZI ya makocha kwenye mchezo wa soka, imebadilika zaidi kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Awali ilikuwa mara chache zaidi kwa makocha kutawala vikosi vyao, lakini kwa kuendelea kwa mapinduzi ya mchezo huu wa kuvutia zaidi duniani, sasa majukumu na kazi zao yameongezeka.

Katika soka la kisasa kocha anatarajiwa kuwa mtu mwenye vipaji vingi na kuwa ndiye kiungo haswa wa uendeshaji wa shughuli zote za soka kwenye klabu.

Huku wanasoka wakisifiwa kwa mafanikio yao dimbani, makocha wanatarajiwa kufanya kazi ya kimiujiza kwa timu zao. Mara zote wapo kwenye presha kubwa ya kusaka mafanikio.

Shukrani pekee ni kwamba, pamoja na kazi yao hiyo kuwa ngumu, lakini linapokuja suala la maslahi binafsi, yaani kiasi cha fedha wanacholipwa ni cha kuvutia kweli kweli.

Makala haya inakuchambulia makocha watano ambao kwa sasa wanalipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha duniani, teremka nayo...

**5. Mauricio Pochettino (Tottenham) - Pauni mil. 8.5**

Mauricio Pochettino alijiunga na Tottenham Hotspur akitokea kule Southampton kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2014 na amekuwa na mchango mkubwa kwa klabu hiyo kwa kuifikisha kwenye fainali ya Kombe la Ligi. Ingawa alimaliza akiwa nafasi ya pili dhidi ya Chelsea kwenye fainali, raia huyo wa Argentina aliiwezesha Tottenham kumaliza nafasi ya 5 kwenye msimamo wa Ligi Kuu msimu uliopita.

Tangu hapo, Spurs imekuwa iking'ara na Pochettino amekuwa katikati ya mafanikio hayo.

Pochettiono alikaribia kutwaa taji la Ligi Kuu ya England msimu wa 2015-16, kabla ya kuzidiwa kete na Leicester City waliolibeba kombe hilo. Licha ya ukweli kwamba, Pochettino bado hajashinda taji lolote akiwa na Spurs, amekuwa mmoja wa makocha walioitengeneza vizuri zaidi Tottenham.

Akiwa amefika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, kocha huyo mwenye umri wa miaka 47, amekuwa ndiye kama mhimili wa kiwango bora cha Spurs katika miaka ya hivi karibuni. Ingawa timu yake imekuwa ikisuasua msimu huu, Muargentina huyo anatarajiwa kubadilisha mambo haraka hivi karibuni.

Pochettino alisaini mkataba mpya Mei mwaka huu baada ya kumaliza kwenye nne bora kwa msimu kadhaa. Mkataba wake wa miaka mitano una thamani ya pauni milioni 42.5 na hiyo inamfanya atie mfukoni kiasi cha pauni milioni 8.5 kwa mwaka, na kumfanya kuwa kocha wa pili anayelipwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya England kwa sasa.

**4. Zinedine Zidane (Real Madrid) - Pauni mil. 10.5**

Wakati Zinedine Zidane alipoondoka Real Madrid mwishoni mwa msimu wa 2017-18, alikuwa anaingiza kiasi cha euro milioni 7.5 kwa mwaka. Kwa kipindi chake cha miaka miwili na nusu, Mfaransa huyo aliiwezesha klabu hiyo kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo. Pia alishinda taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, moja la Supercup, mawili ya UEFA Super na mawili ya Klabu Bingwa Dunia.

Baada ya kipindi kifupi, msimu wa 2018-19, Real Madrid walikuwa kwenye kina cha maji na Zidane akarudi hapo Machi mwaka 2019.

Zidane anaripotiwa kuingiza kiasi cha euro milioni 12 au pauni milioni 10.5 kwa mwaka kwa sasa, na kumfanya kuwa kocha wa tatu anayelipwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya Hispania na wanne duniani.

**3. Pep Guardiola (Man City) - Pauni mil. 15.2**

Hispania inachukuliwa kama moja ya nchi yenye makocha bora duniani kwa sasa. Pep Guardiola ametoka kwenye viunga vya Barcelona, kabla ya kupata mafanikio makubwa kule Ujerumani akiwa na Bayern Munich.

Lakini kazi kubwa ilikuwa inamsubiri kwenye Ligi Kuu ya England wakati alipochukua mikoba ya kuinoa Manchester City kipindi cha majira ya joto mwaka 2016.

Guardiola alianza taratibu, lakini baadaye akaifanya City kuwa miongoni mwa timu bora Ulaya, huku akiiwezesha kutwaa taji la Ligi Kuu mara mbili mfululizo na mataji matatu ya nyumbani.

Mhispania huyo anachukua nyumbani kiasi cha pauni milioni 15.2 kwa mwaka na alisaini mkataba mpya Mei ambao utamfanya kuwa na klabu hiyo hadi mwaka 2021.

Guardiola anashika nafasi ya kwanza kwa kuwa kocha anayelipwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya England na wa tatu duniani.

**2. Ernesto Valverde (Barcelona) - Pauni mil. 20.2**

Kocha huyu wa Barcelona kwa sasa anaweza kuwa kwenye presha kubwa pale Camp Nou baada ya kuanza kwa kusuasua msimu huu, lakini kila mmoja anajua kwamba Ernesto Valverde ana rekodi ya aina yake. Ameshinda taji la Ligi Kuu kwa misimu yake yote miwili tangu alipojiunga nayo mwaka 2017, huku pia akishinda taji la Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] na Super Cup.

Valverde kwa sasa anaingiza kiasi cha pauni milioni 20.2 kwa mwaka na kumfanya kuwa kocha wa pili anayelipwa zaidi kwenye Ligi ya Hispania na duniani.

**1. Diego Simeone - Pauni mil. 35.9**


Nahodha huyu wa zamani wa Argentina amekuwa na staili ya aina yake akiwa anaiongoza timu yake dimbani. Diego Simeone amekuwa akitoa changamoto kubwa kwa klabu za Real Madrid na Barcelona kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, tangu alipochukua mikoba ya kuinoa Atletico Madrid mwaka 2011.

Kwa sasa ndiye kocha anayelipwa mkwanja mrefu zaidi duniani kwa kuingiza kiasi cha pauni milioni 35.9 kwa mwaka na mkataba wake unamalizika mwaka 2022.



Simeone

**USILOLIJUA**



KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amepoteza mechi nane kwenye mashindano yote dhidi ya Jurgen Klopp, idadi ambayo ni mechi tatu zaidi ya alizopoteza dhidi ya makocha wengine.



# Waomba kuvuna miti Hifadhi ya Kitulo

**Na Nebart Msokwa,**
BUSOKELO

WAKAZI wa Bonde la Mwakaleli katika Halmashauri ya Busokelo, wameiomba serikali iwaruhusu kuvuna miti waliyoipanda ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo kabla hawajahamishwa kupisha upanuzi wa hifadhi hiyo miaka 16 iliyopita.

Wananchi hao wanadai kuwa pamoja na kwamba miti hiyo waliipanda wenyewe lakini kwa sasa wanazuiliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kwa madai kuwa wanaharibu mazingira pamoja na vyanzo vya maji vilivyomo ndani ya hifadhi hiyo.

Walitoa ombi hilo wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Jimbo la Busokelo, Atupele Mwakibete na kuhudhuriwa na uongozi wa hifadhi hiyo ambapo walisema miti hiyo inaweza ikawasaidia kuendeshea maisha yao.

Theresia Mahenge alisema wamekuwa wakifuatilia kwa muda mrefu ili wapewe vibali vya kuvuna miti yao, lakini hawajawahi kufanikiwa kutokana na maofisa wa Tanapa kuwazungusha. "Ile miti tuliipanda wenyewe lakini wakati tunahamishwa hatukulipwa fidia mpaka leo na haturuhusiwi kuivuna, tunaomba watu wa Tanapa waturuhusu tuivune kwa ajili ya shughuli zetu maana sasa hivi tunaogopa hatuwezi hata kwenda humo," alisema Theresia.

Naye Bonny Mwasantukwa, alisema mbali na kutoruhusiwa kuvuna miti yao, lakini pia hawana eneo la kuchungia mifugo, hivyo akauomba uongozi wa Tanapa kuwamegea eneo kwa ajili ya kuchungia ili kudumisha ujirani mwema.

Alisema awali walikuwa wanafuga kutokana na kuwa na eneo la kuchungia lakini baada ya kuondolewa kwenye maeneo yao ya asili na kupelekwa kwenye maeneo ambayo ni mafinyu wamepunguza idadi ya mifugo.

Mwasantukwa alisema awali walikuwa wanashindwa kuomba maeneo hayo kwa maelezo kuwa hakukuwa na uhusiano mzuri baina yao na watu wa Tanapa kitu ambacho alidai kuwa kwa sasa hali imekuwa ni shwari.

"Ninyi ni majirani zetu na tunasema hivyo kwa sababu hali imepoa na tunaishi vizuri kabisa, tunaomba mtusaidie na sisi eneo la kuchungia mifugo yetu, hata sisi hatuko tayari kuona mazingira yanaharibika na tutashirikiana kulinda," alisema Mwasantuka.

Akijibu maombi ya wananchi hao, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, Kamishna Msaidizi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, Theodora Alloysalisma, alisema upo uwezekano wa wananchi hao kuruhusiwa kuvuna miti hiyo endapo watafuata taratibu.

Aliwashauri waache kulalamika na badala yake wafuate taratibu ili wapewe vibali vya kuivuna ama wapewe fidia ma mamlaka hiyo endapo kuvunwa kwa miti hiyo kutaathiri mazingira ya hifadhi pamoja na vyanzo vya maji.

Alisema wao ni wasimamizi wa sheria na wala hawapo juu ya sheria hivyo sio rahisi wakaamua kutoa vibali kwa wananchi hao kuingia hifadhini na kuvuna miti kiholela hata kama waliipanda wao kabla ya kuhamishwa.

"Mazungumzo yapo, kwa hiyo mtu yeyote ambaye ana miti ambayo ni ya kigeni na hata kama ni ya asili aje tuzungumze, tunaweza tukaruhusu avune au akatafutiwa miti mingine, lakini hatuko tayari kuona vyanzo vya maji vinaharibiwa," alisema Kamishna Theodora.

Aliwataka wananchi hao kuzingatia sheria ili kuepuka mikwaruzano na serikali.



Wafanyabiashara wa mbao katika Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, wakipanga mbao mpya kwenye makundi tofauti kulingana na vipimo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bibi wa watoto waliozaliwa njiti afunguka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMA mzazi wa mwanamke aliyejifungua watoto watano katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Cecilia Mbaza, amewaomba Watanzania kuepuka kuamini imani potofu dhidi ya watoto wenye uzito pungufu (njiti), kuwa watoto hao hawawezi kukua.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi katika hospitali hiyo, Cecilia alisema wajukuu zake wawili kati ya wanne waliokuwa wamewekwa kwenye chumba cha joto kutokana na kuzaliwa na uzito pungufu, kwa sasa wana afya njema.

Alisema baadhi ya watu huwa wanaamini kuwa watoto njiti hawawezi kuishi na badala yake huwa wanafariki, kitu ambacho alidai sio kweli kwa maelezo kuwa watu wanatakiwa kufuata maelekezo wanayopewa na wataalamu wa afya.

"Sio kweli kwamba watoto njiti hawawezi kuishi, wapo wengi waliozaliwa hivyo na ni viongozi wakubwa, naamini wajukuu zangu watakua na dalili zinaonekana maana wananyonya vizuri kabisa na nawashauri watu waache kuamini vitu ambavyo hawajaambiwa na wataalamu wa afya," alisema Cecilia.

Alisema kwa sasa wajukuu zake wanaendelea kunyonya pamoja na kutumia maziwa mbadala baada ya kushauriwa na wataalamu wa afya wa Hospitali ya Mkoa.

Aliushukuru uongozi wa hospitali hiyo kwa huduma ambazo mwanaye alikuwa anapewa kuanzia mwezi Mei alipogundulika kuwa ana ujauzito wa watoto watano mpaka alipojifungua kwa upasuaji Oktoba 31 mwaka huu.

Alisema bado wanaendelea kuwahudumia bila ya gharama zozote baada ya uongozi wa hospitali kuwasamehe malipo.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kumsaidia kulea wajukuu zake hao kwa maelezo kuwa hana uwezo wa kutosha kuwahudumia watoto hao pamoja na mama yao.

Mama wa watoto hao, Emelia Joram (21), alisema kwa sasa anaendelea vizuri kiafya pamoja na watoto wake, huku akiwashukuru madaktari wa hospitali hiyo kwa kumsaidia kujifungua liche ya kwamba mtoto mmoja alifia tumboni.

Pia aliwashukuru Watanzania wanaoendelea kujitolea vitu mbalimbali kwa ajili ya kumsaidia kuwalea watoto wake kwa maelezo kuwa bila misaada hiyo hawezi kumudu kuwalea watoto hao vizuri.

# Wakulima wadogo wafundwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wadogo wameshauriwa kuzingatia matumizi ya teknolojia bora za kilimo na kuachana na kilimo cha mazoea ili wakue na kuwa wakulima wa kati na baadaye kuwa wakulima wakubwa.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kituo cha Uyole Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu teknolojia za kilimo ambazo taasisi hiyo imebuni.

Alisema wakulima wanatakiwa wazalishe kwa kufuata utaratibu wanaoelekezwa na wataalamu wakiwamo maofisa kilimo wa vijiji pamoja na wataalamu wanaouza pembejeo za kilimo.

Alisema taasisi hiyo haitaki watu kuendelea kujiita wakulima wadogo wakati teknolojia zipo nyingi na kwa sasa hivi wamekuja na teknolojia ya kupima udongo na kuwashauri wakulima mazao yanayofaa kulingana na aina ya virutubisho.

"Kwa sasa serikali inapambana kuingia kwenye uchumi wa viwanda ambao unahitaji malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda vinavyoanzishwa, sasa tukiendelea kuwa na wakulima wadogo wengi haitatusaidia," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisisitiza maofisa kilimo wa vijiji wanatakiwa kuanzisha utaratibu wa kufuatilia ukuaji wa wakulima kwenye maeneo yao ili kuepuka kuwa na wakulima ambao hawakui kila mwaka.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo mbalimbali kuzalisha mazao ya kimkakati kwa kutumia mbegu za kisasa zinazozalishwahwa na taasisi hiyo ili wainuke badala ya kuendelea kuwa vile vile huku baadhi wakitumia mbegu za kienyeji.

Dk. Bucheyeki alisema kwa sasa taasisi hiyo imezalisha mbegu mbalimbali za kisasa ambazo wakulima wanashauriwa kuzitumia ili kuongeza tija zikiwamo za maharage, mahindi, alizeti, maparachichi na ngano.

Mtafiti wa zao la viazi mviringo katika taasisi hiyo, Dk. Dolla Mende alisema katika utafiti walioufanya wamegundua mbegu mbalimbali ambazo zikitumiwa na wakulima zitawainua kutokana na kuzaa vizuri na kukinzana na magonjwa pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema wameshazalisha aina 10 za mbegu za viazi na kwamba aina zingine zipo kwenye hatua mbalimbali za utafiti ili kuangalia ubora wake na kama zitafaa zitasambazwa kwa wakulima ili waendelee kuzizalisha.



# Wataka maofisa ugani wapewe mafunzo

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa maofisa ugani wanashindwa kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima kuhusu matumizi ya ardhi na mbegu bora kutokana na ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wakulima Wadogo wilayani Chamwino (JUWACHA) ambalo lipo chini ya ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali la Action Aid, Janeth Nyamayahasi, wakati wa maonyesho maalumu ya mbegu na vyakula asilia wilayani humo.

Alisema maofisa hao wanashindwa kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima ikiwa ni pamoja na namna bora ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotokana na mabadiliko ya mifumo ya kilimo nchini.

"Wengi wanashindwa kutekeleza majukumu yao kwa kutoa elimu au kushauri wakulima na kusababisha kupata mavuno kidogo kutokana na kukosa ushauri wa kitaalamu," alisema. Aidha, mwenyekiti huyo alitaja miongoni mwa changamoto zinazowakabili wakulima ni pamoja na uhaba wa pembejeo, ukosefu wa masoko na maofisa ugani.

"Pembejeo zinachelewa kufika kwa wakati, masoko ya uhakika hakuna na changamoto kubwa ni mabadiliko ya tabia ya nchi hii ni ya kitaifa hususani ni mikoa ya Singida na Dodoma, kwa sababu kwa hali halisi ni mikoa yenye ukame," alisema. Aliongeza: "Lakini hatuna vipimia hali ya hewa, hatuna vipimo ambavyo vitaonyesha mwaka huu mvua ni chache kweli, kwa hiyo tulikuwa tunaomba watabiri wa hali ya hewa na vipimo vyake viwekwe sahihi."

Alipongeza shirika hilo kwa kuwa mstari wa mbele katika kuwawezesha wakulima wanawake wadogo wadogo vijijini kulima kwa kufuata kanuni za kitaalamu na kuwajengea uwezo wa kuweza kumiliki ardhi.

Kwa upande wake, Mratibu wa Shirika la Pelum Tanzania, Donati Senzia, alisema lengo la maonyesho hayo ni kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya chakula cha asili na kuwakutanisha wakulima na wataalamu wa kilimo.

Alisema katika maonyesho hayo wakulima wamekutanishwa na taasisi mbalimbali ikiwamo Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA) na Kituo cha Tafiti za Kilimo Tanzania.



Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, akizungumza kwenye sherehe za Maulid ya Msikiti wa Dodoma Sunni Jamaat Nunge jijini Dodoma, sherehe hizo zilifanyika usiku wa juzi. **PICHA: INRAHIM JOSEPH**

# Wasiolipa mikopo Saccos kikaangoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UONGOZI wa Kazi Saccos Limited, umeagizwa kuwaburuza mahakamani wanachama wasiorejesha mikopo ili wachukuliwe hatua stahiki za kisheria kutokana na kukiuka mikataba yao.

Saccos hiyo inaundwa na watumishi waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Akifungua jana mkutano mkuu wa Saccos hiyo, Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye ulemavu, Esther Mwakilima, alisema kuna wanachama ambao wamekuwa na mwenendo mbaya wa kukopa bila ya kutaka kurejesha kwa wakati na kwa makusudi.

"Naomba niseme wazi kuwa suala hili lipo mezani kwangu na nimeshatoa maelekezo ya awali kwa mwenyekiti wenu kuwa wale wote ambao hawataki kurejesha mikopo hiyo kama mlivyokubaliana kwenye mikataba yenu, wachukuliwe hatua stahiki za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani," aliagiza.

Mwakilima alisema uongozi wa Saccos hiyo unatakiwa kuwafikisha watumishi hao mahakamani baada ya mkutano huo.

"Ofisi yangu ilishatoa maelekezo kwa watumishi waliopo Ofisi ya Waziri Mkuu (KVAU) kuhakikisha wanakopa kwa busara na kulipa madeni yao kwa wakati, hatutasita kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa yeyote atakayepatikana na hatia na kuhukumiwa kwa tuhuma za namna hii," alisema.

Aidha, aliwataka kubadilika kuanzia sasa kila mmoja awajibike kwa chama kwa kukijali, kukithamini na kuheshimu kwa kuweka akiba, kukopa na kurejesha kwa wakati ili wapate manufaa zaidi ya wanayopata kwa sasa. Mwenyekiti wa Saccos hiyo, Omari Sama, alisema fedha zilizopo kwenye mzunguko wa wanachama ni takribani Sh. milioni 200.

"Changamoto kubwa tuliyonayo ni madeni mabaya kwa wanachama ambao wengine wapo kwenye wizara mbalimbali na chama chetu kina watumishi wa kada zote, kuna wakurugenzi wapo kwenye wizara zingine tunawadai na hawajalipa kwa kipindi kirefu," alisema.

Alisema madeni hayo yapo kwenye hoja za wakaguzi na wamekuwa wakikaguliwa na Shirika la COASCO kila mwaka.

Hata hivyo, alisema pamoja na kuwa na changamoto ya mikopo isiyolipika pia hawana ofisi hali inayoongeza gharama za uendeshaji.

# 'Madereva serikali chanzo cha ajali'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WABUNGE wamesema baadhi ya madereva wa magari ya serikali wamekuwa wakisababisha ajali za barabarani kutokana uzembe na mwendo kasi.

Wakizungumza katika mkutano wa kuwakumbuka waathirika wa ajali za barabarani, wabunge hao walisema madereva wa serikali ndio wanaoongoza kwa kuvunja sheria za barabarani.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alisema ajali nyingi zinasababishwa na uzembe wa madereva, mwendo kasi, kusinzia na ubovu wa barabara.

Alishauri kufanyiwa marekebisho sheria ya usalama barabarani ili kuwekewa makali na kupunguza ajali zitokanazo na sababu hizo.

"Nikiwa Mkuu wa Wilaya nilipata ajali na nilivunjika mguu wangu mara nne sababu ya uzembe wa dereva wa gari lililokuwa likija mbele yetu alitugonga na lilikuwa ni gari la serikali kutokana na uzembe," alisema.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Rose Tweve, alitaka kuwapo na usawa katika utoaji wa adhabu za uvunjifu wa sheria za barabarani bila kuangalia vyeo.

Alisema wengi wa wanaosababisha ajali ni madereva wa serikali ambao mara nyingi huendesha kwa mwendokasi kuyapita magari mengine bila tahadhari yoyote.

Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Allan Kiula, alitaka askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, waache tabia ya kujificha na kuvizia magari kwenye maeneo hatarishi bali wajikite katika kutoa elimu ili kujiepusha na ajali. "Kitu hichi si cha kiungwana na ni kinyume cha maadili ya kazi, mnapaswa kusimamia usalama wa eneo husika."

"Mfano mzuri makutano ya barabara ya Area C jijini Dodoma pale hutokea ajali nyingi, lakini unakuta askari wapo badala ya kuongoza magari wao hukaa pembeni," alisema Mbunge Kiula.

Awali, Ofisa Programu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Mackphason Buberwa, alisema ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) inaonyesha vifo vitokanavyo na ajali za barabarani vinashika nafasi ya nane duniani kutokana na idadi kubwa ya watu kufariki.

Alisema kwa mujibu wa ripoti hiyo, watu zaidi ya milioni moja wanafariki kwa ajali, na kwamba inaonyesha hadi kufikia mwaka 2030 ajali za barabarani zinaweza kushika namba moja kwa kuua watu.

"TLS tangu mwaka 2003 imekuwa ikishauri namna ya kuweka mikakati ya kuzuia ajali ili zisiendelee kuacha makovu kwa ndugu zetu wanaopata ajali," alisema Buberwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili Dodoma, Mary Munisi, alisema suala la kutofunga mikanda huchangia ajali.

"Sheria inasema mtu wa mbele na dereva wafunge mikanda na si abiria wote kitu ambacho kinaleta mkanganyiko hivyo ni vyema zikaangaliwa upya," alisema.

Inspekta wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Josephat Mjema, alisema sheria ipo kimya kuhusu mwendokasi maeneo maalumu kama sokoni, shuleni na hospitali.

"Tunapendekeza mwendokasi wa 30kph badala ya 50kph, pia miundombinu isiyofaa na ufinyu wa barabara umekuwa ni tatizo," alisema.

Alisema wataendelea kufanya kazi kwa weledi kwa kusimamia sheria zilizopo, huku akitoa rai kwa viongozi wa serikali kuacha kuwaona kama ni sehemu ya vikwazo kutokana na madereva wao kutotii sheria za barabarani.





# CCM Zanzibar yajinadi kwa wazee

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Zanzibar ambaye ni Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali anayoiongoza itaendelea kuwatunza na kuwaenzi wazee ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii ili waishi maisha bora na yenye furaha.

Akizungumza na wazee wa Wilaya ya Amani na Wilaya ya Mjini Kichama, alisema serikali imeandaa sera ya wazee na hivi sasa inaandaa sheria ya kuwatunza wazee.

Alieleza kuwa hivi sasa wazee wote waliofikia umri wa miaka 65 na kuendelea wanapewa pensheni jamii ya Sh. 20,000 kila mwezi na kuahidi kuwa, uwezo ukiruhusu pensheni hiyo ataiongeza kabla ya kuondoka madarakani.

Alieleza haja kwa wazee kuwaeleza vijana juu ya heshima ya wazee na vipi wazee wanatakiwa kuenziwa na kutunzwa sambamba na kupewa heshima yao kutokana na mambo makubwa waliyoyafanya.

Alisema serikali inathamini na inazijali juhudi za wazee walizozichukua hadi kupelekea kupatikana Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar kupitia vyama vya ASP na TANU.

Alisema wazee ndio walioijenga Zanzibar na kuleta ukombozi na kuwakomboa wanyonge.

Aidha, alieleza kuvutiwa na taarifa ya wazee hao waliyoisoma, huku akieleza kuwa ahadi zote zilizoahidiwa na chama hicho zitatekelezwa hatua kwa hatua.

Alisisitiza haja ya kutumia busara ndani ya chama hicho sambamba na kuwatumia wazee katika kufanikisha masuala mbalimbali ndani ya chama hicho kwa maendeleo ya chama na nchi kwa jumla. Dk. Shein alisema huu ni wakati wa viongozi, wanachama na wazee wa CCM kufanya mambo yao kwa pamoja.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdalla Juma Mabodi, alisema CCM itaendelea kuwatunza na kuwaenzi wazee kama ilivyoeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020.

Alisema CCM imewatambua wazee kwa kuweka mabaraza ya wazee katika ngazi zote, likiwamo Baraza la Asili la Wazee wa Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui ambalo limeundwa siku ya pili baada ya kuundwa ASP.

Wazee katika taarifa yao, walimpongeza Dk. Shein kwa kuwapatia wananchi huduma za kijamii ikiwamo majisafi na salama, afya na elimu bure.



Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (Zec), Makama Juma Pandu, akitoa maoni yake juzi, jijini Dar es Salaam, katika mkutano wa wadau wa uchaguzi kuhusu nafasi ya mwanamke katika uongozi, uliondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).**PICHA: SABATO KASIKA**

# Kusini Unguja waahidiwa majisafi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema serikali itaendelea kuwatumikia wananchi wa mjini na vijijini katika kuwapatia huduma muhimu za kijamii ikiwamo majisafi na salama.

Alisema hayo Uroa Wilaya ya Kati Unguja, baada ya kushiriki kazi ya ufungaji na ulazaji wa mabomba ya majisafi, katika kambi ya Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) iliyopo Bambi.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma zote muhimu kwa wakati ili kuwaondolea usumbufu.

Alieleza kwamba serikali inatambua changamoto kubwa inayowakabili wananchi wa kijiji hicho ni majisafi na salama kutokana na maji yaliyopo kijijini hapo kuchanganyika na chumvi.

Hata hivyo, aliwaomba wananchi kuthamini jitihada za serikali kwa kuhakikisha wanautunza mradi huo ili udumu kwa muda mrefu.

Aliwashukuru wadau waliofanikisha kukamilika kwa mradi huo, na kuwaomba kuendelea kuiunga mkono serikali katika miradi mingine.

Naye Ofisa wa Maji Wilaya ya Kati, Ali Abdi, alisema mradi huo upo katika hatua ya mwisho na unatarajiwa kukamilika kabla ya Januari 2020, ambapo hadi sasa umeshagharimu zaidi ya Sh. milioni 280.

Wananchi wa kijiji hicho walielezea kufurahishwa kwa hatua ya serikali ya kuendelea kuwakamilishia mradi huo na kuiomba Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuona umuhimu wa kutoa kipaumbele cha kuwaunganishia mapema huduma hiyo.

# UPDP Zanzibar yamkana Dovutwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha United Peoples Democratic Party (UPDP), kimepinga tamko la Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho Fahmi Nassor Dovutwa, alilolitoa hivi karibuni kuhusiana na kutoshiriki kwa chama hicho katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji.

Kimeeleza kuwa hatua iliyotolewa na Mwenyekiti huyo inakwenda kinyume cha katiba chama hicho, hivyo aliwataka wagombea wote wa chama hicho kuendelea na taratibu za uchaguzi katika maeneo yao kama iliyopangwa ili kukipatia ushindi chama chao.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari katika Ofisi za Makao Makuu ya chama hicho, Mjini Zanzibar, Katibu Mkuu wa UPDP, Hamad Mohammed Ibrahim, alidai chama kinapinga na kutengua tamko hilo kwani amekwenda kinyume cha katiba ya chama chao kifungu cha 15.7.

Alisema kifungu hicho kinatoa mwongozo kwa kamati kuu kusimamia mambo mbalimbali ikiwamo kutoa uongozi wa siasa mwelekeo na msimamo wa chama katika nchi kazi ambayo inafanywa na kamati kuu na si ya mwenyekiti.

Alidai kwa mujibu wa kifungu hicho mwenyekiti huyo alitakiwa kuitisha kamati kuu kujadili hali ya kisiasa ikiwa ni pamoja na kushiriki au kutokushiriki katika uchaguzi huo.

"Mimi kama katibu mkuu sina kumbukumbu ya kikao chochote hadi sasa, maamuzi haya amejichukulia mwenyewe kwa tamko lake mwenyewe bila kujali kuwa anakwenda kinyume cha katiba yetu sasa hili ni tamko la chama" alisema.

Alieleza kushangazwa na mwenyekiti huyo kushiriki vikao mbalimbali vya vyama vingine na kutoa maazimio bila ya idhini ya kamati kuu ya chama ya chama chake.

Alodai makao makuu ya chama itahakikisha inamshughulikia Mwenyekiti huyo kwa mujibu wa katiba yao.

Makamo Mwenyekiti wa chama hicho, Abdalla Mohammed Khamis, alisema chama baada ya tamko hilo liliandika barua kwa msajili wa vyama vya siasa yenye kumbukumbu namba UPDP/HQ/ZNZ/VOL/12/2019 ya Novemba 12, mwaka huu kuwa kauli aliyoitoa mwenyekiti huyo ni maamuzi yake pekee na sio ya chama.

# SMZ yatakiwa kuchukua hatua udhalilishaji kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA ya Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, kimelaani kasi ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, hivyo kuitaka serikali kuchukua hatua madhubuti dhidi ya vitendo hivyo vinavyotokea na kuripotiwa katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kaimu Mkurugenzi wa Tamwa-Zanzibar, Asha Abdi Makame, vitendo vya udhalilishaji wa kingono wanavyofanyiwa kinamama, watoto na wajane vinapaswa kukomeshwa ili kuwezesha wananchi kuishi kwa amani na utulivu katika visiwa hivyo.

"Kuanzia Januari hadi Oktoba 2019, Tamwa Zanzibar imerekodi kesi 116 za udhalilishaji zinazohusiana na kubaka, kulawiti, kubaka kwa kundi, kupiga, kuchoma moto, kutorosha na shambulio la aibu na kutelekeza," alisema Makame na kuongeza: "Tunaziomba mamlaka husika zichukue hatua stahiki ili kukomesha vitendo hivi."

Alisema ushahidi wa baadhi ya matukio ya udhalilishaji wa kingono kwa watoto, wanawake na wajane umekuwa ukivurugwa na kubadilishwa jambo linalosababisha watuhumiwa kuachiliwa huru na hivyo kuongeza ukubwa wa tatizo.

"Kingine kinachovunja moyo ni pale kesi inapofikishwa mahakamani ikiwa ushahidi umeshavurugwa, kilichoandikwa kwenye hati ya mashtaka ni kidogo kuliko tatizo lililoripotiwa awali, mathalani wazazi wamepeleka kesi ya mtoto kubakwa, jalada lililopelekwa mahakamani linasoma ametoroshwa," alisema.

Kaimu Mkurugenzi huyo ameitaka jamii kutokufumbia macho vitendo hivyo kwa kuhakikisha inatoa taarifa kwa mamlaka husika pale yanapojitokeza matukio ya udhalilishaji wa kijinsia na kutoa ushirikiano kikamilifu ili kukomesha vitendo hivyo.

Alitaja maeneo yaliyokithili vitendo hivyo visiwani humo kuwa ni Bopwe, Wete na Mkoa wa Kaskazini Pemba na kuviomba vyombo vya dola kuongeza nguvu katika maeneo hayo ili kudhibiti hali hiyo na kurejesha amani na utulivu kwa wananchi.




Ofisa Masoko wa Zantel, Haji Mussa (kulia), akimkabidhi simu janja ya gharama nafuu aina ya SMARTA, Fainat Jaffar, mkazi wa Mbweni Zanzibar, mmoja wa washindi 4 wa SMARTA katika hafla iliyofanyika katika ofisi za kampuni hiyo mjini Zanzibar, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka malezi ya kidini shuleni

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

TAASISI binafsi na za serikali zinazotoa elimu kwa watoto kuanzia ya msingi, sekondari na vyuo, zimetakiwa kutoa malezi ya kidini kwa wanafunzi, ili kuwezesha nchi kupata watumishi wenye maadili mema, ambao watatumikia taifa kwa uadilifu na uaminifu.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri waViwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, wakati wa mahafali ya wanafunzi zaidi ya 300 wa darasa la saba na kidato cha nne katika shule za msingi na sekondari za Kaizirege na Kemebos, ambayo yamekwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 13 tangu kuanzishwa kwa taasisi ya Kaizirege, iliyoko katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera. Waziri Bashungwa alisema malezi bora yenye misingi ya kidini yanaendana na elimu bora, maana bila maadili hakuna elimu bora.

"Tuko katika dunia ya utandawazi, kwa hiyo tusipotoa elimu ya dini kwa watoto wetu, tunaweza baadaye tukapata watendaji na viongozi wasio na maadili ambao wanaweza kuliingiza taifa matatani," alisema.

Aidha, aliwataka wazazi kuwekeza katika kuwapatia watoto wao elimu bora, maana ndio urithi pekee na wenye manufaa kwa familia na taifa kwa ujumla, huku akiwataka watoto waliohitimu kuthamini gharama wanazozitumia wazazi wao kuwasomesha, kwa kwenda kuwa watu wema huko waendako.

Alisema serikali inaendelea kuboresha sekta ya elimu, lakini bila ushiriki wa dhati wa sekta binafsi mafanikio yanayolengwa yanaweza yasifikiwe, lwa kuwa sekta binafsi inategemewa kusaidiana na serikali kutoa elimu bora.

"Kama serikali tunatambua mchango mkubwa wa sekta binafsi katika kuwezesha utoaji wa elimu bora kwa Watanzania, na ndiyo maana tunaendelea kuweka mazingira mazuri yanayoruhusu watu kuwekeza katika sekta hiyo," alisema Bashungwa.

Meneja wa shule hizo, Eurogius Katiti, aliiomba serikali kuboresha miundombinu ikiwamo barabara inayopita katika shule hiyo, ikiwa ni hatua mojawapo ya kuweka mazingira yanayovutia uwekezaji, lakini pia barabara hiyo ikitengenezwa itakuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa kata Ijuganyondo, hasa wanawake wajawazito na wagonjwa wengine, pindi wanapohitaji kusafiri kufuata huduma.

# NEMC yaridhishwa utunzwaji mazingira mradi umeme Rufiji

**Na Mwandishi Wetu,** RUFIJI

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) limelidhishwa na hatua za ujenzi wa mradi wa umeme Mto Rufiji unavyoendelea sambamba na uzingatiaji wa tathmini ya athari kwa mazingira hali inayopeleka mazingira kutoathirika na shughuli za ujenzi.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hayo alipofanya ziara katika eneo la mradi huo mwishoni mwa wiki nakujionea hatua mbalimbali za ujenzi ambazo mkandarasi kampuni ya JV Arab Contractors na Elsewedy Electric wanatekeleza ujenzi pamoja na kusimamia mazingira.

Alisema NEMC imefungua kanda maalum katika eneo la mradi ili kufanya ufuatiliaji wa karibuni wa utunzaji wa mazingira katika eneo zima kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika eneo la mradi.

"Tumeweka kambi katika eneo hili lengo elimu ya mazingira iendelee kutolewa kwa na kufanya ufataliaji wa karibu wa hatua zinazochukuliwa na mkandarasi katika swala zima la utunza mazingira katika eneno la mradi," alisema.

Aliongezea kuwa mradi huu utakwenda kuondoa tatizo la umeme nchini na hata kuuza nchi nyingine za karibu hivyo kupelekea taifa kupata mapato na uifanya nchi kukua kiuchumi, hivyo nguvu ya pamoja katika kufanya mradi huu ukamilike unahitaji.

"Kila mdau kwa nafasi yake awajibike ili kufanya mradi huu wa ujenzi wa umeme ukamilike kwa wakati pasipo kuleta athari zozote za kimazingira katika eneo hili la mradi ambalo lipo ndani ya mbuga ya Nyerere," alisema.

Alieleza kuwa shughuli za binadamu katika eneo la mradi zinahitaji uratibu NEMC ili kuhakikisha mazingira ya eneo hilo yanabaki salama na viumbe wanaotegemea eneo hilo wanaendelea na maisha pasipo athari zozote.

"Kukamilika kwa mradi huu kutaleta chachu ya kukuza utalii nchini kutokana na uwepo wa mradi huo na pia miundombinu itakayojengwa itavutia uwekezaji katika sekta ya utalii, hali itakayochochea zaidi ukuaji wa uchumi nchini," alisema.

# Mpinzani atangazwa kushinda urais Sri Lanka

**SRI JAYAWARDENAPURA, Sri Lanka**

TUME ya Uchaguzi nchini Sri Lanka, imemtangaza mgombea wa upinzani na waziri wa zamani wa ulinzi, Gotabaya Rajapaksa, kuwa mshindi wa uchaguzi kwa kupata zaidi ya asilimia 50.

Gotabaya, Luteni Kanali mstaafu mwenye umri wa miaka 70, alipata asilimia 52.2 ya kura kwa mujibu wa matokeo rasmi yaliyotangazwa na tume ya uchaguzi.

Mpinzani wake mkuu miongoni mwa wagombea 35 amepata asilimia 41.99, Sajith Premadasa waziri wa serikali inayomaliza muda wake na mwenye msimamo wa wastani alitangaza mapema kukubaliana na matokeo hayo na kumpongeza Gotabaya.

Idadi ya waliojitokeza kupiga kura ni asilimia 83.7 ya watu waliosajiliwa kwa ajili ya uchaguzi huu, kwa mujibu wa tume ya uchaguzi.

Wakati Premadasa alikuwa na uungwaji mkono mkubwa kwenye maeneo yanayokaliwa na Watamil, mwenzake Gotabaya alikuwa akiungwa mkono na maeneo yanayokaliwa na jamii ya Sinhalese, ambao ndio wengi nchini Sri Lanka.

Gotabaya anatazamiwa kuapishwa leo. Gotabaya, aliyepewa jina la utani la "Terminator" na familia yake mwenyewe kutokana na kusimamia operesheni ya kikatili kabisa dhidi ya kundi la waasi.

Sajith Premadasa, waziri mwenye msimamo wa wastani, ameshindwa kwenye uchaguzi wa rais wa Sri Lanka.

Kaka huyo wa aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Mahinda Rajapaksa, alitumia kampeni yake kuzungumzia juu ya masuala ya usalama, akiapa kuyaangamiza makundi ya itikadi kali ndani ya taifa hilo lenye waumini wengi zaidi wa dini ya Buddha, kufuatia mashambulizi hayo ya tarehe 21 Aprili, ambayo yanaaminika kufanywa na kundi la ndani la siasa kali za kidini.

Ushindi huu, hata hivyo, unatajwa kupokelewa kwa shaka na jamii za wachache nchini Sri Lanka, wakiwamo Waislamu na Watamil, na pia waandishi wa habari, wanaharakati wa haki za binaadamu na jumuiya ya kimataifa wanaokumbuka jinsi miaka kumi ya utawala wa kaka yake,

Mahinda, kuanzia 2005 hadi 2015 kilivyokuwa kipindi kigumu kwa makundi hayo.

Ndugu hao wawili, Mahinda na Gotabaya, waliendesha operesheni yenye mafanikio makubwa iliyokomesha miaka 37 ya vita vya wenyewe kwa wenyewe na Watamil waliokuwa wakipigania kujitenga na kuunda taifa lao.

Muongo huo mmoja unakumbukwa na wengi kama kipindi cha uvunjwaji wa haki za binadamu, mauaji ya kiholela na pia cha kukaribiana sana na China.

**DW**



Mgombea wa Upinzani na Waziri wa zamani wa Ulinzi Sri Lanka, Gotabaya Rajapaksa, ametangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi kwa kupata zaidi ya asilimia 50. **PICHA: DW**

# Kupanda bei mafuta kwaibua hasira

**TEHRAN, Iran**

WAANDAMANAJI waliokasirishwa na kupanda kwa bei ya mafuta Iran kwa asilimia 50 wamefunga barabara katika miji mikubwa nchini humo na walipambana mara kwa mara na polisi Jumamosi.

Katika ghasia hizo inaaarifiwa kuwa mtu mmoja ameuawa. Maandamano hayo yameweka shinikizo jipya dhidi ya serikali wakati ikihangaika kuondokana na vikwazo vya Marekani vinavyoikabili nchi hiyo baada ya Rais Donald Trump wa Marekani kuitoa nchi hiyo kutoka katika makubaliano ya kinyuklia kati ya Iran na mataifa yenye nguvu duniani.

Katika maandamano hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yalikuwa ya amani ghafla yaligeuka kuwa ya ghasia katika maeneo kadhaa ambapo video zilizowekwa katika mtandao zilionyesha polisi wakifyatua mabomu ya gesi ya kutoa machozi na makundi ya watu yakiwasha moto.

Wakati yakiwakilisha kitisho cha kisiasa kwa Rais Hassan Rouhani kabla ya uchaguzi wa bunge mwezi Februari, pia yanaonyesha ghadhabu iliyosambaa kwa watu wengi miongoni mwa Wairan milioni 80 ambao wameshuhudia hifadhi yao ya fedha ikiyeyuka kutokana na ukosefu wa ajira na kuporomoka kwa sarafu ya taifa hilo ya Rial.

Maandamano yalifanyika katika miji zaidi ya 12 katika muda mfupi kufuatia uamuzi wa Rouhani mapema siku ya Ijumaa kupunguza ruzuku katika mafuta ili kugharamia fedha zitolewazo kwa watu masikini nchini humo.

Mafuta nchini humo bado yanabaki kuwa rahisi duniani, ambapo bei mpya imepanda hadi rial 15,000 kwa lita moja, ikiwa ni ongezeko la asilimia 50 kutoka siku moja kabla. Hii ni senti 13 kwa lita, ama kiasi ya senti 50 kwa galoni moja. Galoni ya mafuta ya kawaida nchini Marekani ni kiasi ya dola 2.60, ukilinganisha.

Lakini katika taifa ambako wengi wanaendesha maisha yao kama madereva wa teksi ambao sio rasmi, mafuta rahisi yanaonekana kuwa haki ya kuzaliwa. Iran ni nchi ya nne duniani yenye hazina kubwa ya mafuta ghafi.

Wakati ilitarajiwa kupanda kwa bei ya mafuta kwa miezi kadhaa, uamuzi huo bado umewashtua watu wengi na kuzusha maandamano ya ghafla nchini humo.

Ghasia zilizuka Ijumaa usiku katika mji wa Sirjan, ulioko kilometa 800 kusini mashariki mwa tehran. Shirika la habari la nchi hiyo IRNA limesema, waandamanaji walijaribu kuchoma moto kituo cha kuhifadhi mafuta, lakini walizuiwa na polisi.

Polisi hawakutoa taarifa zaidi, lakini video zilizowekwa mtandaoni nchini Iran zinaonyesha moto katika kituo hicho cha kuhifadhi mafuta wakati magari ya polisi yakisikika.

Video nyingine inaonyesha kundi kubwa la watu likipiga kelele: Rouhani, aibu kwako! Ondoka nchini peke yako!"

Mohammad Mahmoudabadi, ofisa wa Wizara ya Mambo ya Ndani katika mji wa Sirjan, baadaye aliimbia televisheni ya taifa kuwa polisi na waandamanaji walishambuliana kwa risasi, na watu kadhaa kujeruhiwa.

Amesema maandamano yalikuwa ya amani, lakini baadaye watu waliojifunika nyuso zao wakiwa na bunduki na visu walijiingiza katika maandamano hayo.

**DW**

# Uingereza kuchapisha ripoti kuhusu Urusi

**LONDON, Uingereza**

SERIKALI ya Uingereza itachapisha ripoti ya bunge inayochunguza madai ya Urusi kuingilia siasa za Uingereza baada ya uchaguzi mkuu wa Desemba 12.

Waziri wa Usalama wa Uingereza, Brandon Lewis, amekiambia kituo cha televisheni cha Sky News kwamba ripoti hiyo huenda isichapishwe katika kipindi hiki tete cha kuelekea uchaguzi.

Wapinzani wanaituhumu serikali kupitia kamati ya bunge ya ujasusi na usalama kwa kuikalia ripoti hiyo, ambayo imeshapitishwa na idara za usalama kwa kuwa inaweza kufichua mambo ya aibu dhidi ya Waziri Mkuu, Boris Johnson pamoja na chama chake.

Lakini Lewis amesema wanataka kuhakikisha wanachukua tahadhari hususan katika masuala yanayohusiana na usalama wa taifa na kusisitiza kuwa ripoti hiyo itachapishwa baada ya uchaguzi.

**DW**

# Mazoezi Marekani, Korea yasitishwa

**NEWYORK, Marekani**

WAZIRI wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper, amesema kwamba wamesitisha kwa muda usiojulikana mazoezi ya pamoja za kijeshi na Korea Kusini katika kile alichokitaja nia njema kuelekea Korea Kaskazini.

Hatua hiyo inakuja hata baada ya Waziri wa Ulinzi wa Japan, Taro Kono, ambaye nchi yake imekuwa ikitishwa na majaribio ya mara kwa mara ya makombora yanayofanywa na Korea Kaskazini kumuelezea Esper kwamba hakuna ambaye ana matumaini kuhusu kubadilisha hatua za Korea Kaskazini.

Matamshi hayo ya Kono yanaashiria kuzorota kwa mahusiano kati ya Marekani na washirika wake wa kimataifa, katika wakati wanapojaribu kuirejesha Korea Kaskazini kwenye mazungumzo ya kuachana na mipango yake nyuklia na makombora. Ingawa katika tawala zilizopita Marekani iliziita luteka hizo kuwa ni muhimu, lakini Rais Donald Trump ameziita kuwa ni upotevu wa fedha na uchokozi dhidi ya Korea Kaskazini.

**DW**

# Waziri ashauri ada ipunguzwe shule binafsi

**Na Mwandishi Wetu, KIBAHA**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, ametoa wito kwa shule binafsi nchini, kupunguza ada ili kuwapa unafuu wazazi wanaotaka kusomesha watoto katika shule hizo.

Nditiye alitoa wito huo juzi katika mahafali ya kwanza ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari ya Jostihego iliyoko Kibaha mkoani Pwani.

Alisema serikali inatambua mchango wa shule binafsi katika kuinua elimu nchini na kuwataka wamiliki wake kutambua kuwa elimu ni huduma na si biashara.

"Shule binafsi ni wabia wa serikali, hivyo wamiliki wake wanapaswa kufuata maelekezo ya serikali. Baadhi ya wamiliki wamegeuza elimu kuwa biashara badala ya huduma.

"Ni ukweli usiopingika baadhi ya shule ada zake hazishikiki, jambo ambalo linawafanya wananchi wa kawaida kushindwa kumudu gharama za kusomesha," alisema.

Nditiye alisema serikali imeendelea kutatua vikwazo mbalimbali vilivyopo kwenye elimu, huku akiwataka wanafunzi kusoma kwa bidii.

"Zingatia mambo haya matatu: Soma kwa bidii; soma sana; soma kwelikweli. Hii ndio siri ya kufaulu, hakuna mchungaji atakayekuombea ufaulu, ni jitihada zako mwenyewe," alisema.

Awali, Nditiye alitembelea na kukagua mazingira ya shule hiyo na kuzindua bweni la wavulana na kupanda mti.

Mkuu wa Shule hiyo, Joakim Kinyunyu, akizungumza katika mahafali hayo, alisema shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2016 na imekuwa ikifanya vizuri kitaaluma mwaka hadi mwaka.

"Katika mtihani wa kidato cha pili mwaka juzi, watoto wetu wote walifaulu kwa alama za daraja la kwanza na la pili pekee.

"Ni matarajio yetu matokeo ya mtihani wa kidato cha nne ya mwaka huu yatakuwa mazuri zaidi kwa wahitimu wetu hawa tunaowaaga leo (juzi)," alisema.

Jumla ya wahitimu 17 waliagwa shuleni hapo. Kati yao, wasichana ni 10. Shule hiyo kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 95.



Kiongozi wa Waislamu Shia Ithnasheriya Maulana, Sheikh Hemed Jalala, akiongea katika sherehe za Maulid, katika Viwanja vya Pipo Kigogo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ataka udhibiti magonjwa yasiyoambukiza

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

IDARA ya Afya mkoani Tabora imesema kuna umuhimu wa jitihada za kuzuia na kudhibiti ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza mkoani humo.

Baadhi ya magonjwa yasiyoambukizwa ni kisukari, shinikizo la damu, seli mundu, saratani, magonjwa ya akili na pumu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuzuia na kudhibiti magonjwa hayo, Katibu Tawala Msaidizi (Afya), Dk. Honoratha Rutatinisibwa, alisema tangu mwaka 2017 hadi 2019, kumekuwapo na ongezeko la magonjwa hayo mkoani humo.

Alitaja baadhi ya wagonjwa wa magonjwa yasioambukizwa waliongeza kuwa ni kisukari, mwaka 2017 walikuwa wagonjwa 4,345 na kuongezeka hadi 6,732, mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la wagonjwa 2,387 sawa na asilimia 35.

Dk. Rutatinisibwa alisema kwa upande ugonjwa wa shikizo la damu, wagonjwa wameongezeka katika kipindi hicho kutoka 13,940 hadi kufikia 19,460 ikiwa ni ongezeko la wagonjwa 5,520 sawa na asilimia 28.

Pia upande wa ugonjwa wa pumu umeongezeka kutoka wagonjwa 5,338 hadi 8,434 ikiwa ni ongezeko la wagonjwa 3,096 sawa na asilimia 37 ndani ya kipindi hicho.

Akizungumza wakati wa kilele cha Wiki ya Maadhimisho ya Kupambana na Magonjwa hayo, Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Komanya Kitwala, aliwataka wakazi wa Mkoa wa Tabora kujenga tabia ya kuchunguza afya zao mapema mara mbili kwa mwaka.

Alisema hatua hiyo itasaidia kugundua matatizo mapema na kuwahi kukabiliana nalo likiwa bado katika hatua za awali kwa kutumia gharama kidogo.

Kitwala aliongeza kuwa suluhisho jingine ambalo halihitaji gharama kubwa kukabiliana na tatizo hilo ni pamoja na wakazi wa Tabora kubadili mfumo wa maisha kuhusu ulaji wa vyakula na kushiriki mazoezi.

# Kampeni usajili laini yawafikia Pemba

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na wadau wengine imewapa elimu wananchi wa Pemba kuhusu kampeni ya mnara kwa mnara na kuwahamasisha wasajili laini zao kwa kutumia alama za vidole na kuhakikisha wanapata kitambulisho cha taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman, akizungumza katika kampeni hizo jana, zilizofanyika viwanja vya Gombani mjini humo alisema usogezaji wa huduma hiyo utarahisisha mawasiliano na wananchi kusajili laini zao na kupata kitambulisho hicho kwa wale ambao hawana.

Kampeni hizo zinafanywa kwa ushirikiano wa TCRA na wadau wengine ambao ni Jeshi la Polisi Kitengo cha Uhalifu Mtandao na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) na Idara ya Uhamiaji.

Hemed aliwataka wananchi kujitokeza kusajili laini zao ambazo zitasajiliwa kwa kutumia kitambulisho cha Taifa.

Naye Mkuu wa TCRA, Zanzibar, Esuphatie Masinga, alisema hiyo ni fursa kwa wananchi wa Pemba kujitokeza kujisajili kwa alama ya vidole pamoja na kupata usajili wa kitambulisho cha taifa.

"Kampeni hii ilianzishwa ili kutoa fursa kwa wananchi waweze kusajiliwa laini zao kwa alama za vidole pamoja na huduma nyingine za mawasiliano," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi ambao hawana kitambulisho cha Taifa watumie fursa hiyo kuvipata.

Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabed Masasi, aliwahamasisha wananchi hao kutumia kampeni hiyo ili kupata vitambulisho.

**"Kampeni hii ilianzishwa ili kutoa fursa kwa wananchi waweze kusajiliwa laini zao kwa alama za vidole pamoja na huduma nyingine za mawasiliano," alisema.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MASHINE INAUZWA** DE-OILING MACHINE. Mashine ya kukausha mafuta kutoka katika vyakula vilivyokaangwa na mafuta kwa mfano Crisps, karanga, korosho nk. Kwa mawasiliano: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**MASHINE INAUZWA,** SEASONING MACHINE. Mashine ya kuchanganya chumvi au pilipili nk. Kwenye vyakula kama karanga, korosho, crisps nk. Kwa mawasiliano piga simu namba: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**MASHINE INAUZWA,** PACKING MACHINE. Mashine ya kupaki karanga, korosho, crisps nk. Kwa mawasiliano piga simu namba: 0764 127 853 / 0762 222 407 / 0628 883 003.

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila*

### KUPOTEA KWA KADI

**Lawrence Marima Madole** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina BENZ ML yenye namba ya Usajili T 545 BAM iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**KW/RB/7340/2019**

### KUPOTEA KWA KADI

**Henrika Stephen Simbila** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina TOYOTA IST yenye namba ya Usajili T987 DCH iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/SEL/RB/459665/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI



Mwenye picha hapo juu **WINNEFRIDA L.MANYANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index No. S1067/0036 Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2004 PASUA SECONDARY.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye .

Polisi taarifa:
**ARU/ARU/RB/443794/2019**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Peter Mathew Swai** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mistubish fuso yenye namba za usajili **T 354 AHU**

Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa ya polisi
**KAH/TR /RB/ 835 /2019.**

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0767 223311*

### TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnataarifiwa kuwa kampuni ya CHINA HENAN INTERNATIONAL COOPERATION GROUP CO. LTD (CHICO) itasafirisha gari lake tupu la mzigo yenye upana mkubwa (Low bed Truck) lenye namba za usajili T 507 BKM/T 509 BKM kutoka DODOMA kwenda TABORA kupitia ITIGI.
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu: 12.0m
   Upana: 03.0m
   Kimo: 3.2m
3. Njia itakayotumiwa ni barabara ya DODOMA-TABORA kupitia ITIGI
4. Gari za usindikizaji:
   T 643 CVZ itakuwa mbele
   T 304 CVZ itakuwa nyuma

Tunaomba radhi kwa usumbufu

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# MASHABIKI

## UNITED WAMKATAA SANCHO

**MANCHESTER, England**

MASHABIKI wa Klabu ya Manchester United wamemwambia kocha wao, Ole Gunnar Solskjaer aachane na mpango wa kumsajili Jadon Sancho kwa sababu Daniel James ni bora zaidi.

Sancho mwenye umri wa miaka 19, amekuwa kwenye kiwango bora tangu alipoondoka Manchester City na kwenda Borussia Dortmund mahali ambako amepewa nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza tangu mwaka 2017.

Lakini sasa staa huyo anayethaminishwa na pauni milioni 100 anataka kuondoka kwenye kikosi cha Bundesliga, huku Man United wakitajwa kwamba wanasaka huduma yake kwa nguvu zote.

Kocha Solskjaer anataka kuboresha safu yake ya ushambuliaji baada ya dirisha lililopita kuweka mkazo zaidi kwenye ukuta, alipowasajili Harry Maguire na Aaron Wan-Bissaka.

Lakini, sasa kinda Mason Greenwood ameanza kuonyesha ubora mkubwa sambamba na Anthony Martial, Marcus Rashford na James, jambo linalowafanya mashabiki wahoji kama Sancho anahitajika.

Mmoja aliandika kwenye Twitter: "Sancho hana ubora kumzidi Electric James". Mwingine aliandika: "Simtaki Sancho, mimi niko sawa tu na James...Hakuna kitu cha kipekee kuhusu Sancho...tafadhali tutumie pesa zetu kumsajili Maddison au Kai Havertz."

Shabiki mwingine aliandika: "Sancho anakuzwa tu. Mchukueni Jovic anaweza kucheza pia kama kiungo mbunifu. Atatusaidia kwenye 4-4-2. Pesa iliyobaki tunasajili beki wa kushoto na Halaand."

Rekodi za wawili hao kwenye ligi msimu huu, James amecheza mechi 12, ameanza 11, amecheza dakika 984, amefunga mabao matatu, pasi za mwisho mbili na kupiga mashuti 18, manane yakilenga goli, huku akitengeneza nafasi 11, krosi 43 na kugusa mpira mara 499, wakati Sancho amecheza mechi tisa, ameanzishwa nane, amecheza dakika 666, akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho tano, akipiga mashuti 14 na manane yamelenga goli akitengeneza nafasi 14 na kupiga krosi 13 huku akigusa mpira mara 592.

## HAZARD, MDOGO WAKE WAIBANJUA URUSI KWAO

**St Petersburg, Urusi**

EDEN Hazard alifunga mara mbili na kumtengenezea bao mdogo wake, Thorgan kwa Ubelgiji wakati ikipata ushindi wa 4-1 dhidi ya Urusi katika michuano ya kufuzu Euro 2020.

Kikosi hicho cha kocha, Roberto Martinez kilikuwa na kazi rahisi dhidi ya Urusi huku kikitoka kushinda mechi saba mfululizo.

Kocha wa Urusi beki yake ikisambaratishwa na kina Hazard, Dries Mertens na Kevin De Bruyne, ambao walitawala dimba la kati.

Romelu Lukaku alifunga bao la nne kwenye ushindi huo na kuifanya Ubelgiji kupata pointi sita zaidi kileleni mwa Kundi I, ikiwa imeshinda mechi tisa.



## KAMARA AIPONDA SIERRA LEONE

**FREETOWN, Sierra Leone**

MSHAMBULIAJI wa Sierra Leone, Kei Kamara, ambaye ametangaza kustaafu soka la kimataifa, licha ya kuitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa, amesema amechoshwa na mwenendo mbovu wa Shirikisho la Soka la nchini hiyo.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35, alitangaza maamuzi ya kustaafu soka la kimataifa kabla ya mchezo dhidi ya Lesotho, uliochezwa mjini Free Town.

Alisema maamuzi yake ya kustaafu soka la kimataifa yamekuja kutokana na kuchoshwa na mwenendo mbovu wa uendeshaji wa timu ya Taifa ya Siera Leone, ambayo inanolewa na kocha kutoka Ghana Sellas Tetteh.

Kamara anayeitumikia klabu ya Colorado Rapids inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MLS), alisema maamuzi yake ya kustaafu soka la kimataifa yamekuja wakati muafaka.



"Ninathibitisha kustaafu soka la kimataifa, nimechoshwa na mwenendo wa uendeshaji wa timu ya taifa," Kamara aliiambia BBC Sport.

"Nimeitumikia timu yangu ya taifa tangu mwaka 2008, kumekua hakuna maendeleo yoyote, hakuna mipango ya kuiongoza timu ili ifanikishe malengo ya kushiriki fainali kubwa barani Afrika na duniani.

"Sehemu yoyote duniani soka la vijana limekua likitumika kama mpango wa kufanikisha malengo ya timu ya taifa ya wakubwa, lakini nchini kwangu hakuna jambo kama hilo, na ndio maana kila siku tumekua tunaendelea kufanya vibaya na hatufiki mbali."

Kikosi cha Siera Leone kitaendelea na mchakato wa kusaka nafasi ya kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika wiki hii kwa kucheza mchezo wa pili wa Kundi L dhidi ya Benin mjini Porto-Novo.



# VAN DIJK: UHOLANZI ITAKIMBIZA EURO 2020

**AMSTERDAM, Uholanzi**

NAHODHA Virgil van Dijk amesema Uholanzi itafurahia wakati mzuri baada ya kufuzu kucheza michuano ya Euro 2020.

Waholanzi hao walimaliza muda wao wa kutoshiriki michuano mikubwa, baada ya kushindwa kufuzu Euro 2016 na Kombe la Dunia, wakati walipotoka sare ya bila kufungana na Ireland Kaskazini na kuwa vinara wa Kundi C.

Uholanzi ilikuwa bila ya Memphis Depay aliye majeruhi, wakati Ireland ilikosa penalti kipindi cha kwanza iliyopigwa na Steven Davis ambayo ingewapa presha vijana hao wa kocha, Ronald Koeman.

Lakini Uholanzi ilifuzu kucheza michuano hiyo mwakani ambayo inashirikisha timu 24.

Van Dijk, ambaye alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Liverpool msimu uliopita, aliiambia televisheni ya Uholanzi, NOS: "Tunakwenda tena kwenye mashindano. Hicho ndio kitu muhimu zaidi.

"Tulitaka kushinda leo (juzi) na tulikuwa na nafasi. Tulijua ingekuwa ngumu mwisho na tulifuzu.

"Katika dakika 15 za mwisho, Ireland Kaskazini walianza kucheza soka la kushambulia, lakini tuliwadhibiti vizuri."

## Mkataba Messi, Fati wamwibua Abidal

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi yupo kwenye mazungumzo na Barcelona juu ya kusaini mkataba mpya, Mkurugenzi wa soka wa klabu hiyo, Eric Abidal amethibitisha.

Mchezaji huyo raia wa Argentina ametumia miaka 18 akiwa Barca, lakini majaliwa yake yamekuwa shakani baada ya mwaka huu kusema kwamba anaweza kuondoka hapo Camp Nou akiwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or mkataba wake wa sasa na mabingwa hao wa LaLiga unamalizika mwaka 2021, lakini Abidal ana matumiani kuwa atakubali kusaini mwingine mpya.

"Tayari tupo kwenye mazungumzo," alisema akiliambia Gazeti la Mundo Deportivo. "Sijui kama tutakuwa na habari hivi karibuni kwa sababu maamuzi yatategemea na mchezaji mwenyewe."

Alipoulizwa kama anatarajia makubaliano hayo yatatangazwa hivi karibuni, Abidal alisema: "Itajulikana wakati utakapokuwa sawa, lakini nina imani mambo yatakuwa sawa."

Abidal pia alithibitisha kwamba, zao la akademi yao, Ansu Fati yupo kwenye mpango wa kuongeza mkataba wake, hasa kutokana na kuonyesha kiwango cha kuvuti.

"Tunazungumza naye," alisema Abidal. "Ni mchezaji kijana ambaye tunataka kumlinda. Tutazungumza na familia yake pamoja na wawakilishi wake."



## Lukaku aja na mapya kwa Solskjaer United



**MANCHESTER, England**

ROMELU Lukaku amedai kwamba, Ole Gunnar Solskjaer alitaka kumbakisha pale Manchester United, ingawa kocha huyo wa 'Mashetani Wekundu' alidai kwamba alikuwa na furaha kumuona nyota huyo wa Ublegiji akijiunga na Inter Milan Agosti.

Solskjaer aliiambia Sky Sports kwamba, uamuzi wa kumuachia Lukaku kuondoka "aliufanya yeye na alikuwa na furaha," lakini Lukaku alisema kuwa kulikuwa na muda ambao kocha huyo wa United hakuridhia yeye kuondoka.

Inter waliilipa United pauni milioni 74 kumchukua mchezaji huyo Agosti mwaka jana, akimaliza miezi ya uvumi juu ya majaliwa yake ya baadaye.

Lakini katika mahojiano na Het Belang van Limburg, Lukaku amesema kuondoka kwake kuliamuliwa mapema Machi.

"Solskjaer ana heshima yake," alisema Lukaku.

"Alielewa wakati nilipomwambia Machi kwamba ni wakati wangu wa kutaka kuondoka.

"Nimekuwa kwenye Ligi Kuu ya England tangu nikiwa na miaka 18 na sasa nina miaka 26. Solskjaer alitaka kunibakisha, lakini nilikuwa tayari kwa kitu kingine."

Lukaku amefunga mabao tisa katika mechi 12 za Ligi Kuu ya Italia, lakini alikumbwa na kupigiwa kelele za ubaguzi Septemba mwaka huu.

Alisema alijua alichokitarajia wakati akiwasili Italia, na akasisitiza anafurahia maisha yake hapo kwenye mji wa Milan.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ALONSO AMTAJA GUARDIOLA SABABU KUITOSA MADRID

Nilivutiwa kutaka kujua siri za ukocha wake, ana hamasa ya asili, mara zote alikuwa tayari kwa...

**MADRID, Hispania**

XABI Alonso amebainisha kwamba, aliondoka Real Madrid kwenda Bayern Munich kwa sababu alikuwa "amevutiwa" kutaka kujua siri ya ukocha wa Pep Guardiola.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, alijiunga na miamba hiyo mwaka 2014 baada ya kukaa na klabu hiyo kwa misimu mitano pale Santiago Bernabeu, ambako alishinda mataji sita.

Alonso aliondoka Madrid miezi mitatu baada ya kuwasaidia kutwaa ubigwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na akakaa kwa miaka mitatu pale Bayern kabla ya kuamua kustaafu.

Akielezea sababu ya kuondoka kwa miamba hao wa soka la Hispania, Alonso aliiambia The Athletic: "Nilikuwa nimevutiwa kutaka kujua siri za ukocha wa Guardiola.

"Ana hamasa ya asili. Soka ina msimu mrefu, lakini hadi mwisho wa msimu Pep kamwe haonyeshi kuchoka.

"Mara zote alikuwa tayari. Kwa wachezaji, pengine kunakuwa na hamasa lakini miguu haionyeshi kuchoka kabisa."

Alonso, ambaye kwa sasa amechukua nafasi ya kuwa kocha wa klabu ya Real Sociedad B kuanzia Juni, pia alisifia kazi inayofanywa na kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp.

Mchezaji huyo wa zamani wa Hispania, ambaye alicheza dhidi ya Borussia Dortmund iliyokuwa inafundishwa na kocha Klopp wakati akiwa pale Madrid na Bayern, alisema: "Sikufurahia kucheza dhidi yao kwa sababu walikuwa imara, na ilikuwa ngumu kuwapita.

"Ilionekana kama alikuwa na timu ambayo imeimarika kila sehemu. Yeye alikuwa anataka ushindi tu. Ilikuwa ni timu ambayo imejipanga na kucheza kwa umoja. Muda wote nilikuwa kwenye presha.

"Nilifurahia muda wote wa mchezo kwa sababu ilikuwa ni muhimu, lakini changamoto ilikuwa kubwa kuweza kuifunga Dortmund."

## KWA UFUPI

**PSG KIZUIZI UTD KWA SANCHO**
PARIS St-Germain inawezekana kuwa kizuizi kikubwa kwa Manchester United kuweza kumnasa winga wa Borussia Dortmund anayetajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 120, Jadon Sancho, 19. ***(Express)***

**LALLANA AMULIKWA PSG**
PSG inavutiwa na kiungo wa Liverpool, Muingereza Adam Lallana, 31. ***(Mirror)***

**COMAN KUMRITHI SANE CITY**
MANCHESTER City inapanga kumfuata winga wa Bayern Munich, Mfaransa Kingsley Coman, 23, endapo Leroy Sane atajiunga na mabingwa hao wa Ujerumani kama ilivyotajiwa majira ya joto. ***(Sky Sports)***

**ARSENAL KUTUA JUVE KWA DEMIRAL**
ARSENAL inaandaa ofa kwa beki Uturuki, Merih Demiral, 21, ambaye anaweza kuuzwa na Juventus kama ofa sahihi itatolewa. ***(Tuttosport)***

**MESSI, BARCA WATETA RASMI**
BARCELONA inajadili mkataba mpya na mshambuliaji Muargentina Lionel Messi, 32. ***(Mundo Deportivo)***

**EVERTON YAMTAKA PACIENCIA**
EVERTON itamuwinda mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Mreno Goncalo Paciencia, 25, katika dirisha la Januari baada ya kocha Marco Silva ameiomba klabu hiyo kumsajilia straika huyo. ***(Goal)***

**UNITED YAMFUATILIA PEREIRA**
Manchester United inamfuatilia winga wa West Brom, Mbrazil Matheus Pereira, 23, kwa mkopo kutoka kwa Sporting Lisbon. ***(Mirror)***

**ROMA KWA SMALLING JUMLA**
ROMA itapaswa kuilipa Manchester United pauni milioni 18, kama inataka kumpata jumla beki Muingereza Chris Smalling, 29, anayeichezea kwa mkopo. ***(Tuttosport, via Metro)***

**PARROTT KUZIDI KUULA SPURS**
TOTTENHAM itampa ofa ya ongezeko la mshahara mshambuliaji wa Jamhuri ya Ireland, Troy Parrott, 17, katika kumuongezea mkataba wake wa miaka mitatu. ***(Football Insider)***

**FERNANDES KUICHOMOLEA REAL**
KIUNGO wa Ureno, Bruno Fernandes, 25, ambaye amekuwa akihusishwa sana na Manchester United pamoja na Real Madrid, amesema "anajisikia upendo" na Sporting Lisbon. ***(Goal)***

**LUKAKU AFUNGUKIA SOLSKJAER**
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji Romelu Lukaku, 26, amedai Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer alimtaka kuendelea kubaki Old Trafford kabla ya kujiunga na Inter Milan kwa pauni milioni 73. ***(Mail)***

**BECKHAM AMPANIA MODRIC**
DAVID Beckham ameonyesha nia ya kumfanya kiungo wa Real Madrid, Mcroatia Luka Modric, 34, kuwa nyota wake mkubwa kusajiliwa katika klabu yake mpya ya Inter Miami. ***(AS)***



HABARI MICHEZO

# MAXIME ATAKA TATU ZA JUU LIGI KUU BARA

**Na Somoe Ng'itu**

TUTAPAMBANA! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, ambaye amesema kikosi chake kimejipanga kupambana ili kumaliza katika nafasi tatu za juu msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kagera Sugar imecheza mechi 10, ina pointi 20 na katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iko kwenye nafasi ya pili nyuma ya vinara na mabingwa watetezi, Simba ambayo ina pointi 22 na ikiwa imeshuka dimbani mara tisa.

Hata hivyo, Maxime ametahadharisha kuwa kuendelea kukaa kwenye nafasi za juu katika msimamo wa ligi hiyo, kunahitaji kuongeza bidii kutokana na timu zote zinazoshiriki ligi hiyo kutamani kufika kwenye nafasi hizo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Maxime, alisema anawakumbusha wachezaji wake kutodharau mechi hata moja kwa sababu klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zina hadhi sawa.

Maxime alisema anataka kuona anamaliza msimu katika nafasi ya juu msimu huu, lakini akiweka wazi kwamba bado mbio za kuwania ubingwa ziko wazi na klabu yoyote inaweza kuutwaa endapo itafanya vizuri katika mechi zake zote zilizobakia.

"Kwa sasa tunafikiria kumaliza katika nafasi tatu za juu kwenye msimamo, lakini tutakapoingia kwenye mzunguko wa pili, picha ya ubingwa itaanza kuonekana, klabu zinaongeza nguvu kwa sababu kila mmoja atahitaji kujiweka mahali salama," alisema Maxime.

Beki huyo wa zamani wa Kagera Sugar alisema ushindani utaongezeka zaidi kwa sababu timu zilizoko chini zitakuwa zinapambana kujinasua kutoka kwenye mstari wa kushuka daraja na msimu huu, timu zitakazoteremka zikiwa zimeongezeka.

Baada ya mapumziko ya siku nne, kikosi cha Kagera Sugar kinaendelea na mazoezi yake kwa ajili ya kuikaribisha Lipuli FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Novemba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba uliopo Bukoba mkoani Kagera.




Katibu Tawala wa Wilaya ya Kigamboni, Rahel Mhando (wa pili kulia) akikabidhi zawadi ya kompyuta bapa (Tablet) na jezi ya Copa Coca-Cola kwa Happy Stephano, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kambangwa wilayani Kinondoni katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa juma kwenye ofisi za wilaya hiyo, jijini Dar es salaam. Mwanafunzi huyo alikusanya jumla ya chupa 22,743 wakati wa Kampeni ya Rejesha na Ushinde iliyokuwa inaendeshwa na Kampuni ya Coca-Cola wakati wa mashindano ya Copa-Umisseta na kuibuka mshindi wa pili kwa mkoa wa Dar es Salaam. Kulia ni Mkurugenzi wa Mauzo na Masoko wa Kampuni ya Coca-Cola Kwanza, Josephine Msalilwa na wa pili kushoto ni Ofisa wa Chapa ya Coca-Cola Tanzania, Pamela Lugenge. **MPIGAPICHA WETU**

# Washindi Copa Coca-Cola wazawadiwa

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya Coca-Cola nchini Tanzania, kupitia mmoja wa washirika wake Coca-Cola Kwanza, imekabidhi zawadi kwa shule na wanafunzi katika jijini Dar es Salaam baada ya shule hizo kukusanya chupa nyingi za plastiki kupitia Kampeni yake ya Copa Coca-Cola ya Rejesha na Ushinde.

Sambamba na kauli mbiu ya mwaka huu, mashindano ya Copa Coca-Cola yalikuwa zaidi ya mpira wa miguu kwa shule zote zilizoshiriki barani Afrika kwa kujikita zaidi katika kubadili tabia kwa wanafunzi baada ya kuja na kampeni ya ukusanyaji wa chupa za plastiki kama sehemu ya kuwaelimisha juu ya umuhimu wa usafi wa mazingira.

Kwa Tanzania, takriban kilo 880,835 za plastiki zilikusanywa ambazo ni mkusanyiko mkubwa zaidi wa kampeni hii katika nchi zote za Afrika Mashariki na Kati, ambapo Shule ya Sekondari ya Kihesa ya mkoani Iringa ilikusanya idadi kubwa zaidi, kilo 52,710 za chupa za plastiki na kushinda zawadi kubwa ambayo ni urekebishaji wa kiwanja cha mpira na zawadi nyingine mbalimbali.

Kwa Dar es Salaam, shule tatu zimefanya vizuri ikiwa ni pamoja na Shule ya Sekondari ya Kisarawe II ya iliyopo wilayani Kigamboni, Shule ya Sekondari ya Kambangwa ya Wilaya ya Kinondoni na Shule ya Sekondari ya Mikwambe (Temeke).

Wanafunzi kutoka katika shule hizo tajwa walikusanya kiasi cha chupa za plastiki kama ifuatavyo, kilo 7,052, 6,279 na 3,110 wakati wa kampeni na jana walizawadiwa jezi 32 za Copa Coca-Cola na mipira miwili kwa kila shule. Sambamba na hilo wanafunzi watatu kutoka kila shule zilizoshinda walipewa zawadi za kompyuta bapa (Tablet) na saa za kisasa (smart watch) kwa kukusanya chupa nyingi zaidi katika shule zao huku walimu watatu kutoka kila shule wakiondoka na zawadi za kompyuta mpakato (Laptop), begi na fulana za Coca-Cola.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Josephine Msalilwa, Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo wa Kampuni ya Coca-Cola Kwanza, aliwasihi na kuwahamasisha wanafunzi na Watanzania kwa ujumla kuendelea kushiriki kampeni za ukusanyaji wa chupa za plastiki na kampeni nyingine za namna hiyo ili kupunguza taka na kujenga mazingira safi na yenye afya.

"Ukusanyaji wa chupa haulindi tu mali asili, lakini husaidia kuleta maisha bora kwa kila mtu. Kama kampuni tuliona ni sawa na kuhamasisha wanafunzi wanaoshiriki katika Copa Coca-Cola kushiriki katika ukusanyaji wa chupa za plastiki kutoka kwenye umri mdogo ili kuleta mabadiliko ya tabia ndani yao kwa sasa na katika maisha kwa ujumla," alisema.

Kampuni ya Coca-Cola mapema mwaka huu ilitangaza lengo la kusaidia kukusanya na kuchakata sawa na asilimia 100 ya ufungaji wake ifikapo 2030. Ili kufanikisha hilo, Kampuni ya Coca-Cola inafanya kazi na jamii za mitaani, washirika, wateja, na watumiaji katika kusaidia kushughulikia masuala ya taka na uchafu wa baharini.

## Mfilipino apania KO kwa Mwakinyo

**Mwandishi Wetu**

WAKATI bondia Mfilipino Arnel Tinampay akitarajiwa kuwasili nchini leo majira saaa 6:30 mchana na kupiga kambi ya siku 10 jijini Dar es Salaam kabla ya kuvaana na Hassan Mwakinyo, ametamba kumchakaza Mtanzania huyo kwa KO.

Tinampay na Mwakinyo watazichapa Novemba 29, mwaka huu katika pambano la raundi 10 la uzani wa super welter litakalopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam huku Rais John Magufuli akiombwa kuwa mgeni rasmi.

Mapema wiki iliyopita, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa bungeni mjini Dodoma aliwaomba Watanzania kujitokeza kwa wingi kumsapoti Mwakinyo katika pambano hilo lililobeba hisia za wadau mbalimbali wa michezo ndani na nje ya nchi.

Akiwa nchini, Tinampay ambaye ameambatana na kocha wake, Victor Man 'On fire' atafanya mazoezi ya wazi jijini Dar es Salaam kabla ya kuelekea Tanga, ambako atajifua kwenye Uwanja wa Tangamano na kisha kurejea Dar es Salaam kumkabili Mwakinyo.

Bondia huyo ambaye ni namba moja kwa ubora nchini Ufilipino, ametamba kumpiga kwa Knock Out, Mwakinyo katika ardhi ya Tanzania akisisitiza kuwa anafahamu ubora wa Mtanzania huyo ambapo amesema ana punchi nzito.

"Nimejiandaa kushinda, nitajaribu kumpiga kwa KO mpinzani wangu, lazima nikashinde Tanzania," alisema Tinampay muda mfupi kabla ya kuanza safri ya kuja Tanzania. Promota wa pambano hilo, Jay Msangi alisema Tinampay atakapowasili atafanya mazoezi ya wazi Mlimani City na Mbagala jijini Dar es Salaam kabla ya kuelekea Tanga ilipo kambi ya Mwakinyo ambako pia atafanya mazoezi ya wazi kisha kurejea Dar es Salaam tayari kwa pambano.

## Z'bar Queens yataja ukata kipigo Cecafa

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake Zanzibar (Zanzibar Queens), Muhamed Salaa amesema timu yake imeanza vibaya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge) kwa Wanawake yanayoendelea kwenye Uwanja wa Azam Complex Chamazi jijini Dar es Salaam, kutokana na ukata wa pesa.

Akizungumza kwa masikitiko kocha huyo, alisema hawawezi kufanya vizuri kutokana na kwamba hawajafanya maandalizi yoyote kama ilivyo kwa timu nyingine.

"Sisi hatujapewa kitu chochote kuanzia posho za wachezaji mpaka jezi za kuvaa tumeshindwa hata kuweka timu kambini kutokana na ukata tuliokuwa nao bila maandalizi huwezi kufanya vizuri," alisema.

Alisema katika mchezo wao wa kwanza Burundi walipata nafasi wakazitumia na hatimaye kuibuka na ushindi mnono wa mabao 5-0.

Alisema ataendelea kukinoa kikosi chake kwa ajili ya michezo ijayo na kuwataka wachezaji wake waongeze juhudi uwanjani ili waweza kumaliza katika nafasi nzuri.

# Michezo

Jumatatu Novemba 18, 2019

Nipashe




Alonso amtaja Guardiola sababu kuitosa Madrid HABARI UK 30

PASUA...



Mshambuliaji wa Coastal Union ya Tanga, Deogratius Anthony, akijaribu kupasua katikati ya mabeki wa Yanga, Ally Mtoni 'Sonso' na Juma Abdul (kulia) katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana na Yanga kushinda 3-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BALINYA, TSHISHIMBI WAIUA COASTAL USIKU

●●●Yanga yaanza kutulia dimbani, Molinga ashindwa kuonyesha ufundi wa penalti huku...

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, ameanza kuirejesha timu hiyo katika mstari baada ya jana angalau kuonyesha kucheza kwa kuelewana wakati wakiibanjua Coastal Union ya Tanga kwa mabao 3-1 kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mabao mawili ya usiku (yaliyofungwa dakika za nyongeza) yalitosha kwa Yanga kuibuka na ushindi wa 3-1, huku ikionyesha kucheza vizuri kwa kuonana tofauti na wakati ikiwa chini ya Mkongomani Mwinyi Zahera, aliyetimuliwa wiki mbili zilizopita.

Papy Tshishimbi alifunga bao la pili dakika ya pili ya nyongeza, baada ya uzembe wa mmoja wa mabeki wa Coastal Union kutaka kucheza mchezo wa kuotea na kumuacha mfungaji peke yake kabla ya kuukwamisha mpira wavuni.

Wakati zikitimia dakika nne zilizoonyeshwa kabla ya mechi kumalizika, Yanga ilipata penalti, baada ya beki mmoja wa Coastal kuukumbatia mpira katika harakati za kuokoa, iliyokwamishwa wavuni na Juma Balinya na kuifanya timu hiyo kuondoka na ushindi huo.

Kabla ya mabao hayo, Mrisho Ngassa aliisawazishia Yanga bao dakika ya 69, baada ya kuachia shuti kali akiwa nje ya eneo la hatari lililomshinda kipa Aboubakar Abbas na mpira ukajaa wavuni.

Lilikuwa ni la kusawazisha, baada Coastal kupata bao la kwanza dakika ya 44, wakati krosi ya Mudathir Said ilipomkuta Ally Mtoni 'Sonso' ambaye aliukwamisha mwenyewe wavuni katika harakati za kutaka kuuokoa.

Huenda Yanga ingeibuka na ushindi wa mabao manne kama David Molinga asingekosa penalti iliyotolewa kitatanishi na mwamuzi dakika ya 68, lakini kipa Aboubakar alipangua na kuwa kona tasa.

Kipindi cha kwanza Yanga ilifanya mashambulizi kadhaa, lakini hayakuwa makali. Shambulizi hatari zaidi lilikuwa ni dakika ya 29, Mapinduzi Balama alipoachia kombora kali nje ya eneo la hatari, lakini lilipanguliwa na kipa Aboubakar na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Mudathir Said akiwa nje kidogo ya eneo la hatari alipiga shuti kali lililodakwa kwa ustadi na kipa Farouk Shikalo.

Kipindi cha pili, Coastal walitumia muda mrefu kulinda lango lao na kuwapa mwanya wapinzani wao kushambulia muda mrefu wa mchezo.

Yanga iliwatoa David Molinga, Said Mussa, na nafasi zao zikachukuliwa na Ngassa na Balinya, huku Coastal wakimtoa Mohamed Mussa na nafasi yake ikachukuliwa na Haji Ugando, James Kahimba pia akitoka na nafasi yake kutwaliwa na Atoub Semtawa.

Mabadiliko hayo yaliisaidia zaidi Yanga, kwani wachezaji wake wawili walioingia waliweza kupachika mabao.

Baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, Novemba 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Yanga watavaana na JKT Tanzania kwenye mwendelezo wa Ligi Kuu Bara.

# Aussems atoa neno kipigo KMC

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU timu yake ikipoteza mchezo wa kirafiki juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema anahitaji kuona timu yake inashinda mechi nyingine tano mfululizo ili kurudisha kasi ya ushindi waliyokuwa nayo wakati wa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ulipoanza.

Simba ilikubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka KMC FC katika mchezo wa kirafiki uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex Chamazi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema hakufurahishwa na matokeo waliyopata katika mchezo huo wa kirafiki, lakini kiufundi umemsaidia kuwaimarisha wachezaji wake.

Alisema matokeo hayo yatawafanya pia wachezaji waliocheza kujipanga vizuri watakapopata nafasi nyingine ya kucheza katika mechi za kirafiki au zile za mashindano zinazoendelea.

Mbelgiji huyo alisema kila siku benchi la ufundi hutumia mechi wanazocheza kuimarisha idara zote za timu na huwaamsha zaidi pale wanapopoteza mchezo.

"Tuko katika mipango ya kujiimarisha, tunarekebisha na kuimarisha kila idara kwenye timu kulingana na kile tunachokiona katika mechi au kwenye mazoezi, naamini kila mmoja pia huweka mawazo kwenye kutorudia makosa kwa sababu wanajua malengo ya klabu na kila mmoja wetu, matumaini yangu tuko kwenye mstari mmoja," alisema Aussems.

Baada ya kumaliza mechi hiyo, Simba ambayo nyota wake wa kikosi cha kwanza wako katika timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Zambia na Rwanda, itakutana na Ruvu Shooting Novemba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini wakati siku moja kabla, watani zao Yanga watavaana na JKT Tanzania.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002